

KUFUNGUA MKUTANO

AGENDA ZA MKUTANO

**AGENDA ZA MKUTANO WA KAMATI YA USHAURI YA MKOA WA KIGOMA
TAREHE 13 OKTOBA, 2017**

1. Kufungua Mkutano.
2. Kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa tarehe 25 Novemba 2016 na Muhtasari wa Mkutano maalum uliyofanyika tarehe 17 Machi 2017.
3. Yatokanayo Muhtasari wa Mkutano wa tarehe 25 Novemba 2016 na Muhtasari wa Mkutano maalum uliyofanyika tarehe 17 Machi 2017.
4. Taarifa ya Mpango na Bajeti mwaka 2017/18 kama ilivyopitishwa na Bunge.
5. Taarifa za Maendeleo ya Kisekta:-
 - 5.1 Kilimo-Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Msimu wa 2016/2017 na maandalizi ya Kilimo Msimu wa 2017/2018
 - 5.2 Elimu- Utekelezaji wa shughuli za Elimu
 - 5.3 Maji- Hali ya Huduma ya Maji katika Mkoa
 - 5.4 Afya- Hali ya Utoaji wa Huduma za Afya katika Mkoa
6. Maombi ya Wilaya ya Uvinza kusajili msitu wa Masito kuwa Hifadhi inayosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza
7. Taarifa kutoka Wadau mbalimbali
 - 7.1 UNCHR- Utekelezaji wa shughuli za Wakimbizi
 - 7.2 UN- Program ya Pamoja ya Kigoma (Kigoma Joint Programme)
 - 7.3 TANESCO-Utekelezaji wa Mradi wa kusambaza umeme Vijijini
 - 7.4 TRA-Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2016/2017 na Malengo ya 2017/2018
 - 7.5 TPA-Uboreshaji wa Bandari ya Kigoma
8. Taarifa kuhusu MSM zinavyotekeleza maagizo ya Serikali ya kufanikisha Uchumi wa Viwanda
9. Mengineyo
10. Kufunga Mkutano

**KUTHIBITISHA
MUHTASARI WA
MKUTANO WA TAREHE
25 NOVEMBA 2016 NA
MUHTASARI WA
MKUTANO MAALUM
ULIYOFANYIKA TAREHE
17 MACHI 2017.**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) KILICHOFANYIKA
TAREHE 25 NOVEMBA, 2016 KATIKA UKUMBI WA NSSF - KIGOMA**

A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA

S/N JINA KAMILI

1. Brig Gen.(Rtd) Emmanuel Maganga
2. Eng. Aziz Mutabuzi
3. Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko
4. Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto
5. Mhe.Eng. Nditiye, Atashasta J.
6. Mhe. Hasna. S. K. Mwilima
7. Mhe. Josephina Genzabuke
8. Mhe. Peter Serukamba
9. Mhe. Zainabu Katimba
10. Mhe. Col. Marco E. Gaguti
11. Mhe. Samson A. Anga
12. Mhe. Col. Hosea M. Ndagala
13. Mhe. Mwanamvua Mrindoko
14. Mhe. Hussein Juma Ruhava
15. Mhe. Twallib S. Mangu
16. Mhe. Jackson T. Mateso
17. Mhe. Juma Maganga
18. Mhe. Enock G.Chobaliko
19. Mhe. Yohana Mshita
20. Mhe. Saimoni Kanguye
21. Judethadeus J. Mboya
22. Eng. Godfrey Kasekenya
23. Frank Magabiro
24. Adili C. Mlowe
25. Seif Salum
26. Fred Fandey
27. Lusubilo J. Mwakabibi
28. Hanji Y. Godigodi

CHEO/WADHIFA

- Mkuu wa Mkoa wa Kigoma -Mwenyekiti
- Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa - Katibu
- Mbunge - Kasulu Mjini
- Mbunge - Kigoma Mjini
- Mbunge - Muhambwe
- Mbunge – Kigoma Kusini
- Mbunge wa Viti Maalum
- Mbunge wa Kigoma Kaskazini
- Mbunge Viti Maalum
- Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe
- Mkuu wa Wilaya ya Kigoma
- Mkuu wa Wilaya ya Kakonko
- Mkuu wa Wilaya ya Uvinza
- Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji
- Mwenyekiti Halmashauri ya Mji Kasulu
- Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza
- Mwenyekiti H/Wilaya ya Kakonko
- Mwenyekiti H/Wilaya ya Kigoma
- Mwenyekiti H/Wilaya ya Kasulu
- Mwenyekiti H/Wilaya ya Kibondo
- Mkurugenzi Manispaa ya Kigoma/Ujiji
- Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kasulu
- Kaimu Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Uvinza
- Kaimu Mkurugenzi wa Mji wa Kasulu
- Kaimu Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kibondo
- Kaimu Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Buhigwe
- Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kakonko
- Mkurugenzi Mtendaji, H/Wilaya ya Kigoma

B. WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

1. Mhe. Vuma A. Holle - Mbunge wa Kasulu Vijijini
2. Mhe. Albert Obama Ntabaliba - Mbunge wa Buhigwe
3. Mhe. Bilago Kasuku Samson - Mbunge wa Buyungu
4. Mhe. Sabrina Sungura - Mbunge Viti Maalum
5. Mhe. Col. Martin E. Mkisi - Mkuu wa Wilaya ya Kasulu
6. Mhe. Louis P. Bura - Mkuu wa Wilaya ya Kibondo

C: WAJUMBE WA KUU MKOA

- | | |
|---------------------------|-----------------------------------|
| 1. DCP Ferdinand Mtui | Kamanda wa Polisi Mkoa |
| 2. SS Dismas J. Moshia | Kaimu Afisa Uhamiaji Mkoa |
| 3. Israel A Mwamale | Kaimu Afisa Usalama wa Taifa Mkoa |
| 4. Col. Mamdali M. Msuya | Mshauri wa Mgambo Mkoa |
| 5. Rafael Mbwambo | Kamanda wa TAKUKURU Mkoa |
| 6. ACP Leonard M. Burushi | Kaimu Afisa Magereza Mkoa RPO |

D: WATAALAM WA SEKRETARIETI YA MKOA

- | | |
|-----------------------------|---|
| 1. Samuel Z. Tenga | Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu |
| 2. Dr. Paul Chaote | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Afya |
| 3. Daniel L. Machunda | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Rasilimali Watu |
| 4. Jailos K. Pilla | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu |
| 5. Omary Mkombole | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Elimu |
| 6. Sotely M. Tundwe | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Menejimenti ya Serikali za Mitaa |
| 7. Deogratiasi Sangu | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji |
| 8. Adiriki F. Mohamed | Afisa Ugavi Mwandamizi |
| 9. Bw. Kwame A. Daftari | Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigoma |
| 10. Upendo G. Marango | Katibu Tawala wa Wilaya ya Uvinza |
| 11. Peter Masindi | Katibu Tawala wa Wilaya ya Buhigwe |
| 12. Zainabu S. Mbunda | Katibu Tawala wa Wilaya ya Kakonko |
| 13. Zilpa Kisonzela | Afisa Maendeleo ya Jamii |
| 14. Renatus S. Mukasa | Mchumi |
| 15. James Peter | Katibu wa Mkuu wa Mkoa |
| 16. Benard Mpakasi | Afisa Elimu Taaluma |
| 17. Eng. Zephania M. Yohana | Mhandisi wa Kilimo cha Umwagiliaji |
| 18. Noely A Byamungu | Afisa Mifugo |
| 19. Renfrida Joseph | Mkaguzi wa Ndani |
| 20. Waltruds R. Luvakubusa | Mwangelizi wa Ofisi |

E: VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA

- | | |
|---------------------------|-------------------------|
| 1. Dr. Amani W. Kabourou | Mwenyekiti wa CCM Mkoa |
| 2. Gervas Bahingai | Mwenyekiti NCCR Wilaya. |
| 3. Selemani Saidi Msanu | Kutoka CCK Mkoa |
| 4. Sendwe Ibrahim Mbaruku | Mwenyekiti ACT Mkoa |
| 5. Rehani M. Rehani | Katibu – DP |
| 6. Nuru S. Bashange | Katibu UMD |
| 7. Mandela Daniel | M/Kiti TADEA |
| 8. Frank L. Ruhasha | Katibu CHADEMA |
| 9. Sharon Joseph | Katibu ACT |
| 10. Adamu Muhama | Katibu CUF |

F: TAASISI ZA SERIKALI NA MASHIRIKA YA UMMA

- | | |
|--------------------------|--|
| 1. Josephati Rwegasila | Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa KUWASA |
| 2. Stephen Myamba | Mratibu wa Program ya EQUIP |
| 3. David H.Shunu | Meneja wa Mkoa Shirika la Nyumba |
| 4. Eng.Augustine Fashe | Kaimu Meneja wa Mkoa wa TANROADS |
| 5. Thobias Sijabaje | Mwakilishi wa Mratibu wa Kanda, Idara ya Wakimbizi |
| 6. Ramadhani Gange | TCCIA – Kigoma |
| 7. Donald K. Silaa | TFS Kasulu |
| 8. Gervas R. Ntahamba | Meneja wa Mkoa - SIDO - Kigoma |
| 9. Said Kirari | VETA – Kigoma |
| 10. Salehe S. Kurwa | TRA |
| 11. Emmanuel Adina | NHIF |
| 12. Teiding E. Mshiu | TPA |
| 13. Dr.James Mchemba | Manager BOT Mwanza |
| 14. Isabell Von Oertze | BTC KIGOMA |
| 15. Mwamini Masanja | BTC KIGOMA |
| 16. Phulumensi Kavumvuli | BTC KIGOMA |
| 17. Moses Kahero | Meneja NBS(M) |
| 18. Bakari S Mwichande | Meneja - FETA - Kigoma |

G: WATALAM KUTOKA HALMASHAURI

- | | |
|-----------------------|-------------------------------------|
| 1. Yotham J. Mkayamba | Afisa Mipango HW ya Uvinza |
| 2. Salome Mboya | Afisa Mipango HW Kigoma |
| 3. Lilian Mshanga | Afisa Mipango Manispaa Kigoma Ujiji |

H: WAWAKILISHI WA BARAZA LA WAZEE MANISPAA YA KIGOMA/UJJI

1. Kilonzo M. Dunia
2. Lt (Mst) Ramadhani A. Macheke
3. Hamza K. Sungura
4. Brambat A. Kiyola
5. Juma A. Juma

I: WAANDISHI WA HABARI

- | | |
|---------------------|----------------------|
| 1. Fadhili Abdallah | Gazeti la Habari leo |
| 2. Kassim Msoma | ITV |
| 3. Richard Katunka | STAR TV |

RCC 1/2016/2017/01: KUFUNGUA KIKAO

Kabla ya kufungua kikao rasmi, wajumbe na waalikwa wote walipewa fursa ya kujitambulisha kwa makundi kwa lengo la kufahamiana. Baada ya utambulisho Katibu wa kikao akatoa salamu zake na kisha kumkaribisha mwenyekiti ili kufungua kikao rasmi.

Mwenyekiti aliwakumbusha wajumbe kuwa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kipo kwa mujibu wa sheria na kwamba kinatumika kufanya tathimini ya masuala ya maendeleo kwa kupata taswira na hali halisi ilivyo ndani ya Mkoa. Aliwafahamisha wajumbe kuwa vikao vya RCC hufanyika mara mbili kwa mwaka kama hakuna dharura. Mwenyekiti aliwataarifu wajumbe kuwa kikao hicho kilikuwa ni kikao cha kwanza kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hivyo, aieleza kwa kifupi mambo yaliyopangwa kujadiliwa wakati wa kikao na kuwataka wajumbe kuwa huru kutoa mawazo yao na ushauri unaolenga kuboresha yaliyowasilishwa kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Mkoa wa Kigoma.

Mwenyekiti alieleza kuwa maendeleo ya Mkoa wa Kigoma yanategemea sana uboreshaji wa sekta za kiuchumi na kijamii kwa kuanza na vipaumbele vya Mkoa na Taifa. Alizitaka Halmashauri zote kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo na vya kati na kuweka mkakati wa kuyaendeleza kwa kushirikiana na SIDO Kigoma. Pia alizitaka Halmashauri kuweka mkakati wa kuwavutia wawekezaji hasa katika sekta za kilimo, uvuvi, ufugaji, na viwanda vya kuchakata mazao ili kuongeza thamani. Kwa kufanya hivyo wananchi wataongeza mapato na ajira zitaongezeka.

Mwenyekiti alipongeza mafanikio ya kitaaluma yaliyopatikana kwa ufaulu kuongezeka katika shule za msingi na sekondari. Aliwashukuru viongozi na watendaji waliochangia kupatikana kwa mafanikio hayo. Aidha viongozi na watendaji walitakiwa kuendelea kusimamia kikamilifu mpango wa serikali wa kutoa elimu bure kwa wanafunzi kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Akizungumzia suala la kujitosheleza kwa madawati, Mwenyekiti aliwafahammisha wajumbe kuwa Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa ambayo haijakamilisha kutekeleza agizo la Mhe. Rais la kujitosheleza kwa madawati kwa shule za msingi. Alisema Mkoa una upungufu wa madawati 25,539 sawa na asilimia 17. Hivyo Viongozi na watendaji walikumbushwa kuzingatia makubaliano yaliyofanyika katika kikao cha kazi cha tarehe 20 Novemba, 2016 juu ya kuondoa upungufu wa madawati uliobakia. Hata hivyo aliwaomba wadau wote kuchangia katika kuondoa upungufu wa madawati Mkoani.

Mwisho aliwataka viongozi na watendaji wote walioko Mkoani Kigoma kuongeza juhudi na ubunifu katika kutekeleza shughuli za umma ikiwa ni pamoja na kutafuta majibu ya kero za wananchi.

Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alitangaza kufungua kikao rasmi saa 4.08 asubuhi.

RCC 1/2016/2017/02: KUTHIBITISHA AGENDA

Wajumbe walithibitisha agenda za kikao baada ya kukubaliana na pendekezo kuwa taarifa za Shirika linalohudumia Wakimbizi (UNHCR) zinazohusu huduma kwa wakimbizi na miradi ya kusaidia jamii inayotekelezwa ziwe zinawasilishwa katika vikao vya RCC.

RCC 1/2016/2017/03: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 09 FEBRUARI, 2016

Kwa kuwa wajumbe walipewa muhtasari wa mkutano uliopita siku chache kabla ya kikao na kuusoma, Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari huo ukurasa kwa ukurasa ili kufanya masahihisho. Hata hivyo hakuna makosa yaliyoonekana na muhtasari ulithibitishwa kuwa kumbukumbu sahihi.

RCC 1/2016/2017/04: YATOKANAYO NA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 09 FEBRUARI, 2016.

Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya mkutano uliopita ilisomwa azimio moja baada ya linguine pamoja na utekelezaji wake. Wajumbe walichangia na kuhoji maeneo yaliyohitaji ufafanuzi zaidi na pia kushauri kama ifutavyo:-

- Zao la Kahawa ni zao muhimu katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Kigoma, hivyo wataalamu wa kilimo watambue maeneo yanayofaa kwa kilimo cha kahawa kisha kuzalisha mbegu zinazokidhi mahitaji kwa kila wilaya.
- Ili kuimarisha uchumi wa mwananchi mmoja mmoja kupitia kilimo, ushauri ulitolewa kuwa nguvu zaidi zielekezwe katika uboreshaji wa zao la chikichi kwa kuandaa mpango endelevu.
- Ili kuendana na msimu wa kilimo wananchi wasisubiri mbolea ya ruzuku bali watumie mbolea za asili na kutoka vyanzo vingine kuanza uzalishaji. Aidha, wananchi waelimishwe kuzalisha mazao yanayostahimili ukame hasa katika kipindi cha upungufu wa mvua.
- Ili kuimarisha na kuboresha utendaji na ufanisi katika elimu, changamoto za uchakavu wa miundombinu hasa madawati na nyumba za walimu zitatuliwe kwa ushirikano baina ya watendaji na wananchi kwa kutumia rasilimali zilizopo Mkoani, ikiwemo matumizi sahihi ya rasilimali za misitu.

RCC 1/2016/2017/05: TAARIFA YA MPANGO NA BAJETI MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOPITISHWA NA BUNGE

Taarifa ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/2017 kama ilivyopitishwa na Bunge iliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe. Mwasilishaji alieleza kuwa Mkoa wa Kigoma uliwasilisha katika ngazi ya Taifa maombi ya sh. 211,359,000,000 ambapo kati ya fedha hizo: mishahara zilikuwa

sh.152,637,403,000; matumizi mengineyo sh. 19,384,554,000; fedha za maendeleo sh. 35,485,693,000 na vyanzo vya ndani vya Halmashauri sh. 9,981,714,000.

Fedha zilizoidhinishwa ni sh. 179,499,899,000 kama ifuatavyo: mishahara sh. 126,134,165,000; matumizi mengineyo sh. 13,663,319,000; vyanzo vya ndani MSM sh. 9,981,714,000 na fedha za maendeleo ni sh. 29,714,892,000. Wajumbe waliipokea taarifa hiyo.

RCC 1/2016/2017/06: UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KILIMO- HALI YA CHAKULA NA UPATIKANAJI WA PEMBEJEO

Taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuwa Mkoa unakadiriwa kuwa na eneo linalofaa kwa kilimo la hekta 2,668,630 (sawa na asilimia 34). Ilielezwa kuwa mahitaji ya chakula katika Mkoa yamekuwa yakiongezeka kila mwaka kutokana na ongezeko la watu. Msimu wa mwaka 2015/2016 Mkoa ulilenga kulima hekta 702,330 za mazao ya chakula, tathimini iliyofanyika mwisho wa msimu ilibaini kuwa hekta zilizolimwa zilikuwa 637,320 na kuzalisha tani 1,295,713 sawa na asilimia 78 ya lengo la uzalishaji. Kutokana na mazao yaliyopatikana Mkoa ulikuwa na ziada ya tani 596,429. Hata hivyo ilionekana kuwa upungufu unaweza kujitokeza kutokana na mikoa ya jirani kutokuwa na chakula cha kutosha.

Kwa upande wa pembejeo ilielezwa kuwa Mkoa ulipata mbolea ya kupandia tani 3,700, mbolea ya kukuzia tani 3,700; mbegu za mahindi tani 702 na mbegu za mpunga tani 57. Kaya zilizolengwa kwa musimu wa 2015/2016 ni 74,000. Kwa msimu wa 2016/2017 Mkoa umepata tani 900 za mbolea ya kukuzia na tani 90 mbegu za mahindi ambapo kaya zilizolengwa ni 18,000. Mgao huo ni mdogo ukilinganisha na msimu uliopita kutokana na mabadiliko ya mfumo wa utaratibu wa kutoa pembejeo za ruzuku.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliijadili na kueleza kuwa taarifa inakosa maelezo ya kuendeleza zao la chikichi ambalo kwa mwaka zinapatikana takribani tani 30 za mawese. Walitaja baadhi ya changamoto za kuendeleza zao hili ni kukosekana kwa sera ya kilimo cha chikichi, kituo cha utafiti wa zao hili na pia kukosekana Bodi ya zao la Mawese. Hivyo wajumbe walishauri kikao kijacho kuwepo maelezo ya mkakati wa kuboresha zao la chikichi Mkoani Kigoma ili kuendeleza wakulima wa zao hilo. Aidha, walishauri Mkoa kuandaa andiko la kuendeleza zao la chikichi na andiko hilo lijadiliwe na wadau. Pia walishauri kuwa kwa mwaka huu ambao mvua zinaonekana kuwa kidogo, wananchi washauriwe kulima mazao yanayohimili ukame.

RCC1/2016/2017/07: SERA YA ELIMU YA MWAKA 2014 ILIYOANZA KUTEKELEZWA MWAKA 2016

Mada iliwasilishwa kwa kueleza sababu na chanzo cha kuhuisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Mambo muhimu yaliyomo katika sera hiyo kuwa ni:

- Kurekebisha muda wa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali ili kuleta tija, ufanisi na matumizi bora ya rasilimali.

- Kuinua ubora wa mitaala ya elimu na mafunzo ili kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa.
- Kuendeleza matumizi ya lugha ya kiswahili, kiingereza, alama, pamoja na lugha nyingine za kigeni.
- Kutoa fursa za elimu na mafunzo kwa usawa,
- Kwenda sambamba na mahitaji ya rasilimali watu kulingana na vipaumbele vya Taifa.
- Kuwa na mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini.
- Kuwa na usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini.

Pamoja na hayo ulitolewa ulinganisho wa sera ya elimu ya mwaka 1995 na sera ya mwaka 2014. Mada ilihitimishwa kwa kueleza kuwa madhumuni ya sera ni kutoa mwongozo wa ujumla wa uendeshaji wa elimu na mafunzo kwa mtizamo wa Dira ya Taifa 2025 na mabadiliko ya ulimwengu katika nyanja mbalimbali.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo.

RCC 1/2016/2017/08: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2015/2016 NA ROBO YA KWANZA 2016/2017

Taarifa ilieleza kuwa mwaka **2015/2016** Mkoa uliidhinishiwa sh. 48,417,935,260 kupitia fungu 74. Pia Mkoa ulikadiri kupokea fedha za miradi sh. 39,138,657,190 kupitia OR TAMISEMI, Wizara za Kisekta na wadau walioko katika Mkoa wa Kigoma.

Fedha zilizopokelewa kutoka Hazina ni sh. 14,608,001,210 ambazo ni sawa na 30% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yalikuwa sh. 10,971,951,733 sawa na 75% ya fedha zilizopokelewa Aidha, fedha zilipokelewa kutoka OR TAMISEMI, Wizara za Kisekta na wadau wengine ni sh. 25,969,224,222 na matumizi yalikuwa sh. 19,900,740,019 sawa na 51% ya fedha zilizoidhinishwa. Utekelezaji kimaumbile kwa Mkoa wote ulifikia wastani wa 23%.

Kwa mwaka wa fedha wa **2016/17** Mkoa uliidhinishiwa sh. 35,948,089,000 katika bajeti ya maendeleo kupitia fungu 74. Aidha, sh. 33,910,382,377 ziliidhinishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia OR-TAMISEMI na Wizara za Kisekta na wadau wengine wa maendeleo.

Fedha zilizopokelewa kutoka Hazina kufikia Septemba 30, 2016 zilikuwa sh 364,567,824 sawa na 1% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh. 120,086,000, sawa na 32.9% ya fedha zilizopokelewa.

Aidha, kwa kipindi hicho Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea sh. 4,694,369,656 kupitia OR TAMISEMI, Wizara za Kisekta na wadau wengine na matumizi ni sh. 3,501,241,585 sawa na 74.6% ya fedha fedha zilizopokelewa.

Baada ya maelezo hayo wajumbe walipitishwa kwenye majedwali yanayoonesha muhtasari wa utekelezaji wa miradi ya mwaka 2015/2016 na robo ya kwanza ya mwaka 2016/2017. Taarifa ilihitimishwa kwa kueleza changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya mwaka 2015/16 na mwaka 2016/17. Taarifa ilipokelewa na wajumbe.

Aidha, baada ya majadiliano ilisisitizwa kuwa wataalamu waende vijijini kushughulikia miradi na matatizo ya wananchi. Hata hivyo ilionekana kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika Mkoa wa Kigoma. Hivyo, ushauri ulitolewa kuwa uchambuzi ufanyike kujua wanaohitajika na upungufu uliopo ili kuomba ajira mpya Serikalini.

Mwishoni wajumbe walitaka taarifa za Hali ya Afya, Hali ya Maji na Hali ya Umeme Vijijini zilandaliwe na kuwasilishwa katika kikao kijacho ili kuonesha maendeleo ya sekta hizo.

RCC 1/2016/2017/09: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAM YA TASAF III.

Taarifa iliwasilishwa kwa kueleza kuwa Program ya TASAF Awamu ya Tatu (TASAF III) ni mwendelezo wa mpango uliokuwepo kwenye TASAF awamu ya kwanza na ya pili. TASAF III inaboresha mafanikio ya TASAF awamu ya kwanza na ya pili na itatekelezwa kwa miaka 10 katika awamu mbili za miaka mitano mitano. Mwasilishaji alieleza kwa muhtasari madhumuni ya mpango, sehemu kuu za TASAF III, mzunguko wa mpango na utekelezaji wa mpango huo katika Mkoa wa Kigoma. Pia alieleza idadi ya kaya zinazonufaika na mpango ni kama ifuatavyo: mwaka 2014/15 kaya 22,417; mwaka 2015/16 kaya 70,817 na mwaka 2016/17 kaya 60,467. Fedha zilizopokelewa ni sh. 21,442,671,044/= ambazo ni kwa ajili ya walengwa na usimamizi. Pia taarifa ilieleza mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa program hii.

Kikao kiliwataka Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kuhakikisha kuna usalama wa fedha za walengwa ambazo zinalipwa tasilimu. Pia ushauri ulitolewa kwamba kila baada ya miaka 3 ifanyike tathimini ya kuona namna walengwa wanavyonufaika na mradi na kuondokana na umaskini.

RCC 1/2016/2017/10: TAARIFA KUTOKA MASHIRIKA MBALIMBALI

1) BENKI KUU KANDA YA ZIWA – MWENENDO WA UCHUMI KANDA YA ZIWA KWA MWAKA 2015/16

Katika mada hii, mtoa mada alieleza mwenendo wa ukuaji wa Uchumi kanda ya Ziwa kwa kuelezea pato la Mikoa ya Kanda ya ziwa ukiwepo na Kigoma; wastani wa pato la mtu mmoja mmoja; utendaji kissekta ambapo alielezea sekta kuu na mazao yanayozalishwa na kuuzwa nje ya nchi. Alieleza kuwa zao la pamba liliuzwa kwa asilimia 99, madini asilimia 95, uvuvi asilimia 90 na mifugo (ngozi) asilimia 42. Taarifa ilionesha uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao ya biashara katika sekta ya kilimo.

Aidha, alieleza idadi ya mifugo iliyouzwa, uvuvi na uzalishaji katika viwanda vya samaki. Katika Sekta ya madini aliwataja wachimbaji wakubwa na madini yanayochimbwa ambayo ni dhahabu, almasi, shaba, fedha na chumvi. Suala la utalii lilielezwa kwa kuonesha jinsi watalii walivyochangia mapato katika kanda ya ziwa.

Mtoa mada alieleza pia ukusanyaji wa kodi ya mapato, huduma za fedha na mabanki ambazo zilipungua kwa asilimia 8.2 na riba ya mikopo ilipungua kwa asilimia 0.37 na kwamba riba zilizotozwa kwa mwaka mzima zilipunguzwa kutoka wastani wa asilimia 18.85. na kufikia asilimia 17.09 kwa mwaka 2015.

Alihitimisha taarifa yake kwa kueleza kuwa uzalishaji katika viwanda vya minofu ya samaki unaendelea kushuka na kwa sasa viwanda vinazalisha kwa asilimia 50 ya uwezo wake. Alisema hii ilisababishwa na uvuvi usiokuwa na mpangilio, matumizi ya zana haramu za uvuvi na uharibifu wa mazingira na mazalia ya samaki. Alitoa mapendekezo kuwa sheria za uvuvi na ulinzi wa mazingira zifuatwe. Wavuvi wahamasishwe kujiunga na kutumia mikopo ya mabanki ili kuwawezesha kupata zana bora za kisasa za uvuvi. Alipendekeza kuendeleza ufugaji wa samaki katika mabwawa ili kupunguza utegemezi katika uvuaji wa samaki wa asili.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kutaka hoja iliyojadiliwa katika mkutano uliopita kuhusu kuanzisha tawi la Benki Kuu Kanda ya Magharibi katika Mkoa wa Kigoma ifuatiliwe.

2) TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA SIDO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2015/2016 NA ROBO YA KWANZA 2016/2017.

Mtoa mada alianza kuwasilisha taarifa yake kwa kueleza historia fupi ya kuanzishwa kwa shirika la SIDO. Alitaja walengwa katika huduma za SIDO kuwa ni viwanda na biashara ndogo na za kati, Wajasiriamali chipukizi na mashirika au taasisi zinazosaidia wajasiriamali. Huduma kuu zinazotolewa na SIDO ni zifuatazo:

- Uendelezaji wa teknolojia
- Mafunzo ya biashara na huduma za ugani
- Huduma za kifedha na
- Kuhabarisha walengwa juu ya masoko.

Alieleza shughuli zilizofanywa na shirika la SIDO kwa mwaka 2016/2017 kipindi cha robo mwaka ni zifuatazo:

- Uendelezaji wa teknolojia ambapo mashine 56 zilitengenezwa; kituo cha SIDO Kigoma kilisaidia vifaa bora vya kufanyia kazi; kutoa mafunzo kwa vikundi 50 vya mafundi mchundo kutoka Manispaa ya Kigoma/Ujiji na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na kuimarisha kongano (cluster) iliyoko SIDO yenye viwanda vidogo 48 vilivyoajiri watu zaidi ya 300.

- Kutoa mafunzo ya kibiashara na vitendo ambapo watu 2,248 walipatiwa mafunzo wakiwemo wanawake 1,499 na wanaume 749 katika maeneo 56 Mkoani Kigoma. Mafunzo yaliyotolewa yalikuwa ni ujasiriamali, utengenezaji wa sabuni, usindikaji na mafunzo ya mikopo.
- Kutoa huduma za kifedha kwa wajasiriamali 293 (wanawake 189 na wanaume 104) ambao walipata mkopo wa sh. 385,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kipindi cha Julai Septemba 2016 wajasiriamali wadogo 83 (wanawake 54 na wanaume 29) walikopeshwa sh. 134,300,000/= na wajasiriamali 23 waliunganishwa na taasisi za fedha ili waweze kukopa fedha kwa wale wanaohitaji kiasi kinachozidi milioni 5,000,000/=.
- Kuhusu masoko, Wajasiriamali 11 waliwezesha kushiriki maonesho mbalimbali ya biashara ndani na nje ya nchi zikiwemo Rwanda na Kenya. Shirika limefanya maonesho ya bidhaa za wajasiriamali kanda ya kati yaliyofanyika Mkoani Tabora na wajasiriamali 22 kutoka Kigoma walishiriki.

Alihitimisha mada yake kwa kueleza mkakati wa SIDO wa kuendeleza viwanda vidogo ngazi ya Wilaya kuwa ni kutumia kongano (cluster) ambayo ni kusanyiko la shughuli zinazoshabihiana, zinazofanyika eneo moja ili kuweza kusaidia ukuaji wa sekta husika. Aidha alieleza kuwa SIDO iliandaa mkakati wa kuendeleza kongano ambayo inaitaka kila Halmashauri kutenga eneo ambalo wataanzisha viwanda vidogo na vya kati.

Wajumbe walipokea taarifa ya SIDO na kulitaka shirika hilo kupanua wigo wa shughuli zake katika wilaya zote kwa sababu ilionekana wamejikita zaidi katika wilaya ya Kigoma na kwa kiasi kidogo katika wilaya ya Kasulu.

3) MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA MKOA KWA UFADHILI WA BTC MWAKA 2015/2016 NA MWAKA 2016/2017

Taarifa ya miradi inayotekelezwa katika Mkoa wa Kigoma kwa ufadhili wa Serikali Ubeligiji kupitia shirika la BTC na hatua iliyofikiwa iliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe. Ilielezwa kuwa shirika la BTC linafadhili miradi Mikoa ya Kigoma, Pwani, Dodoma na Tanga. Katika Mkoa wa Kigoma shirika lilianza kufadhili mradi wa kuhifadhi mazingira katika Wilaya zote sita.

Aidha mwaka huu wa 2016/17 umeanzishwa mradi wa Kilimo unaolenga kuongeza mnyororo wa thamani ya mazao ya wakulima ujulikanao *Sustainable Agriculture Kigoma Regional Project (SAKiRP)*. Pamoja na kilimo pia itatekelezwa miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa kushirikiana na wananchi hususan vikundi vya watumiaji wa maji (COWSO).

Katika majadiliano wajumbe walipongeza jitihada zinazofanywa na Serikali ya Ubeligiji katika kusaidia maendeleo katika Mkoa wa Kigoma na Tanzania kwa ujumla. Walieleza juu ya umuhimu wa mradi kuwa na matokeo yanayoonekana kwa wananchi. Wajumbe walisistiza umiliki wa miradi hiyo uwe wa

Halmashauri, hivyo kila Halmashauri ihakikishe inaelewa vizuri miradi yote inayofadhiliwa na BTC katika eneo lake.

4) SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA ASASI YA WEGCC MKOANI KIGOMA

Mratibu wa asasi hii alianza kwa kueleza kuwa **WEGCC** ni Baraza la Kuratibu na Kukuza Maendeleo na Mahusiano ya Jamii Kijinsia na kwamba ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania. Makao yake makuu ni Arusha, na Shirika hilo linafanya kazi zake Tanzania Bara ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Ofisi ya WEGCC Mkoa wa Kigoma ipo Wilaya Kasulu eneo la Mwilamvya.

Alieleza malengo ya shirika ni pamoja na kuiwezesha jamii kutambua na kuthamini mchango wa watu wote (wanawake na wanaume) katika maendeleo ya jamii na kiuchumi na kuwawezesha wanawake kujiamini na kutambua wajibu na nafasi zao katika jamii.

Alieleza kuwa shirika linafanya kazi katika Wilaya zote sita za Mkoa wa Kigoma. Alitaja miradi iliyotekelezwa, miradi inayotarajiwa kutekelezwa na wafadhili waliotoa fedha.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na walishauri kuwa kuwepo utaratibu wa kutembelea na kukagua shughuli za asasi zisizo za kiserikali kwani fedha wanazopewa ni kwa ajili ya shughuli za wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Lengo ni kuzifahamu shughuli zao kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Mkoa.

5) SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA ASASI YA KIVIDEA- KIGOMA.

Mratibu wa asasi hiyo alieleza kuwa KIVIDEA (Kigoma Vijana Development Association) ni shirika ambalo lilianza mwaka 1999 na linajishughulisha na watoto wa miaka 3 - 14 na vijana wa miaka 15 – 24 likiwa limejikita kwa watoto na vijana wasiojiweza katika ngazi ya vijiji na mtaa. Alieleza malengo ya shirika kuwa ni kuwawezesha vijana kuwa na maamuzi sahihi katika maisha na kushiriki katika shughuli za maendeleo yao.

Alieleza kuwa shirika lina watoto wasiojiweza 120 ambapo watu wazima 528 wanaojitolea kuhudumia watoto 18. Shirika lina wafanyakazi (waelimisha rika) 48 katika kata 16 za Halmashauri 8 yaani 3 kila kata. Shirika la KIVIDEA linafanyakazi na vijana walioko shuleni na nje ya shule, wanawapa stadi za maisha kwa kutumia waelimishaji rika. Pia mratibu aliwataja wafadhili wa shirika na kiasi cha fedha walichopata. Alisema shughuli wanazoendelea nazo kwa mwaka 2016/17 kuwa ni pamoja na masuala ya kompyuta, kujengea uwezo vijana, kutoa elimu na uelewa wa umuhimu wa uzazi wa mpango kwa kushirikiana na shirika la Engender Health.

Wajumbe walipokea taarifa ya KIVIDEA na kulitaka shirika hilo kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za NGOs na watoe taarifa ya shughuli wanazotekeleza kwa Serikali.

6) FURSA ZILIZOPO MANISPAA YA KIGOMA UJJI.

Taarifa iliwasilishwa na ilieleza kuwa Manispaa ya Kigoma imeandaa wasifu wa fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika eneo lake. Pia wameandaa mwongozo kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza eneo la Manispaa. Taarifa ilieleza kuwa huu ni mkakati wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji katika kuvutia wawekezaji na kushirikisha wananchi kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizopo.

Taarifa ilipokelewa na wajumbe.

RCC 1/2016/2017/11: MENGINEYO

Katika agenda hii lilijitokeza suala la wakimbizi kuharibu mazingira kwa kukata miti kwa wingi kwa ajili ya kuni na kujengea katika maeneo wanayoishi. Mratibu wa masuala ya wakimbizi wa Wizara ya Mambo ya Ndani alieleza mkakati uliopo wa kunusuru misitu katika maeneo yenye wakimbizi.

Alisema kuwa katika wilaya ya Kasulu inazalishwa miche ya miti 1,000,000 na Kakonko miche 800,000 ambayo itapandwa ambapo kila kaya itapatiwa na kupanda miche 5. Alisema pia uliandaliwa mpango wa kutoa majiko ya gesi kwa kaya 3,000 za wakimbizi kwa kuanzia na kaya 15,000 walijenga nyumba na vyoo kwa matofali ili kupunguza matumizi ya miti. Pia alisema yapo mashirika ambayo yamepewa jukumu la kusimamia hifadhi ya mazingira katika makambi yote.

RCC 1/2015/2016/12: KUFUNGA KIKAO

Akifunga kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote pamoja na wadau wote walioalikwa na kufika kushiriki katika kikao. Alieleza kuwa wajumbe na washiriki wametimiza wajibu wao kwa kujadili kwa kina mada zilizowasilishwa kwenye kikao, lengo likiwa ni kutoa mawazo ya kuwezesha Mkoa wa Kigoma kusonga mbele kimaendeleo.

Mwenyekiti alieleza kuwa watendaji wa Serikali waliopo sasa karibu wote ni wapya na kwa upya huo wananchi wanategemea mabadiliko chanya katika maeneo waliyokabidhiwa. Alisema ni muhimu kuanzisha kituo cha matrekta katika Mkoa kwa ajili ya kupanua kilimo. Alisema idadi ya trekta zilizopo Mkoani ni chache, mfano Wilaya za Uvinza na Buhigwe wana trekta moja moja hivyo hazitoshi, na aliwataka wataalamu kuandika andiko ili yapatikane matrekta kwa kila Wilaya. Aliongeza kuwa kujitoshleza kwa chakula peke yake haitoshi. Kinachotakiwa sasa ni kuzalisha ziada kwa ajili ya maendeleo. Alisema Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa mikoa ambayo inapata fedha nyingi kupitia miradi na programu kama TASAF, EQUIP, BTC na LIC, hivyo akataka fedha hizo zitumike vizuri kuendeleza Mkoa wa Kigoma

Alieleza umuhimu wa kutumia pembejeo bora na kwa wakati ili kuleta tija katika kilimo. Aliagiza vifaa vya wananchi vilivyokamatwa katika eneo la hifadhi ya Taifa (pikipiki 5, baiskeli 800 na majembe 400

vipelekwe mahakamani ili viuzwe. Kama kuna waliojenga msituni, wasimamishe ujenzi huo na wananchi waambiwe kuwa hawatakiwi kujenga au kulima katika misitu.

Akizungumzia malalamiko kuwa kuna wananchi wanapigwa wanapokamatwa katika misitu, alisistiza kuwa hakuna anayefiki mwananchi kupigwa. Ikibainika kuwa jambo hilo limefanyika na kukawa na ushahidi hatua za kisheria zichukuliwe mara moja.

Mwisho alipongeza mafanikio katika sekta ya elimu na kwamba vijana wahimizwe kuongeza bidii kwani elimu ndiyo mkombozi wao. Aliwatakia wajumbe na washiriki sikukuu njema za Krisimas na Mwaka mpya wa 2017. Aliwashukuru tena wajumbe na washiriki wote na kuwatakia safari njema wote waliotarajia kusafiri kurudi katika maeneo yao.

Alifunga kikao saa 2.50 usiku.

Muhtasari Umethibitishwa na:

.....
Mwenyekiti

.....
Katibu

.....
Tarehe

**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA KILICHOFANYIKA
KATIKA UKUMBI WA OFISI YA MKUU WA MKOA WA KIGOMA TAREHE 17 MACHI, 2017**

A) WAJUMBE WALIOHUDHURIA

NA.	JINA KAMILI	CHEO/WADHIFA
1.	Mhe. Brig Gen.(Mst) Emmanuel Maganga	Mkuu wa Mkoa wa Kigoma - Mwenyekiti
2.	Mhe Charles A. Pallangyo	Katibu Tawala wa Mkoa - Katibu
3.	Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko	Mbunge - Kasulu Mjini
4.	Mhe. Kabwe Zuberi Ruyagwa Zitto	Mbunge - Kigoma Mjini
5.	Mhe. Samson A. Anga	Mkuu wa Wilaya ya Kigoma
6.	Mhe. Col. Marco E. Gaguti	Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe
7.	Mhe. Louis Peter Bura	Mkuu wa Wilaya ya Kibondo
8.	Mhe. Col. Hosea M. Ndagala	Mkuu wa Wilaya ya Kakonko
9.	Mhe. Hussein Juma Ruhava	Meya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji
10.	Mhe. Twallib S. Mangu	Mwenyekiti H/Mji wa Kasulu
11.	Mhe. Bwami J. Mathias	Makamu Mwenyekiti H/Wilaya ya Kigoma
12.	Mhe. Yohana Mshita	Mwenyekiti H/Wilaya ya Kasulu
13.	Mhe. Saimoni Kanguye	Mwenyekiti H/Wilaya ya Kibondo
14.	Mhe. Salome Luhingulanya	Kny Mwenyekiti H/Wilaya ya Uvinza
15.	Mhe. Juma Maganga	Mwenyekiti H/Wilaya ya Kakonko
16.	Mhe. Elisha Bagwanya	Mwenyekiti H/Wilaya ya Buhigwe
17.	Bw. Judethadeus J. Mboya	Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji
18.	Bibi. Fatina H. Laay	Mkurugenzi wa Mji wa Kasulu
19.	Eng. Godfrey Kasekenya	Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kasulu
20.	Bibi. Hanji Y. Godigodi	Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kigoma
21.	Bw. Juma A. Mnwele	Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kibondo
22.	Bw. Anosta L. Nyamoga	Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Buhigwe
23.	Bw. Lusubilo J. Mwakabibi	Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Kakonko
24.	Bw. Weja L. Ng'olo	Mkurugenzi Mtendaji H/Wilaya ya Uvinza

B. WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

1.	Mhe.Eng. Atashasta. J. Nditiye	Mbunge wa Muhambwe
2.	Mhe. Hasna. S. K. Mwilima	Mbunge wa Kigoma Kusini
3.	Mhe. Josephina Genzabuke	Mbunge wa Viti Maalum
4.	Mhe. Peter Serukamba	Mbunge wa Kigoma Kaskazini
5.	Mhe. Zainabu Katimba	Mbunge Viti Maalum
6.	Mhe. Vuma Holle	Mbunge wa Kasulu Vijijini
7.	Mhe. Albert Obama Ntabaliba	Mbunge wa Buhigwe
8.	Mhe. Bilago Kasuku Samson	Mbunge wa Buyungu
9.	Mhe. Sabrina Sungura	Mbunge Viti Maalum
10.	Mhe. Mwanamvua Mrindoko	Mkuu wa Wilaya Uvinza

C. WATAALAM WA SEKRETARIETI YA MKOA

- | | |
|-------------------------|---|
| 1. Samuel Z. Tenga | Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu |
| 2. Moses D. Msuluzya | Katibu Tawala Msaidizi Menejimenti ya Serikali za Mitaa |
| 3. Daniel L. Machunda | Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Utumishi |
| 4. Jailos K. Pilla | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu |
| 5. Robinson M. Wanjala | Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mali |
| 6. Omary Mkombole | Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Elimu |
| 7. Adiriki F. Mohamed | Afisa Ugavi |
| 8. Zilpa Kisonzela | Afisa Maendeleo ya Jamii |
| 9. James Peter | Katibu wa Mkuu wa Mkoa. |
| 10. Gabriel Ng'honoli | Afisa Habari |
| 11. Jesca Festo | Mwanasheria, |
| 12. Lundgreen J. Mcharo | Mahasibu wa Mkoa. |
| 13. Sotely M. Tundwe | Afisa Serikali za Mitaa |
| 14. Kwame A. Daftari | Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigoma |
| 15. Upendo G. Marango | Katibu Tawala wa Wilaya ya Uvinza |
| 16. Peter N. Masindi | Katibu Tawala wa Wilaya ya Buhigwe |

D. WATAALAM KUTOKA HALMASHAURI ZA WILAYA

- | | |
|-------------------|---|
| 1. Alex Ntiboneka | Afisa Mipango Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma |
| 2. Salum Mandai | Afisa Mipango Halmashauri ya Manispaa Kigoma/ Ujiji |

E. VIONGOZI NA WATAALAM KUTOKA TAASISI ZA UMMA.

- | | |
|-------------------------|--|
| 1. Obadia Jonas Nselu | Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi Mkoa |
| 2. Edmund Novaita | Mwakilishi wa Ofisa Uhamiaji Mkoa |
| 3. Meja Suleiman Kassim | Mshauri wa Mgambo Mkoa |
| 4. Frank Ndamizwe | Mwakilishi wa Kamanda wa TAKUKURU Mkoa |
| 5. George Mwasalyanda | Kaimu Mkuu wa Magereza Mkoa |
| 6. Israel Mwamale | Kaimu Afisa Usalama wa Taifa Mkoa |
| 7. Miriam J. Buyekwa | Kutoka NIDA-Kigoma |
| 8. Marco Maige | Kutoka NIDA- Kigoma |
| 9. Tandika S. A | Meneja NSSF |
| 10. Suleyman Abdulaziz | Afisa Mwendeshaji Shirika la FELISA |
| 11. Victor E.D.Msuya | Kutoka TRA – Kigoma |
| 12. Edwin D. Ulikaye | Kutoka TRA – Kigoma |
| 13. Dr Hashim Hongo | Mkurugenzi Shirika la FELISA |
| 14. Eng. Narcis Choma | Meneja wa Mkoa TANROADS –Kigoma |
| 15. Karonda S | Meneja wa Mkoa TEMESA - Kigoma |
| 16. Mbike Jones | Mwakilishi - KUWASA |
| 17. Stephen Myamba | Mratibu wa Program ya EQUIP- Kigoma |
| 18. Gervas R. Ntahamba | Meneja wa Mkoa - SIDO - Kigoma |

- | | |
|------------------------|-------------------------------|
| 19. Said Kirari | Kutoka Chuo cha VETA – Kigoma |
| 20. Emmanuel Adina | Meneja wa Mkoa, NHIF |
| 21. Bakari S Mwichande | Meneja wa Mkoa, FETA |
| 22. Benard Marwa | SUMATRA - KIGOMA |
| 23. Salum Kangeta | Mwenyekiti BAKWATA (M) |

F. VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA

- | | |
|---------------------------|--------------------------|
| 1. Naomi Kapambala | Katibu wa CCM Mkoa |
| 2. Sendwe Ibrahim Mbaruku | Mwenyekiti ACT Wazalendo |

G. WAANDISHI WA HABARI

- | | |
|---------------------|-----------------------|
| 1. Jacob E Ruvilo | Azam TV |
| 2. Abel Daudi | Azam TV (mpiga Picha) |
| 3. Egidius Adax | TBC1 |
| 4. Fadhili Abdallah | Gazeti la Habari leo |
| 5. Kassim Msoma | ITV/Radio One |
| 6. Yoctan Ngelly | The Guardian |
| 7. Antony Kayanda | Gazeti la Mwananchi |

MUHT. 1: KUFUNGUA KIKAO

Kabla ya kikao kufunguliwa Katibu wa kikao aliwatambulisha Wajumbe na wageni waalikwa kwa makundi na kisha aliwaeleza wajumbe kuwa agenda kuu ya kikao ilikuwa ni kujadili mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/2018. Baada ya maelezo hayo mafupi, Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao.

Mwenyekiti alianza kwa kueleza kuwa, kikao hicho kilipaswa kifanyike mapema kabla ya mpango na bajeti kuwasilishwa Wizarani lakini muda ulikuwa mfupi. Aliwakumbusha wajumbe kuwa mpango na bajeti inayowasilishwa ilishajadiliwa ngazi ya Halmashauri kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango, hivyo wajumbe wana uelewa wa yale yaliyojadiliwa na kupitishwa katika Halmashauri zao na kwamba hilo litafanya mjadala katika kikao usiwe mirefu.

Aliwajulisha Wajumbe kuwa msingi wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa ni kuleta maendeleo. Alieleza kuwa kuna mambo mengi yanayohitaji kusukumwa na Kamati hii kwa faida ya Wananchi wa Kigoma. Alieleza Katika Mkoa kuna mashirika mengi ambayo shughuli zao zisiposimamiwa na kuratibiwa vizuri hayataleta matokeo yanayotazamiwa. Alieleza kufurahishwa na mchango wa mashirika yanayosaidia Sekta ya Elimu kwani Mkoa wa Kigoma unafanya vizuri kitaaluma katika sekta hii.

Aliwataka Wakurugenzi katika Halmashauri kufanya kazi kwa bidii na kuwajibika ipasavyo na kwamba kwa muda waliokaa katika Mkoa tangu waanze kazi ugeni umekwisha. Aidha, alizikumbusha

Halmashauri kutenga maeneo ya viwanda na biashara kwa ajili ya wawekezaji na wajasiliamali. Pia alikumbusha na kusisitiza kila Halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo ya vijana na wanawake na kuzigawa kwa vikundi kulingana na maombi yao.

Mwenyekiti aliwataka Watendaji kuzingatia na kuyatekeleza kwa wakati maagizo na maelekezo yanayotolewa na ngazi za juu. Pia aliwaagiza Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa mkakati wa matumizi ya shilingi milioni 50 zitakazogawiwa kwa kila Kijiji. Alihimiza Wakurugenzi kuwasaidia wananchi kupanga matumizi ya fedha hizo zitakazopelekwa kila kijiji ili zitumike na kufikia matarajio yaliyokusudiwa na viongozi wa Kitaifa na Mkoa.

Akihitimisha hotuba yake ya ufunguzi, Mwenyekiti alielekeza mambo yafuatayo:

- Ni vema kila Halmashauri ikaandaa mpango mikakati wa kuboresha kilimo.
- Viongozi hususan Wabunge kufika kwenye vikao vya Kimkoa na Wilaya kila vinapoitishwa ili kuchangia mawazo ya kuuendeleza Mkoa wetu na pia kuyafahamu vizuri mahitaji ya Mkoa na kuyasemea ngazi ya Taifa.
- Vikao vya RCC ni vya muhimu sana kwa kuwa vinawezesha viongozi wote katika mkoa, wataalam na wadau mbalimbali kushirikishana mambo mengi ya kujenga Mkoa wetu.

Mwisho aliwakaribisha wote kwenye kikao na kisha kufungua kikao rasmi saa 4:38 asubuhi.

MUHT. 2: MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 MKOA WA KIGOMA

2.1 Muhtasari wa Mapendekezo ya Mkoa (RS na MSM)

Kabla ya kuwasilisha mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2017/18, iliwasilishwa taarifa ya utekelezaji wa bajeti mwaka **2015/16** ambapo hadi kufikia Juni 30, 2016 Mkoa ulikuwa umepokea sh. 153,157,639,720 ambazo ni sawa na 73.6% ya fedha iliyoidhinishwa. Matumizi yake yalifikia 98.1% ya fedha zilizopokelewa. Aidha, Halmashauri zilikusanya 79.1% ya malengo ya kukusanya mapato ya ndani kwa mwaka 2015/16.

Kwa mwaka **2016/17** kufikia 31 Januari 2017 Mkoa ulikuwa ulipokea sh. 105,597,454,886 sawa na 47.4% ya fedha zilizoidhinishwa, matumizi yalikuwa sh. 93,955,744,700 sawa na 88.5% ya fedha zilizopokelewa. Kwa mapato ya ndani, hadi 31 Januari 2017 Halmashauri zilikuwa zimekusanya wastani wa 37.6% ya makadirio ya malengo ya mwaka 2016/17.

Kwa muhtasari Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha **2017/2018** uliowasilishwa ulipendekeza kutumia sh.248,293,155,000 kwa ajili ya kutekeleza bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida (pamoja na vyanzo vya ndani vya MSM) ni sh. 202,168,581,000 na fedha za maendeleo ni sh. 46,124,574,000.

Ilielezwa kuwa bajeti ya OC ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeshuka kwa 28.7% kutoka sh. 1,923,966,000 mwaka 2016/17 hadi sh. 1,372,182,000 mwaka 2017/18 na bajeti ya OC ya MSM imeshuka kwa 24.1% kutoka sh. 17,928,395,412 mwaka 2016/16 hadi sh. 13,599,418,000 mwaka 2017/18. Aidha katika bajeti hii Mkoa unakadiriwa kuwa utapokea sh. 36,898,921,269 katika bajeti ya maendeleo kupitia mafungu ya Wizara na Wadau wengine wa maendeleo.

Pamoja na makadirio haya Mkoa uliwasilisha maombi maalum ya sh. 19,880,000,000 nje ya ukomo wa bajeti ambayo yanajumuisha maombi ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa sh 1,260,000,000 na Mamlaka za Serikali za Mitaa sh. 18,620,000,000.

Baada ya mawasilisho hayo wajumbe walipokea taarifa na kuanza kuijadili kama ifuatavyo:

- Wajumbe walitaka kujua kwa nini fedha za baadhi ya wadau ambao wanatekeleza shughuli za maendeleo katika Mkoa hazionekani au kujitokeza katika mpango na bajeti ya Mkoa. Maelezo yalitolewa kuwa wadau hao hususan UNICEF na BTC walikuwa bado hawajathibitisha kiasi cha fedha watakachotoa kwa bajeti ya maendeleo katika Mkoa wa Kigoma.
- Aidha wajumbe walihoji kwa nini katika bajeti iliyowasilishwa hakuna kifungu kinachoonesha madai ya walimu. Majibu yalitolewa kuwa madeni hayo hayawezi kuonekana katika bajeti iliyowasilishwa kwa sababu madeni hayo tayari yalikuwisha kuwasilishwa Hazina. Madeni yaliyopokelewa na kuwasilishwa Hazina yalibusu malimbikizo ya mishahara. Madeni mengine yanahusiana na uhamisho, ada ya masomo, fedha ya matibabu, fedha ya likizo na nauli za kusafiri kurudi nyumbani baada ya kustahafu.

Baada ya ufafanuzi huo kikao kiliagiza Halmashauri kutokuendelea kuzalisha madeni.

2.2 Mapendekezo ya bajeti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

Maptio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka **2015/16** yalionesha fedha zilizoidhinishwa zilikuwa sh. 10,749,964,419 na hadi tarehe 30 June 2016 zilipokelewa sh. 6,452,190,399 ambazo ni sawa na 82.7% ya fedha zote zilizoidhinishwa. Taarifa ilionesha fedha zote zilizopokelewa zilitumika katika mwaka huo.

Aidha mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka **2016/17** yalionesha fedha zilizoidhinishwa zilikuwa sh. 8,936,796,000 na hadi kufikia Januari 2017 zilipokelewa sh. 4,372,145,000, sawa na 48.9% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yalikuwa sh 3,254,167,000 sawa na 74.4% ya fedha zilizopokelewa.

Mwaka **2017/18** ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliwasilishwa bajeti ya sh. 9,830,136,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Fedha za bajeti ya matumizi ya kawaida zilikuwa ni sh. 7,145,275,000, sawa na 73% ya bajeti yote na fedha za bajeti ya maendeleo zilikuwa ni sh.

2,684,861,000, sawa na 27%. Pia ilielezwa kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliwasilisha maombi maalum ya sh. 1,260,000,000 kwa ajili ya kujenga uzio wa Ikulu Ndogo na kununua magari ya viongozi. Baada ya maelezo hayo, bajeti ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ilipokelewa na wajumbe walipewa nafasi ya kujadili.

Wakati wa majadiliano ilihojiwa kama kinachojengwa pale Ikulu Ndogo ni uzio au ukuta. Ufafanuzi ulitolewa kuwa unajengwa ukuta ili kuimarisha usalama. Hata hivyo ilipendekezwa kuwa iko haja ya kupata eneo lingine kwa ajili ya kujenga Ikulu Ndogo kwa ajili ya usalama na kuacha majengo ya sasa yaliyopo kuwa ya kihistoria na ya ukumbusho.

Mjumbe mmoja alitaka kupata ufafanuzi kuhusu maelezo yaliyotolewa kuwa magari yanayotumiwa na viongozi wa Mkoa kuwa yameazimwa kutoka UNHCR ni sahihi. Mwenyekiti alieleza ni kweli kuwa magari yale wameazimwa na gari moja hupatiwa mafuta lita 250 kwa mwezi. Kwa hiyo kama yameazimwa siku moja watahitaji magari yao, hivyo ni muhimu kununua magari ya viongozi wa Mkoa.

Katika majadiliano pia lilijitokeza suala la magari ya UNHCR yaliyoondolewa kwenye matumizi na sasa yamehifadhiwa GTZ Kasulu na kwamba kimkataba yanatakiwa kukabidhiwa Serikali. Hata hivyo, Mwenyekiti aliomba Waheshimiwa Wabunge kulisemea hili kwa Waziri ili utaratibu wa kuyakabidhi ufanyike.

Baada ya hoja hizo kujadiliwa, Mpango na bajeti ya ofisi ya Mkuu wa Mkoa ulipitishwa kama ulivyowasilishwa.

2.3 Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma /Ujiji

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji alianza kuwapitisha wajumbe kwenye mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 na 2016/17. Alieleza mwaka 2015/16 Halmashauri ilipokea sh. 21,148,953,000; sawa na 93.5% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yalikuwa sh. 21,115,563,542; sawa na 99.8% ya fedha zilizopokelewa. Aidha, kwa mwaka 2016/17 kuishia Januari 31 zilipokelewa sh 12,155,976,343; sawa na 40.1% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh. 12,081,387,852 sawa na 99.4 % ya fedha zilizopokelewa.

Kwa **mwaka 2017/18** Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji iliomba sh. 33,874,327,807 ndani ya ukomo wa bajeti ambapo sh 26,037,826.095 ni kwa matumizi ya kawaida na sh. 7,836,501,712 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Taarifa hiyo ilipokelewa na hapakuwa na majadiliano.

2.4 Halmashauri ya Mji Kasulu

Bajeti Halmashauri ya Mji wa Kasulu iliwasilishwa na Mkurugenzi wa Mji Kasulu kwa kufafanua hali ya Mji wa kasulu kiuchumi na kijamii. Katika mapitio ya bajeti ya mwaka 2015/16 alieleza kuwa fedha za

matumizi ya kawaida zilizopokelewa zilikuwa sh. 992,159,436 sawa na 42.2% ya fedha zilizoidhinishwa na fedha za maendeleo zilizopokelewa ni sh. 2,602,566,463 sawa na 67.9% fedha zilizoidhinishwa. Matumizi ya fedha za matumizi ya kawaida ni sh. 947,068,848 sawa na 95% na fedha za maendeleo zilitumika sh. 2,526,546,886 sawa na 97.1% ya fedha zilizopokelewa.

Kwa mwaka 2016/17 Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilipokea sh 7,490,144,740 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na 33.4 % ya fedha zilizoidhinishwa. Hadi Januari 31, 2017 Halmashauri ilikuwa imetumia fedha zote zilizopokelewa. Kwa bajeti ya maendeleo zilipokelewa sh 2,017,843,242, sawa na 23.4% ya fedha zilizoidhinishwa na kutumia sh 823,911,600 sawa na 40.8% ya fedha zilizopokelewa.

Baada ya taarifa hiyo ya mapitio ya utekelezaji, Mkurugenzi aliwasilisha mapendekezo ya mpango na bajeti ya **mwaka 2017/2018** ya jumla ya sh. 36,023,922,014 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo na sh.850,000,000 zilikuwa katika maombi maalumu kwa ajili ya ununuzi wa gari la Mkurugenzi, gari la taka ngumu na taka maji, na ujenzi wa wodi ya wazazi katika hospitali ya mji wa Kasulu.

Baada ya maelezo hayo, wajumbe walijadili na kupitisha bajeti hiyo kama ilivyowasilishwa. Hata hivyo ilitolewa hoja ya kutaka magari ya UNHCR yaliyoko GTZ Kasulu yagawiwe kwa Halmashauri na kwamba Halmashauri ilikwisha andika barua ya kuomba gari hususani la Mkurugenzi. Maelezo yalitolewa kuwa mpango wa kununua gari uwepo na hayo ya UNHCR yatafuata taratibu zilizowekwa.

2.5 Halmashauri ya Wilaya Kigoma

Mapango na bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iliwasilishwa kwanza kwa kutoa utangulizi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2015/16 na mwaka 2016/17. Akiwasilisha bajeti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo alieleza kuwa mwaka 2015/16 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni sh 17,113,124,709 ambazo ni sawa na 82.09% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh. 17,075,643,882, sawa na 99.78% ya fedha zilizopokelewa.

Aidha, kwa bajeti ya maendeleo zilipokelewa sh. 478,038,698 ambazo ni sawa na 21.27% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yalikuwa ni sh 264,736,371 sawa na 55.37 % ya fedha zilizopokelewa.

Kwa mwaka 2016/17 hadi Januari 31 sh. 10,622,315,694 zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambazo ni sawa na 53.20% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh. 10,572,899,784 sawa na 99.53% ya fedha zilizopokelewa. Kwa bajeti ya maendeleo zilipokelewa sh 643,314,471 sawa na 28.11% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh 116,667,157, sawa na 18.13% ya fedha zilizopokelewa hadi Januari 31, 2017.

Kwa Mpango na bajeti ya **mwaka 2017/18** vipaumbele vilitajwa kuwa ni ujenzi wa barabara ya Mwandiga, Chankere, Mwangongo hadi Kagunga; Hospitali ya Wilaya, ujenzi wa majengo ya Halmashauri na kununua gari la Mkurugenzi. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iliomba sh.

32,594,500,126 ndani ya ukomo wa bajeti na sh 6,250,000,000 katika bajeti ya maendeleo zikiwa ni maombi maalum.

Baada bajeti kuwasilishwa, Mwenyekiti alitaka kujua hatua zilizochukuliwa katika bajeti hii ili kukamilisha utengenezaji wa madawati kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Manispaa ya Kigoma kwani zilikuwa nyuma sana.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigoma alieleza kuwa katika bajeti zimetengwa sh. 40m kupitia LCDG kwa ajili ya kutengeneza madawati. Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma mkakati uliowekwa ni kuendelea kushirikiana na wananchi, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuwashirikisha wadau mbailmbali kuchangia. Mwenyekiti alitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iwe imekamilisha utengenezaji wa madawati ifikapo mwisho wa mwezi Mei, 2017.

Pia ulitolewa ushauri kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuitafuta sheria ya kodi ya majengo (property tax) ili waisome, kuelewa vizuri na kuitekeleza ipasavyo ili kuongeza mapato ya ndani.

Bajeti ilipokelewa na kupitishwa kama ilivyowasilishwa.

2.6 Halmashauri ya Wilaya Kasulu

Katika mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2015/16 na mwaka 2016/17, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu alieleza kuwa mwaka 2015/16 fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni sh 30,461,857,100 sawa na 92.9% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh. 30,460,786,800 sawa na 99% ya fedha zilizopokelewa. Aidha, kwa bajeti ya maendeleo zilipokelewa sh 2,619,863,386, sawa na 33.5% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi zilikuwa ni sh 1,955,008,595 sawa na 74.6% ya fedha zilizopokelewa.

Mwaka 2016/17 hadi Januari 31, Halmashauri ilipokea sh. 17,733,176,545 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambazo ni sawa na 47.1% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ni sh. 17,560,883,654 sawa na 99% ya fedha zilizopokelewa. Fedha za maendeleo zilipokelewa sh 4,336,196,689, sawa na 50.7% ya fedha iliyoidhinishwa na matumizi ni sh 2,305,068,586, sawa na 53.2% ya fedha zilizopokelewa kuishia Januari 31, 2017.

Kwa mwaka **2017/18** Halmashauri iliwasilisha mapendekezo ya kutumia sh. 35,865,364,806 kwa Matumizi ya kawaida na Maendeleo ndani ya ukomo wa bajeti na sh. 5,382,164,328 ni maombi maalum nje ya ukomo wa bajeti. Mkurugenzi alieleza vipaumbele ni (1) kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani (2) kukamilisha miundombinu ya shule (3) kuboresha na kuimarisha matumizi bora ya ardhi (4) kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji na kulipa madeni yote.

Bajeti ilipokelewa na kupitishwa kama ilivyowasilishwa.

2.7 Halmashauri ya Wilaya Kibondo

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo alieza katika bajeti ya mwaka 2015/16, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa zilikuwa sh 17,039,457,400 sawa na 68% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi zilikuwa sh. 17,015,012,200, sawa na 97% ya fedha zilizopokelewa. Fedha za maendeleo zilipokelewa ni sh. 2,706,383,000, sawa na 28% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi zilikuwa sh. 1,779,795,000 sawa na 65% ya fedha zilizopokelewa.

Kwa mwaka 2016/17 hadi Januari 31, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni sh 8,416,625,157, ambazo ni sawa na 43% ya fedha iliyoidhinishwa na matumizi ni sh. 8,414,683,157, sawa na 99% ya fedha zilizopokelewa. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni sh 1,672,747,000/=, sawa na 38% ya fedha iliyoidhinishwa na matumizi ni sh 836,672,000/=, sawa na 50% ya fedha zilizopokelewa hadi Januari 31, 2017.

Mwaka 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo iliomba sh. 31,262,961,167/= kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya maendeleo. Mkurugenzi alieleza vipaumbele vya Wilaya kuwa ni (1) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuhakikisha gawio la 20% ya mapato linarudi vijiji kwa ajili shughuli mbalimbali za maendeleo (2) Kuziba mianya yote ya rushwa na ubadhilifu (3) Kushirikisha wadau wa maendeleo wa ndani na nje zikiwemo Asasi za kiraia ili kufanikisha utekelezaji wa bajeti 2017/2018 (4) Kushughulikia kwa wakati stahili za watumishi na kuwachukulia hatua wale wanaoenda kinyume na sheria na taratibu (5) Kuunga Mkono miradi inayoanzishwa na wananchi kwa kwa nguvu zao (6) Kuajiri watumishi wenye sifa na weledi . Vipaumbele vilivyowasilishwa kwa bajeti ya maendeleo ni (1) Kuimarisha kituo cha afya Busunzu, (2) kuboresha miundombinu katika shule za sekondari (3) Kilimo cha zao la alizeti.

2.8 Halmashauri ya Wilaya Uvinza

Katika mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2015/2016 na mwaka 2016/17 Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza alieleza kuwa kwa mwaka 2015/16 fedha ziliyopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa sh. 9,033,996,208 sawa na 44% ya fedha zilizoidhinishwa na fedha zote zilitumika. Kwa bajeti ya maendeleo zilipokelewa 6,460,392,964 ambazo ni sawa na 49% ya fedha zilizoidhinishwa na zilitumika sh 3,314,459,384, sawa na 86% ya fedha iliyopokelewa.

Mwaka 2016/17 hadi Januari 31, 2017, fedha zilizopokelewa kwa bajeti ya matumizi ya kawaida zilikuwa sh 6,676,354,646 ambazo ni sawa na 29% ya fedha zilizoidhinishwa na fedha hizo zote zilizopokelewa zilitumika katika kipindi hicho. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni sh. 3,431,631,760, sawa na 32% ya fedha zilizoidhinishwa na zilitumika fedha zote ziliyopokelewa katika kipindi hicho.

Kwa mwaka **2017/2018** Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza iliomba kuidhinishiwa sh. 36,965,197,431 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ndani ya ukomo wa bajeti na maombi maalum ya sh. 3,000,000,000. Maombi maalumu ni kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na nyumba 10 za Wakuu wa Idara.

Katika mjadala suala la ukusanyaji mapato ya ndani lilijitokeza hususan la mrabaha kwenye kiwanda cha chumvi na migodi ya chokaa na malipo ya kodi ya ardhi. Halmashauri ilishauriwa kuhakikisha hakuna ukwepaji kodi na ushuru katika vyanzo hivyo. Maelezo yalitolewa kuwa ukusanyaji wa mapato ya ardhi yanafanyika na hupelekwa Serikali Kuu na Halmashauri hurejeshewa 30% ya makusanyo hayo. Wakurugenzi wa halmashauri zote walishauriwa kufuatilia ushuru wa huduma (service levy) wa 0.3% katika maeneo yao.

2.9 Halmashauri ya Wilaya Buhigwe

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe alieleza kuwa mwaka 2015/16 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni sh. 1,324,219,939 sawa na 56% ya fedha iliyoidhinishwa na fedha zilizotumika zilikuwa sh. 1,315,723,292 sawa na 99% ya fedha iliyopokelewa. Kwa bajeti ya maendeleo zilipokelewa sh 4,570,975,391 sawa na 62% ya fedha zilizoidhinishwa na zilitumika sh 4,096,695,939 sawa na 90% ya fedha iliyopokelewa kuishia June 30, 2016.

Kuhusu mpango na bajeti ya mwaka 2016/17 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa kuishia 31 Januari, 2017 ni sh. 7,590,877,111, sawa na 49% ya fedha zilizoidhinishwa na fedha zilizotumika zilikuwa sh. 7,544,456,839 sawa na 99% zilizopokelewa. Kwa fedha za maendeleo zilipokelewa sh 3,908,068,390 sawa na 60% ya fedha zilizoidhinishwa na kutumika sh 1,703,697,062, sawa na 44% ya fedha zilizopokelewa.

Kwa mwaka **2017/2018** Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe iliomba kuidhinishiwa sh. 25,404,437,611 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kutekeleza miradi ya maendeleo ndani ya ukomo wa bajeti na maombi maalum ya sh. 2,000,000,000/= kwa ajili ya miradi ifuatayo:

- Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Buhigwe,
- Matengenezo ya Barabara Makao Makuu ya Wilaya
- Mradi wa maji Makao Makuu ya Wilaya

Wajumbe walipokea mapendekezo hayo ya bajeti kama yalivyowasilishwa na kisha kuyajadili. Katika mjadala lilijitokeza suala la kukosekana soko la mifugo na soko la Nyamugali kutofanya kazi kwa kukosa miundombinu ya maji na choo. Kikao kiliagiza ifikapo mwezi Juni 2017 soko lianze kufanya kazi.

Suala lingine ni trekta ya Halmashauri ambayo ilielezwa kuwa halitumiwi na wananchi na sababu mojawapo ilielezwa huenda ikawa bei kubwa ya kulikodi. Halmashauri ilitakiwa kuchunguza sababu ya wananchi kutolitumia trekta na kuchukua hatua za kutatua changamoto hiyo.

2.10 Halmashauri ya Wilaya Kakonko

Kwa mwaka 2015/16 Halmashauri ilipokea fedha ya matumizi ya kawaida sh. 7,054,282,000, sawa na 53.4% ya fedha iliyoidhinishwa na fedha zote zilizopokelewa zilitumika. Kwa bajeti ya Maendeleo, zilipokelewa sh. 1,019,688,410, sawa na 30.5% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi ilikuwa sh. 471,337,792 sawa na 46.2% ya fedha iliyopokelewa.

Mwaka wa 2016/17 hadi Januari 31, 2017, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni sh. 5,750,457,267, sawa na 55% ya fedha zilizoidhinishwa ambapo matumizi ni sh. 5,750,457,267, sawa na 100% ya fedha zilizopokelewa. Kwa miradi ya maendeleo zilipokelewa sh. 3,056,930,661 sawa na 54.2% ya fedha zilizoidhinishwa na matumizi yake yalikuwa sh 1,645,527,622, sawa na 53.8% ya fedha zilizopokelewa.

Kwa mwaka **2017/18** vipaumbele vya Halmashauri ni kukamilisha miradi viporo, kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri, kukamilisha ujenzi wa stendi ya mabasi yatokayo mikoani na kuboresha huduma za kijamii. Halmashauri ya Wilaya iliomba sh. 31,507,581,656 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo na sh. 2,250,000,000 zilikuwa maombi maalum.

Maombi maalum ni kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, ujenzi wa Sekondari ya Kakonko Kidato cha Tano na cha Sita na ununuzi wa magari 5.

Baada ya Halmashauri zote kuwasilisha maelezo na ushauri wa ujumla ulitolewa kama ifuatavyo:

- Kwa Halmashauri zinazojenga Makao Makuu ya Wilaya zilishauriwa kutumia ramani za Halmashauri ya Kongwa au Mvomero na mkandarasi atakuwa TBA au SUMMA JKT kulingana na maagizo ya Serikali.
- Kila Halmashauri ikamilishe majengo ya biashara (one business stop center); ni Kakonko tu waliokamilisha jengo hilo wakati Kasulu bado hawajakubaliana eneo la kujenga.
- Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi wahakikishe fedha za miradi zinazotolewa zinatumika ipasavyo.
- Zianzishwe “farm tractor center” katika kila Halmashauri ili kuondokana na kilimo cha jembe la mkono. Kila Halmashauri iandae andiko la mradi kuanzisha kituo hicho na Wabunge watafute wapi trekta angalau 10 zitapatikana kwa kila Halmashauri.
- Wajumbe walihoji na kutaka kujua maendeleo ya ujenzi wa Kigoma Grand High School na Kigoma Grand Hospital , maelezo yalitolewa kuwa taarifa ya miradi hiyo hazikuwasilishwa

kwa sababu kikao hiki ni maalumu cha kujadili bajeti, hivyo taarifa zake zitaandaliwa na kuwasilishwa wakati wa kikao cha kawaida kijacho.

MUHT. 3: KILIMO CHA MICHIKICHI

Mpango wa Maendeleo ya Zao la Michikichi Mkoani Kigoma uliwasilishwa kwa lengo la kupata maoni na ushauri wa washiriki ili kuweza kuendeleza zao hili kwa utaalumu zaidi na kulitambulisha ndani na nje ya Mkoa wa Kigoma. Mpango huo ulitokana na Mkoa wenyewe na siyo maelekezo kutoka juu.

Mada iliyowasilishwa ilibainisha kwa takwimu umuhimu za zao la chikichi kama ifuatavyo:

- Kutoka mwaka wa 2000 - 2007 zaidi ya 95% ya mafuta ya kula yaliyoagizwa nchini yalikuwa ni mawese.
- Pia takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka wa 2016, mahitaji ya Taifa ya mwezi ya mawese yalikuwa ni tani 50,000, wakati uzalishaji wa mafuta haya kwa mwaka ni tani 40,000 (zikiwemo tani 30,000 zinazozalishwa na Mkoa wa Kigoma).
- Kutokana na takwimu hizi ni dhahiri kuwa uzalishaji haukidhi mahitaji ya Taifa ambayo ni tani 600,000 kwa mwaka (kuna upungufu wa tani 560,000).
- Uagizaji wa mafuta ya mawese umeongezeka kutoka tani 3,000 mwaka wa 1978 hadi tani 510,000 mwaka jana (2016) na utaongezeka kwa miaka ijayo.
- Utumiaji wa fedha za kigeni kuagiza mawese kutoka nje umeongezeka kutoka dola za kimarekani \$ 13,000,000 mwaka 1961 hadi zaidi ya \$320,000,000 kwa mwaka wa 2016.
- Kigoma ni Mkoa pekee unaolima zao la michikichi kwa wingi nchini Tanzania ukiwa na hekta 18,924 zenye michikichi inayozalisha tani 30,010 (tani 1.6 kwa hekta za matunda ya chikichi).
- Uwezekano wa uzalishaji ni tani 75,700 sawa na tani 4.0 kwa hekta kwa eneo lililopo lenye michikichi.
- Hali ya uzalishaji wa chikichi Kigoma kwa sasa unaonekana kuwa chini na duni kwa sababu zifutazo: (1) Uzee wa michikichi iliyopo (2) mashamba kutokutunzwa (3) ukosefu wa mbegu bora pamoja na teknolojia duni ya uchakataji wa zao.

Mpango wa kuendeleza zao la chikichi katika Mkoa wa Kigoma utazingatia yafuatayo:

- Kuanza na wakulima 100,000 ambao watapewa mbegu zilizoreshwa (chotara) kila mmoja miche 150 ambayo itatosha kupanda eneo la hekta moja (ekari mbili na nusu)
- Kwa sasa mbegu bora hazipatikani nchini kwetu bali zinaagizwa kutoka nchi kama Costa Rica, Malaysia na **Indonesia** kwa gharama ya dola ya kimarekani moja kwa mbegu moja.

- Itahitajika miche milioni 15, kwa ajili ya wakulima wetu 100,000, hivyo zitahitajika dola za kimarekani milioni 15 kuagiza mbegu tu na kiasi kama hicho USD 15m kuhudumia mbegu hizo.
- Njia mbadala ambayo Mkoa unapendekeza ni kuwa na kituo chake cha uzalishaji mbegu na maabara.
- Hiki kituo kitafanya utafiti na uzalishaji wa miche bora kwa kutumia mfumo wa 'tissue culture' ili kuzalisha miche mingi kwa gharama ndogo na kwa muda mfupi.
- Mkoa umependekeza kazi hii ifanywe na kampuni ya FELISA ikishirikiana na kituo cha utafiti wa kilimo cha Mikocheni (M.A.R.I.) kilichopo Dar es Salaam.
- Mpango huu utahitaji viwanda 7 vya kisasa ili kusindika malighafi itakayozalishwa, Kiwanda kikuu kimoja kitakachoweza kusindika mawese ghafi, Viwanda vidogo vinne vitawekwa kwenye vijiji vitakavyopendekezwa na MSM, Kiwanda kimoja kwa ajili ya usindikaji wa mafuta ya alizeti. Baada ya miaka kadhaa, Mkoa unatarajia kujenga kiwanda cha kutengeneza gesi kutokana na mashudu ya michikichi.

Ili kuongeza tija ya zao la chikichi hamasa inahitajika katika wilaya zote zenye maeneo yanayofaa kwa kilimo cha chikichi ili kufufua mashamba na kuanzisha mapya. Pia ni muhimu yawepo makampuni binafsi kuzalisha miche bora na kuisambaza kwa wakulima.

Wajumbe walipokea wazo la mpango huu na kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

- Majukumu ya Halmashauri yaainishwe vizuri kwenye mpango na yaonekane wazi.
- Lengo la kuwashirikisha wakulima 100,000 katika mpango lichanganuliwe ili ijulikane kila Halmashauri itakuwa na wakulima wangapi.
- Zao la chikichi halina bodi – ianzishwe bodi ya zao la chikichi ili kusaidia uendelezaji wa kilimo cha zao hilo. Aidha, wananchi wabadilishwe mtazamo juu uendelezaji wa zao la chikichi.
- Wananchi wahamasishwe ili wajunge na walime kupitia vyama vya ushirika.
- Kianzishwe kiwanda cha kuchakata mawese
- Mpango wa kuendeleza zao la chikichi uzingatie kutafuta fedha za ndani (Mkoa na Taifa) badala ya kufikiria nje ya nchi.
- Kwa kuwa kilichowasilishwa ni wazo (concept note) ambalo lilikubalika, hivyo liandaliwe andiko kamili.

Baada ya mjadala Wajumbe kwa kauli moja walipitisha wazo hilo na walitaka andiko liandaliwe.

MUHT. 4: MENGINEYO

Katika agenda hii yalitolewa maelezo mafupi ya uzinduzi wa zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya Taifa kwa Watumishi wa Umma. Mratibu wa uandaaji wa vitambulisho hivyo Mkoani Kigoma aliwasilisha taarifa yake iliyoeleza mchakato mzima ulivyokuwa na kwamba jumla ya watumishi wa

umma 16,173 walisajiliwa na hadi tarehe ya uzinduzi (17/03/2017) vitambulisho 9,500 vilikuwa tayari. Alieleza kuwa zoezi limekamilika kwa Watumishi wa Umma na watakaofuatia ni Wakimbizi, kisha wageni wakazi na mwisho raia wa kawaida. Utaratibu ulioelezwa ni kwa Mkoa wa Kigoma tu.

Akizindua ugawaji wa vitambulisho hivyo Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ambaye alikuwa mgeni rasmi alieleza kuwa sasa tunaingia katika ulimwengu wa kutambuliwa Kimataifa. Aliwataka Watanzania kutunza vitambulisho hivyo muhimu na kuwataka wananchi wa Kigoma kusaidia upatikanaji wa raia halisi ili asiye raia asipewe kitambulisho cha Tanzania. Aliwataka wataalamu wa vitambulisho hivyo kuwahakikishia watumishi waliojijajili kupata vitambulisho vyao.

Baada ya maneno hayo, Mkuu wa Mkoa alizindua zoezi hilo la ugawaji vitambulisho kwa kukata utepe na kumgawia kitambulisho cha uraia Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

MUHT. 5: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga kikao kwa kuwashukuru wajumbe na wageni waalikwa kwa ushiriki na michango yao ambayo ilifanikisha kikao. Aidha, aliwataka viongozi na wataalam kutoka wilayani kwenda kutatua migogoro ya ardhi iliyopo katika maeneo yao na kuwatendea haki wananchi. Aliwaomba Wabunge kuweka msukumo wao katika maombi maalumu yaliyowasilishwa na Mkoa ngazi ya Taifa.

Pia aliwaasa Viongozi wa Serikali wa kuteuliwa na wale wa kuchaguliwa kumaliza tofauti zao kupitia mazungumzo na kwamba kusiwepo tena sababu ya kuundwa tume za uchunguzi na usuluhishi. Vilevile aliwakumbusha wajumbe kuwa sheria iliyounda Mamlaka za Serikali za Mitaa inampa Waziri mwenye dhamana mamlaka ya kuzivunja pale anapoona hazipo kwa masilahi ya wananchi lakini akataka wasiifikishe Serikali katika hatua hiyo.

Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifunga kikao rasmi saa 10.40 jioni.

Muhtasari umethibitishwa na:

.....
Mwenyekiti

.....
Katibu

.....
Tarehe

**YATOKANAYO
MKUTANO WA KAMATI
YA USHAURI YA MKOA
WA TAREHE 25
NOVEMBA, 2016 NA
MKUTANO WA TAREHE
17 MACHI, 2017**

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAMATI YA USHAURI YA MKOA WA KIGOMA (RCC)
ULIOFANYIKATAREHE 25 NOVEMBA 2016**

N A	AZIMIO	UTEKELEZAJI
1	Katibu Tawala Mkoa awe anaalika Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakizi (UNHCR) katika vikao vya RCC ili litoe taarifa za utekelezaji wa kazi linazofanya Kigoma	Agizo limetekelezwa, UNHCR wamealikwa na watawasilisha mada inayohusu shughuli zinazotekelezwa katika kambi za wakimbizi na shughuli za maendeleo katika jamii inayozunguka kambi za wakimbizi
2	Wilaya zinazofaa kwa kilimo cha kahawa ziweke malengo ya uzalishaji na kusimamia uzalishaji	<p>KIGOMA DC</p> <p>Kata tano za Mkigo, Nyarubanda, Kalinzi, Mkongoro na Bitale zinalima kahawa. Vilevile kata za Kagunga na Mwamgongo zimeingizwa kwenye mpango.</p> <p>Kila mkulima kwenye maeneo haya ni lazima awe na miche ya kahawa isiyopunguwa 300. Msisitizo umewekwa katika kupanda miche chotara ya kahawa inayostahimili magonjwa na kutoa mavuno mengi.</p> <p>KIBONDO DC</p> <p>Halmashauri imeanza kufufua uzalishaji wa zao la kahawa. Katika msimu wa kilimo 2016/2017 ilinunua mbegu bora za kahawa kutoka TaCRI Lyamungo kilo 150 ambazo zina uwezo wa kuzalisha wastani wa miche 300,000.</p> <p>Musimu wa 2017/18 Halmashauri imetenga sh. 9,030,000/= za kuendeleza zao la kahawa.</p> <p>KASULU DC</p> <p>Halmashauri imeandaa malengo ya kuendeleza zao la kahawa katika kata ya Buhoro kwa kuanzisha shamba la kuzalisha mbegu (Kitalu cha uzalishaji miche ya vikonyo) na kuwezesha wakulima kupanda miche bora ya kahawa 10,000 kufikia Juni 2018. Uzalishaji wa kahawa ni wastani wa gramu 300 - 400 kwa mti. Halmashauri ina kitalu kimoja cha kuzalisha miche ya kahawa chenye miche mama 410</p> <p>KAKONKO DC</p> <p>Kilimo cha kahawa kinafanyika katika kata ya Muhange, Kiziguzigu na Gwarama. Miche 200,000 ilipandwa katika kata za Kiziguzigu na Muhange na uzalishaji ni wa wastani. Elimu juu ya kilimo cha zao hili inaendelea kutolewa kwa wakulima katika kata zote. Kilo 934.4 huzalishwa kwa mwaka</p>

		<p>na kila kilo moja ni shilingi 1,200</p> <p>UVINZA DC</p> <p>Jitihada za kuanzisha uzalishaji wa zao la Kahawa katika Wilaya ya Uvinza zinaendelea. Hadi sasa kitalu cha shamba mama la kahawa ya vikonyo limeanzishwa kijiji cha Lubalisi kwa lengo la kuanzisha kilimo cha zao la kahawa kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la Upright Society Foundation ambalo limeshamiriya kugawa miche ya kahawa 540 aina ya Compact Arabica Hybrid 2013 kwa kila kaya iliyohamasika kuzalisha kahawa. Jumla ya miche 40,000 imeandaliwa.</p> <p>BUHIGWE DC</p> <p>Zao la kahawa linafaa kulimwa katika kata zote 20 zilizopo Wilaya ya Buhigwe. Hata hivyo, ni kata 6 tu ambazo zinalima kahawa na kata hizo ni Mwayaya, Munanila, Mubanga, Muhinda, Kibwigwa na Buhigwe. Halmashauri imesimamia kilimo na uzalishaji wa zao la kahawa kwa kufanya yafuatayo:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1) Kuhamasisha Kata zote 20 ziweze kulima zao la kahawa. 2) Kutoa miche 3,000 kwa wakulima 100 katika kata za Mwayaya, Buhigwe na Kibwigwa, 3) Kutoa mafunzo kwa wakulima 100 wa zao la kahawa. <p>KASULU MJI</p> <p>Malengo yaliyowekwa Msimu 2016/ 17 yalikuwa Hekta 37 na utekelezaji ulikuwa hekta nne tu hii ilitokana na changamoto ya upatikanaji wa miche hasa ile ya vikonyo katika vitalu vilivyoko Wilaya ya Buhigwe. Halmashauri ina mpango wa kuanzisha kitalu chake ili kutimiza malengo yake.</p>
3	Katibu Tawala Mkoa atoe taarifa ya uzalishaji wa kahawa (miche iliyokuzwa na kupandwa).	<p>Katika Mkoa wa Kigoma zao la kahawa (mibuni) linafaa kuzalishwa katika Wilaya zote katika baadhi ya maeneo. Kwa mwaka 2016/17 Wilaya ya Kigoma ilizalisha miche 25,162 na kuisambaza kwa vikundi vya wakulima vya Upendo miche 900, Mkombozi Miche 980, RUMACO miche 4,300 mingine iliyobaki iligawiwa kwa wakulima mmoja mmoja miche 6,000. Vikundi na wakulima hao ni wa kata ya Kalinzi. Kampuni ya Domans ilizalisha miche 19,062 na kupanda miche 12,982 ambapo Halmashauri ilizalisha miche 6,100. Wilaya ya Kibondo ilizalisha miche 27,000 na wakulima 100 kila mkulima aligawiwa miche 270 kwenye kata ya Mabamba. Kakonko walizalisha miche 8,800 na kuzigawa kwenye kata ya Muhange. Wilaya ya Kasulu walizalisha miche 2,600 na kuzigawa kambi ya JKT Mutabila miche 1,200 na kata ya Heru Juu miche 1,400. Buhigwe kwa kushirikiana na TaCRI walizalisha miche 3000 ambayo iligawiwa kwa wakulima Tarafa ya Mwayaya.</p>
4	Mkoa wa Kigoma	

<p>uweke msisitizo kwenye utekelezaji wa mpango wa Wilaya moja Zao moja (one district one product- (ODOP). Kila Wilaya isimamie utekelezaji wa mpango huu.</p>	<p>MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI: Manispaa imeweka msisitizo kwenye zao la michikichi. Lengo ni kuwa na michikichi ya kisasa. Kuna mpango wa kupanda miche ya kisasa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao ni FELISA na LIC. Pia Manispaa imepanga kupanda miche katika Kata ya Kagera ambako eneo lililotengwa kupandwa miche hiyo lina ukubwa wa ha. 789, hivyo makadirio ni kupanda miche 105,000 ya kisasa.</p> <p>KIGOMA DC Msisitizo umewekwa katika zao la muhogo kama zao la chakula ingawa mazao mengine kama mahindi, mpunga na maharage nayo yanasisitizwa.</p> <p>KIBONDO DC Halmashauri ya wilaya ya kibondo imeweka msisitizo katika zao la muhogo ambalo kwa sasa uzalishaji wake ni mkubwa na wa kuridhisha. Kwa sasa Halmashauri inatumia kikundi cha Kibondo Big Power (KBPG) kuzalisha mbegu kinzani na magonjwa makuu ya mhogo yaani Batobato kali na Michirizi kahawia. Halimashauri kwa kushirikiana na asasi za KIYADO na OXFAM inajenga kiwanda cha kusindika zao la mhogo katika Kijiji cha Kumhasha.</p> <p>KASULU DC Halmashauri imelipa kipaumbele zao la Muhogo kwa kuhamasisha wakulima kulima kama zao la biashara na chakula pia.</p> <p>KAKONKO DC Halmashauri inaendelea kutekeleza kilimo cha mihogo kama zao kuu linalolimwa katika maeneo yote ya Wilaya. Mnyororo wake wa thamani unaendelezwa chini ya mradi wa SAKIP. Wananchi wamejiunga katika vikundi na kupatiwa mbegu bora ya mihogo ili waweze kuzalisha mihogo isiyo na maradhi kama ya batobato. Kuna vikundi 40 katika vijiji 20 na kila kikundi kinahimizwa kuzalisha ekari 1 ya mihogo.</p> <p>UVINZA DC Wilaya ya Uvinza ina kanda 3 za kilimo (Ecological zones) zinazolazimisha kulima mazao yanayotofatiana ndani ya wilaya kama ifuatavyo:- 1. Kanda ya Magharibi – zao la tumbaku 2. Kanda ya kati – mazao ya mafuta, alizeti na ufuta. 3. Kanda ya ziwa Tanganyika – michikichi na Mpunga Hata hivyo zao litakalosimamiwa ambalo linastawi katika kanda zote za wilaya ya Uvinza ni zao la Muhogo.</p>
---	--

		<p>BUHIGWE DC</p> <p>Hali ya Hewa na udongo kwa Wilaya ya Buhigwe inafaa kwa mazao ya Migomba, Kahawa, Michikichi na Mihogo. Mazao yanayopewa kipaumbele na wakulima pamoja SAKiRP ni zao la Muhogo na Maharage katika maeneo ya kata 4 za Munzeze, Janda, Bukuba na Buhigwe. Wilaya inaweka msisitizo wa uzalishaji wa zao la muhogo.</p> <p>KASULU MJI</p> <p>Zao moja inalopewa kipaumbele katika Halmashauri ya Mji ni muhogo. Maeneo yanayozalisha zao hili ni Kata 8 za Kigondo, Ruhita, Murufiti, Kanazi, Msambara, Nyumbigwa, Nyasha, na Marumba.</p>
5	<p>Kila Wilaya ikasimamie suala la kuwaandaa wakulima katika vikundi ili ushauri uliotolewa na WFP wa kununua mazao ya chakula kwenye vikundi litekelezwe.</p>	<p>KIGOMA/UJIJI</p> <p>Kutokana na hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula, Manispaa haina vikundi vitakavyoweza kuingizwa katika mpango wa kuwauzia WFP. Hata hivyo kuna uwezekano wa kushirikisha vikundi vya wafanyabiashara ya mazao ya chakula ambao wana uwezo wa kukusanya mazao kwa wakulima na kuwauzia WFP kiasi cha kutosha.</p> <p>KIGOMA DC</p> <p>Halmashauri imeanza utekelezaji kwa kuvitambua vikundi 31 katika kata 10 za Matendo, Kidahwe, Simbo, Mungonya, Mahembe, Mkongoro, Bitale, Kalinzi, Nyarubanda na Mwamgongo na utaratibu wa kuvitembelea utafanyika.</p> <p>KIBONDO DC</p> <p>Halmashauri imeaandaa vikundi vya Kibondo Big Power na Amani Akina Mama - Kata ya Kibondo Mjini, Turafasha - Kata ya Busunzu, Kikundi cha Utukuzwe, Rukundo, Hazina Women Group, Ushirika, Mshikamano, Lukaya Group na Kazamwendo- Kata ya Rugongwe, Kichananga. Halmashauri itavijengea uwezo vikundi hivyo kwa kuvipa elimu ya kanuni bora za kilimo ili viweze kuzalisha mazao ya kutosha yenye ubora.</p> <p>KASULU DC</p> <p>Halmashauri itanzisha kilimo cha umwagiliaji maeneo yanayozunguka kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu. Kupitia kilimo hicho wananchi wanahamasihwa kuunda vikundi vya wakulima ili waweze kulima kwa tija na kuuza mazao yao WFP.</p> <p>KAKONKO DC</p> <p>Halmashauri kupitia mradi wa MIRVARF inatoa elimu kwa wakulima wa mpunga katika skimu za umwagiliaji kuunda na kuimarisha AMCOS ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga kutoka gunia 15 hadi 40 kwa ekari ili wawe na mazao ya kutosheleza mahitaji ya WFP. Skimu zinazoshiriki katika</p>

		<p>uzalishaji ni Ruhwiti, Kitangera, Nyaronga na Mwiruzi.</p> <p>UVINZA DC Halmashauri inaendelea na juhudi za kuwahamasisha wakulima kujiunga katika vikundi na mpaka sasa vikundi 2 vimeundwa ambavyo ni Kandaga SACCOS na Nyanganga SACCOS.</p> <p>BUHIGWE DC Halmashauri imehamasisha wakulima kujiunga katika vikundi katika vijiji vyote 44. Aidha maafisa ugani waliopo kwenye kata wameagizwa kusimamia utekelezaji.</p> <p>KASULU MJINI Idadi ya Vikundi vya uzalishaji wa mazao vilivyopo ni vifuatavyo:- Vikundi vya Muhogo 43, Vikundi vya Maharage 37, Vikundi vya Kahawa 11 na Vikundi vya alizeti 19.</p>
6	<p>Halmashauri zihakikishe zinanunua mashine za kielektroniki za kutosha na kuzitumia katika ukusanyaji wa mapato</p>	<p>MANISPAA YA KIGOMA/UJJI Mahitaji ya mashine za PoS ni 120 kwa sasa. Halmashauri ina PoS 84 na upungufu wa PoS 36. Ongezeko la mapato baada ya kutumia PoS ni asilimia 50 hadi 70 kwa mwezi na wastani wa asilimia 60 kwa mwaka.</p> <p>KIGOMA DC Mahitaji ya mashine za kukusanyia mapato 60, kwa sasa zipo mashine 15 na kuna upungufu wa mashine 45. Kuna mpango wa kununua nyingine 15 katika bajeti ya mwaka huu 2017/2018 ambapo shs 36,000,000 zimetengwa. Baada ya kuanza kutumia mashine makusanyo yameongezeka kwa asilimia 55 kwa mwaka 2016/17.</p> <p>KIBONDO DC Halmashauri inahitaji mashine 75 za kielektroniki, zilizopo ni 55 (15 zilinunuliwa na LIC na 45 zilinunuliwa na Halmashauri), upungufu ni mashine 20 ambazo zimepangwa kununuliwa mwaka wa fedha 2017/18. Kiasi cha shs 12,500,000/= zimetengwa kwa ajili ya kununulia mashine hizo.</p> <p>KASULU DC Halmashauri inahitaji mashine 45 zilizonunuliwa ni mashine 25 ambapo 23 ndizo zinazofanya kazi huku 2 zikiendelea kufanyiwa marekebisho na mtaalamu wa TEHAMA. Kwa bajeti ya mwaka huu 2017/2018 Halmashauri inategemea kuongeza mashine nyingine 10 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani na kufanya kuwa na jumla ya mashine 35.</p> <p>KAKONKO DC Halmashauri inahitaji mashine 52 kwa kwa sasa zimenunuliwa mashine 39.</p>

		<p>Ili kufikia lengo la kuongeza mapato Halmashauri itahakikisha kila kijiji kina mashine katika masoko yote. Mashine zinaendelea kununuliwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika bajeti ya mwaka 2016/17 mashine mpya 3 zilinunuliwa.</p> <p>UVINZA DC Halmashauri inamiliki mashine 80 za kielektroniki za kukusanyia mapato. Mashine zilizopo ni za aina mbili:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mashine 15 (Complite POS – zilitolewa na LIC) • Mashine 65 (Smartphone + Thermal printer – zilinunuliwa na Halmashali). <p>Vituo vyote vya kukusanyia mapato vinatumia mashine za kielektroniki.</p> <p>BUHIGWE DC Halmashauri inahitaji mashine za kielektroniki 64; zilizopo ni mashine 50 sawa na 78%. Halmashauri imepanga kununua mashine 14 zinazohitajika kwa mwaka huu wa fedha 2017/18. Matumizi ya mashine za kielektroniki hizi zimesaidia Halmashauri kuongeza ukusanyaji wa mapato kutoka 41% mwaka 2015/16 hadi 94% mwaka 2016/17</p> <p>KASULU MJI Halmashauri ya Mji ilinunua mashine 25 kwa ajili ya kukusanyia mapato katika vyanzo vyake. Kwa wakati huu mashine hizo zinatoshleza mahitaji.</p>
7	<p>Kila Halmashauri iunde Kikosi Kazi cha kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki kwa kutumia mwongozo wa Serikali.</p>	<p>MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI Vikosi kazi 20 vya ukusanyaji taka ngumu vimeundwa kwenye kila kata (kila kata kimoja) na kupewa maelekezo ya uhamasishaji wa jamii kuhusu kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki.</p> <p>KIGOMA DC Halmashauri inaendelea kuhamasisha wananchi kutotumia mifuko ya plastiki, inapokuwa imetumika siku za usafi ambazo ni za Alhamisi ya kila wiki na Jumamosi ya mwisho wa mwezi wananchi wanahimizwa kuhakikisha hakuna mifuko ya plastiki inayozagaa katika maeneo yao.</p> <p>KIBONDO DC Halmashauri imeandika barua kwa wafanyabiashara wote tarehe 26/10/2016 kuhusu kuwa na vifaa vya kutunzia taka ngumu (Dustbin). Aidha, Halmashauri ina wazo la ubunifu la kutengeneza magodoro, mikoba, makapeti na maua kwa kutumia mifuko ya plasti ili kuondoa kuzagaa kwa mifuko ya plastiki.</p>

		<p>KASULU DC Halmashauri iliteua wajumbe wa kikosi kazi tarehe 06/01/2017 kwa barua Kumb.Na.KSDC/M.10/31/35 ili kudhibiti matumizi holela ya mifuko ya plastiki.</p> <p>KAKONKO DC Katika Mji wa Kakonko kuna kikundi cha M3 (Mazingira 3) kinachoshughulikia swala la mazingira na udhibiti wa mifuko ya plastiki. Kwa ngazi ya Vijiji M3 hushirikiana na kamati ya mazingira ya vijiji.</p> <p>UVINZA DC Ili kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastic Halmashauri inatekeleza yafuatayo:-</p> <ul style="list-style-type: none"> • Inaendelea kutoa elimu ya athari za matumizi ya mifuko ya plastiki kwa wananchi. • Kampeni za usafi wa mazingira kila Alhamisi na Jumamosi ya mwisho wa mwezi zinatekelezwa ili kudhibiti taka na kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki, • Ukaguzi maalum wa usafi wa mazingira kwenye makazi na maeneo ya biashara, • WEO/VEO wameandikiwa barua ili kutoa elimu kwa wafanya biashara kutumia vifungashio mbadala, • Halmashauri inaendelea kusimamia sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004 ili kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki. <p>BUHIGWE DC Halmashauri imeunda kikosi kazi chenye wajumbe saba kwa ajili ya kudhibiti mifuko ya plastiki ngazi ya Wilaya. Msisitizo zaidi wa kazi hii umewekwa katika maeneo ya Miji midogo ya Mnanila, Muyama na Buhigwe. Wajumbe hufika maeneo hayo siku ya usafi Alhamisi ya kila wiki kuhimiza usafi ikiwa ni pamoja na kukusanya mifuko yote ya plastiki.</p> <p>KASULU MJI Halmashauri imeunda kikosi kazi kwa ajili ya kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki. Kikosi kinaongozwa na Afisa Usafi na Mazingira wa Halmashauri ya Mji.</p>
8	Sekretarieti ya Mkoa iratibu maandalizi ya mpango wa kuendeleza zao la chikichi, taarifa itolewe katika kikao	Mpango wa Uendelezaji wa zao la Chikichi uliandaliwa na kuwasilishwa katika kikao cha RCC kilichofanyika tarehe 17 Machi, 2017.

	kijacho.	
9	Halmashauri zinazolima zao la chikichi ziweke mkakati wa kukuza kilimo cha michikichi	<p>MANISPAA YA KIGOMA/UJJI</p> <p>Halmashauri ina mkakati wa kuendeleza zao la michikichi. Halmashuri imepanga kupanda miche ya kisasa katika maeneo yote, mfano:- pembeni mwa barabara zaidi km 308 zilizopo Manispaa zitapandwa miche ya michikichi. Kila kaya inatakiwa kupanda miche 5 na kuitunza. Shule za Sekondari na za Msingi, Taasisi zenye maeneo zinatakiwa kupanda miche ya kisasa pamoja na maeneo yote yaliyo wazi yatapandwa michikichi. Ili kufanikisha lengo hili, Manispaa imeanza kutunga sheria ndogo itakayotumika kusimamia mkakati huu.</p> <p>KIGOMA DC</p> <p>Halmashauri ya Wilaya imeweka mkakati wa kuzalisha miche bora ya michikichi chotara (TENERA). Msimu wa kilimo 2016/17 Halmashuri kwa kushirikiana na wadau ambao ni kampuni ya SEED CHANGE na KIPAFADA imezalisha miche chotara 5,484 ambayo imesambazwa na kupandwa mashambani. Ekari 96 zilipandwa miche hiyo kwa msimu wa mwaka 2016/17.</p> <p>KASULU DC</p> <p>Uzalishaji wa zao la michikichi katika Wilaya ya Kasulu ni mdogo kwa sababu miti iliyopo ni ya zamani. Kutokana na zao hili kuwa na uzalishaji mdogo, elimu imetolewa kwa wakulima wa vijiji 8 ambavyo ni Rungwe Mpya Lalambe, Titye, Rusesa, Zeze, Bugaga Kalela na Kwaga ili wapande mbegu mpya bora zenye tija.</p> <p>KAKONKO DC & KIBONDO DC</p> <p>Zao la michikichi halizalishwi katika ya Wilaya za Kakonko na Kibondo</p> <p>UVINZA DC</p> <p>Halmashauri kwa kushirikiana na Kampuni ya SEED CHANGE inaendelea kuwahimiza wakulima wa zao la mchikichi kulima kwa kufuata utalaam ili walime kibiashara. Pia Kampuni ya SEED CHANGE inaendelea kuwauzia wakulima miche bora ya michikichi yenye kuzaa mazao mengi. Halmashauri pia inaimarisha huduma za ugani kwa wakulima wa mazao yote.</p> <p>BUHIGWE DC</p> <p>Maeneo yanayolima michikichi ni Janda, Bukuba, Buhigwe, Kinazi na Munzenze.</p> <p>Mpango wa kukuza kilimo cha zao la michikichi ni kama ifuatavyo:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1) Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa kushirikisha asasi za

		<p>kiraia,</p> <p>2) Kuwa na mashine rahisi za kukamua mafuta,</p> <p>3) Kupata utalamu wa kulima na kuchakata zao hili.</p> <p>KASULU MJI</p> <p>Zao la Michikichi si la kipaumbele kwa wakazi wa Halmashauri ya Mji. Mazao ya kibiashara ni Kahawa na Migomba. Mazao mengine ni yale ya chakula ambayo ni mahindi, maharage, mihogo na miwa. Hata hivyo kutokana na fursa zinazotokana na zao hili la mchikichi, Halmashauri itaendelea kuhamasisha wananchi kulima zao la michikichi.</p>
10	Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa wananchi katika Halmashauri wahamasishwe kulima mazao yanayostahimili ukame.	<p>KIGOMA/UJJI</p> <p>Ushauri unatolewa kwa wakulima kulima mazao yanayostahimili ukame kama vile mihogo. Maafisa ugani waliopo wamewatembelea wakulima kwenye kata zao katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2017/2018. Jumla ya wakulima 720 wamepatiwa huduma za Ugani.</p> <p>KIGOMA DC</p> <p>Halmashauri imeendelea kuhamisha wakulima kupanda mazao ya muda mfupi yanayovumilia mvua kidogo kama mazao ya mihogo, viazi vitamu, maharagwe na mahole.</p> <p>KIBONDO DC</p> <p>Halmashauri imetoa tahadhari na kuwahamasisha wananchi kulima mazao yanayokomaa mapema yanayostahimili ukame kama vile muhogo, viazi vitamu, mtama, magimbi na mbaazi. Tahadhari ilitolewa kwa wananchi kupitia barua yenye kumb. Na HW/DADP/VOL.IV/29 ya tarehe 4/01/2017 kwenda kwa Watendaji wa Vijiji 50 na Kata 19.</p> <p>KASULU DC</p> <p>Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa Halmashauri inawahamasisha wakulima kulima muhogo na sasa upo kwa wingi.</p> <p>KAKONKO DC</p> <p>Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imebarikiwa kuwa na mvua za kutosha kwa muda mrefu, ila pale panapotokea upungufu wa mvua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa wakulima huelekezwa kulima mazao yanayostahimili ukame na kukomaa mapema kama vile viazi vitamu, mtama na Muhogo. Pia kuna skimu za umwagiliaji, mabonde na mito ambavyo husaidia katika uzalishaji wa mazao.</p> <p>UVINZA DC</p> <p>Halmashauri kwa kushirikiana na wadau (TUUNGANE na BTC) inahamasisha wakulima kulima mazao yanayostahimili ukame. Mazao</p>

		<p>ambayo wananchi wanalima ni mihogo na viazi vitamu. Pia kwa mazao ya alizeti na ufuta.</p> <p>BUHIGWE DC</p> <p>Wakulima wameshauriwa kulima mazao yanayostahimili ukame katika kata zote 20 ambayo ni mihogo na viazi vitamu.</p> <p>KASULU MJI</p> <p>Hali ya upatikanaji wa vyakula katika kata zote 15 ni nzuri. Hakuna kata iliyokumbwa na ukame. Mvua za masika zilichelewa kunyesha. Hata hivyo, mvua ziliendelea kunyesha kwa mtawanyiko mzuri na hali ya mazao ni nzuri. Wakulima wanaendelea kulima mazao ya mihogo, viazi, Migomba na Magimbi. Mazao haya pia husaidia wakati wa upungufu wa mvua.</p>
11	<p>Halmashauri ziandae motisha kwa watumishi katika kada zenye upungufu mkubwa na mazingira ya kazi ni magumu</p>	<p>MANISPAA YA KIGOMA/UJJI</p> <p>Suala la motisha kwa kada zenye upungufu mkubwa katika sekta ya elimu na afya limezingatiwa kwenye bajeti ya mwaka fedha 2017/2018 ambapo watumishi wameandaliwa stahili zao zote za kiutumishi.</p> <p>KIGOMA DC</p> <p>Kada zenye upungufu mkubwa wa watumishi ni Elimu na Afya. Halmashauri imeendelea kuongeza nyumba za makazi za watumishi wa Afya na Elimu na kuwapa nafasi za kujiendeleza kielimu husani kwa walimu wa mwambao wa ziwa Tanganyika kata za Ziwani, Kagunga na Mwamgongo.</p> <p>KIBONDO DC</p> <p>Halmashauri inatoa fursa kwa watumishi kujiendeleza kitaaluma pia vibali vya kuhudhuri warsha na semina vinatolewa.</p> <p>KASULU DC</p> <p>Kwa sasa Halmashauri imeweka utaratibu wa kutoa magodoro kwa watumishi wa ajira mpya kwa Idara ya Afya. Aidha katika Idara na Vitengo vingine vilivyobaki Ofisi inaendelea kuweka mipango ya kuwa na motisha za watumishi kwa kuzingatia hali ya upatikanaji wa fedha na ukomo wa bajeti.</p> <p>KAKONKO DC</p> <ul style="list-style-type: none"> • Halmashauri inaendelea kuomba vibali vya ajira ili kuajiri watumishi katika kada zenye upungufu kama afya, elimu na utawala, • Motisha hutolewa kwa watumishi waliopo kwa kuwapatia watumishi bora zawadi kila Mei Mosi. Kwa mwaka 2017/2018 shilingi 1,200,000/= zimetengwa kwa ajili ya zawadi na motisha kwa

		<p>watumishi,</p> <ul style="list-style-type: none"> Kwa upande wa elimu, walimu hupewa zawadi kulingana na ufaulu wa wanafunzi. Katika masomo ya sayansi endapo mwanafunzi atapata alama A mwalimu hupewa shilingi 50,000/=, alama B ni shilingi 30,000/= na masomo ya Sanaa alama A=30,000/= na alama B= 15,000/=. <p>Motisha hizi zinafanya kupunguza ugumu kidogo kwa kada ambazo zinawatumishi wachache walioko kwenye mazingira magumu</p> <p>UVINZA DC Halmshauri imeandaa sera ya motisha ya miaka 3 kuanzia 2017- 2020 kwa watumishi wa kada zote hasa afya na elimu. Sera hiyo inaeleza kuwa watumishi wapya watapewa godoro na kitanda kila mmoja na nyumba watakazoishi watumishi zitawekewa solar na Halmashauri.</p> <p>BUHIGWE DC Halmashauri inatoa motisha kwa watumishi katika kada zenye upungufu mkubwa kama ifuatavyo; 1) Inatoa motisha wa magodoro kwa watumishi wapya wanaoajiriwa. Kwa mwaka 2013/2014 magodoro 50 yalitolewa. 2) Halmashauri ina mpango wa kuwapangia (kuwalipia kodi ya nyumba ya miezi mitatu ya mwanzo) watumishi wapya wa idara ya Afya.</p> <p>KASULU MJI Kada zenye upungufu mkubwa wa watumishi ni Afya na Elimu na Utawala (watendaji wa kata na mitaa). Halmashauri imetenga sh. 63,100,000/= kwa ajili ya motisha katika bajeti ya mwaka 2017/2018.</p>
12	Katika kikao kijacho iwasilishwe taarifa kuhusu Hali ya Maji, Hali ya Afya na Umeme Vijijini Katika Mkoa	Mada hizo zimeandaliwa na zitawasilishwa katika kikao hiki katika agenda namba 5
13	Mkoa ufuatilie hatua za ujenzi wa tawi la Benki Kuu Kanda ya Magharibi Mkoani Kigoma.	Ujumbe wa Maofisa wa Benki Kuu walitembelea Kigoma tarehe 26 -27 Julai, 2017 kwa lengo la kuona maeneo yaliyopendekezwa na Mkoa kwa ajili ya ujenzi wa Tawi la Benki Kuu. Baada ya kukagua maeneo yaliyopendekezwa, maafisa wa Benki Kuu walienda kufanya tathmini na kuchagua kiwanja kilichopo karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa chenye ukubwa wa mita za mraba 11,000. Kiwanja hicho ni eneo la wazi ambalo limekuwa linatumika kwa michezo, maonesho na minada. Hivi sasa Ofisi inaandaa utaratibu utakaofuatwa na BOT ili iweze kumilikishwa kiwanja hicho na kuanza ujenzi

		wa tawi hilo la Benki Kuu.
14	Kila Wilaya itambue Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs, CBOs, FBOs) na kufuatilia shughuli zinazotekelezwa na mashirika hayo	<p>MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI Manispaa imetambua mashirika yasiyo ya Kiserikali 55 ambayo yalihakikiwa na Msajili Mkuu. Mashirika hayo yanafanya shughuli katika sekta za Afya masuala ya Ukimwi, hifadhi ya mazingira kuondoa umaskini, masuala ya vijana, huduma kwa yatima na wajane pamoja na walemavu na shughuli zinazohusiana na maendeleo ya jamii kwa ujumla.</p> <p>KIGOMA DC Halmashauri imetambua mashirika 12 yasiyo ya kiserikali na shughuli za mashirika hayo ni pamoja na kutoa msaada wa kisheria kwa jamii, kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kutoa elimu ya kudhibiti virusi vya UKIMWI na elimu na kuhudumia watu wanaoishi na VVU/UKIMWI majumbani, masuala ya ufundi seremala na ushonaji kwa vijana. Kutoa huduma kwa watoto yatima na akina mama wajane. Masuala ya kuondoa umaskini kwa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake. Masuala ya kilimo, mazingira, afya na elimu dhidi ya Malaria, Uzazi wa mpango na Kifua kikuu.</p> <p>KIBONDO DC Halmashauri imetambua mashirika 9 ambayo yanatoa huduma kwa jamii katika maeneo ya Uhifadhi wa mazingira, msaada wa sheria kwa jamii hususan wanawake na watoto, elimu ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake, na elimu ya kudhibiti UKIMWI katika Jamii.</p> <p>KASULU DC Halmashauri imetambua NGOs, CBOs na FBOs 12 zinazofanya kazi katika Wilaya hyo. Huduma zinazotilewa ni pamoja na; mafunzo na kufanya uhamasishaji katika masuala ya ulinzi wa mtoto, afya ya uzazi, kilimo, ujasiriamali, masuala ya afya, UKIMWI, kusaidia ujenzi wa miundombinu midogomidogo ya elimu, afya na maji.</p> <p>KAKONKO DC Halmashauri imetambua mashirika 30 haya ambayo yanatoa huduma katika sekta za afya, elimu, kilimo, Mazingira, maliasili na maendeleo ya jamii. Mashirika hayo mengine yanafanya kazi kwa wakimbizi na wengine katika jamii.</p> <p>UVINZA DC Jumla ya mashirika yasiyo ya kiserikali 33 yametambuliwa na shughuli kubwa zinazotekelezwa na mashirika hayo ni udhibiti wa maambukizi ya VVU/UKIMWI, uzazi wa mpango, Uhifadhi wa mazingira, Ujasiriamali, ujenzi wa zahanati na VICOBA. Zoezi la utambuzi linaendelea.</p>

		<p>BUHIGWE DC Wilaya ya Buhigwe imetambua mashirika 5 ambayo hufanya kazi katika sekta ya Ardhi katika eneo la matumizi bora ya ardhi, ufugaji wa samaki, nyuki, na elimu ya ujasiliamali kwa njia ya VICOBA. Sekta zinazohusika ni Elimu, Afya, Kilimo, Maji na Maendeleo ya Jamii. Sekta nyingine ni Bishara na Kilimo ambapo unafanyiaka utafiti wa zao la kahawa juu ya namna ya kuzalisha miche bora ya kahawa.</p> <p>KASULU MJI Halmashauri ya Mji wa Kasulu imeyatambua mashirika 11 ambayo yanafanya kazi Kasulu na kazi wanazotekeleza zimetambuliwa.</p>
15	Ili kuharakisha maendeleo ya viwanda vidogo vidogo na vya kati SIDO ipanue wigo wa huduma zake katika Halmashauri zote	<p>SIDO imeendelea kufanya kazi zake kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na kupanua huduma zake ili kushiriki ipasavyo katika kuleta maendeleo ya wananchi katika wilaya zote kama ifuatavyo:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kuna mradi wa miaka 5 wa Youth and Women Empowerment utakaogusa maeneo mbalimbali ya kuendeleza biashara kwa Wilaya za Kasulu Kibondo na Kakonko. Mradi huu unafadhiliwa na timu ya Taasisi za Kimataifa za UN WOMEN, UNDP, UNCDF, UNHCR, ILO, na ITC. SIDO ni moja ya taasisi zitakazo tekeleza mradi huu. Hii ni fursa ya kupanua wigo wa huduma za SIDO katika maeneo hayo. • SIDO imetafuta maeneo katika kila Wilaya na hatua za kuyamiliki zinafanyika. Hii ni moja ya hamasa ya uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo katika Wilaya zote. • SIDO itaendelea kushirikiana na taasisi na miradi mbalimbali iliyopo Mkoa wa Kigoma kwa manufaa ya wananchi wa Mkoa huu.
16	Kila Halmashauri itenge maneo ya Viwanda Vidogo na vya Kati ili kuharakisha maendeleo ya viwanda. Aidha, SIDO watengewe ekari 20 katika eneo hilo kwa ajili ya programu mbalimbali.	<p>MANISPAA YA KIGOMA UJIJI Eneo rasmi linalotumika kwa uwekezaji wa viwanda ni eneo la KISEZ lenye hekta 691 linaloratibiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kigoma, ambapo wawekezaji wanaofika ofisi za Manispaa huelekezwa huko. Kwa upande kutenga eneo la SIDO, wanalo eneo eneo la mlote ndani ya Manispaa ambalo lina ukubwa wa hekta 12.33 ambazo shughuli za viwanda vidogo zinaendelea.</p> <p>KIGOMA DC Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma imetenga eneo ukubwa wa 2.88ha kwa ajili ya viwanda vidogo na kati. Eneo hili limetengwa katika michoro wa Mipango miji, mji mdogo wa Mahembe wenye PT No, 12/KG/40/032014. Eneo hili halijaanza kutumika kwani halijapimwa kisheria na kulipwa fidia.</p> <p>KIBONDO DC Halmashauri imetenga ekari 50 kwa ajili ya SIDO lililopo eneo la Nengo kwa barua ya tarehe 02/12/2016 yenye Kumb. Na.HW/A/L.20/VOL.II.O1</p>

	<p>iliyoandikwa kwa Meneja wa SIDO Mkoa.</p> <p>KASULU DC Halmashauri imetenga eneo kwa ajili ya viwanda vidogo na kati katika kijiji cha Mugombe. Eneo hilo lina ukubwa wa hekta 85 ambapo SIDO wametengewa ekari 25.</p> <p>KAKONKO DC Ekari 50 zimetengwa kwa ajili ya viwanda vidogo katika eneo la Ibuga kata ya Kakonko. SIDO wameshatengewa ekari 20 ndani ya hizi ekari 50 na walishafika Wilayani kuliona na mchakato wa kufanya uthamini kwa ajili fidia utafanyika kwa kutegemea fedha za Serikali Kuu katika bajeti ya mwaka 2017/2018.</p> <p>UVINZA DC Halmashauri imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 53 kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati Makao Makuu ya Wilaya Lugufu, ambapo ekari 22 zitamilikiwa na SIDO kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo vidogo na Ekari 31 zitatolewa kwa wawekezaji wengine watakao kuwa tayari.</p> <p>BUHIGWE DC Halmashauri imetenga ha 30 kwa ajili ya maeneo ya viwanda vidogo na vya kati.</p> <p>KASULU MJI Halmashauri imetenga eneo la hekta 120 kwa ajili ya uwekezaji. Eneo lipo katika kata ya Ruhita, Mjini Kasulu. Tayari SIDO wameshapewa eneo la ha 20 na wameshaweka vizingiti (beacons) katika eneo hilo.</p>
--	---

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAMATI YA USHAURI YA MKOA WA KIGOMA (RCC)
ULIOFANYIKATAREHE 17 MACHI 2017**

NA	AZIMIO	UTEKELEZAJI
1	Halmashauri ambazo hazijakamilisha majengo ya biashara (one business stop center) zikamilishe majengo hayo na yaanze kutumika.	<p>Uvinza DC Jengo liko hatua ya ukamilishaji ambapo linapigwa lipu, kuweka sakafu, kufunga milango na madirisha na rangi ili liweze kuanza kutumika mwezi huu wa Oktoba, 2017.</p> <p>KIGOMA/UJJI MC NA KIGOMA DC Kikao cha majadiliano kati ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kimeshafanyika na kukubaliana kujenga jengo hilo la biashara katika eneo lililoandaliwa na Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Mkandarasi wa kujenga jengo hilo ameshapatikana, kwa sasa tunakamilisha uandaaji wa mkataba wa ujenzi ili tuweze kutuma makubaliano hayo LIC kwa ajili ya kupatiwa fedha za kuanza ujenzi. Matarajio yetu ni kuanza ujenzi huo mwezi huu wa Oktoba, 2017 mara tu baada ya kupokea fedha kutoka LIC.</p> <p>KASULU DC & KASULU TC Halmashauri ya Mji wa Kasulu na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu zinataraajia kujenga jengo la pamoja kwa sh. 50,000,000/=. Maandalizi yamekamiliika na zabuni imeshatangazwa na kumpta Mkandarasi wa kujenga jengo hilo. Gharama alizotenda ziko juu ya 50,000,000/=. hivyo sasa Halmashauri inapitia mchoro kupunguza baadhi ya kazi na gharama za ujenzi (BOQ) ili ziendane na pesa 50,000,000/= inayotarajiwa kutolewa na LIC.</p> <p>KAKONKO DC Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imekamilisha ujenzi wa kituo cha biashara na kwa sasa kinatumika kwa shughuli mbalimbaliza za kiofisi.</p> <p>BUHIGWE DC Mchakato wa kuanza ujenzi ulianza lakini kukawa na changamoto za gharama za mradi kuwa kubwa Tsh 72,000,000 kutokana na Mkandarasi aliyepatikana ukilinganisha na fedha Tsh 50,000,000/= iliyotengwa na LIC. Mazungumzo yalifanywa na Mkandarasi ili kukubaliana kupunguza ukubwa wa kazi na gharama ili ujenzi wa kituo hicho uanze lakini haikuwezekana.</p>

		<p>Halmashauri imeamua kuanza ujenzi wa kituo hicho kwa kutumia <i>Force Account</i> ambapo maandalizi yanafanyika na ujenzi umepangwa kuanza wiki ya pili ya mwezi huu wa Oktoba, 2017.</p> <p>KIBONDO DC</p> <p>Awali Halmashauri ilikamilisha taratibu za manunuzi na kumpata Mkandarasi tangu tarehe 30/12/2016 na ikawa imeomba LIC watoe fedha kiasi cha Tsh.49,689,895 za ujenzi wa jengo hilo. Kuanzia kipindi hicho hadi Agosti 2017 LIC ilikuwa bado haijatoa fedha za ujenzi. Wakati wa kikao cha kuboresha mazingira ya Biashara kilichofanyika Kasulu mwezi Agost 2017, Timu ya Viongozi wa Wilaya iliyohudhuria kikao hicho iliona kuwa kutokana na kuwa ni muda mrefu tangu apatikane Mkandarasi wa kujenga jengo hilo na kwa sababu LIC haijatoa fedha kama ilivyokuwa imeahidi ni vizuri kazi hiyo itangazwe upya. Aidha, kupitia kikao cha Baraza la Biashara kilichofanyika tarehe 27/9/2017, Kikao kiliazimia kuwa Mkandarasi apatikane kabla ya tarehe 10/10/2017 ili kazi ya ujenzi ianze mara moja. Zabuni ilishatangazwa ili kumpata Mkandarasi wa kujenga kituo hicho matarajio yetu ni kuanza ujenzi wa kituo hicho mwezi huu Oktoba, 2017.</p>
2	<p>Kila Halmashauri ianzishe “farm tractor center” ili kuondokana na kilimo cha jembe la mkono. Kama hatua ya mwanzo, kila Halmashauri iandae andiko la mradi huo</p>	<p>UVINZA DC</p> <p>Halmashauri ina vituo vine (4) vya kukodisha matrekta na zana zake kwa wakulima. Vituo hivyo vimewekwa kwa kuzingatia jiografia ya wilaya ili kuweka uwiano ulio sawa wa kuwapatia huduma wakulima wanaoishi mwambao mwa Ziwa Tanganyika na wale wanaoishi nchi kavu. Kutengwa vituo hivi kumelenga kuongeza maeneo ya kilimo na uzalishaji kwa kutumia zana bora na kusogeza huduma kwa wananchi katika wilaya. Vituo hivyo vipo katika vijiji vya Malagarasi, Lugufu, Ilagala, na Kalya kama ifuatavyo: Lugufu (trakta1), Malagarasi (2), Ilagala (1), na Kalya (1)</p> <p>Pia kuna baadhi ya Taasisi za Serikali, watu binafsi, vyama vya ushirika na taasisi zisizokuwa za Serikali zinazomiliki matrekta. Taasisi za Serikali zinazomiliki matrekta ni Kambi ya JKT Bulombora ina matrektor makubwa matano. Aidha matrekta yanayomilikiwa na taasisi, watu binafsi na vyama vya ushirika ni matrekta 26. Halmashauri imejipanga kuandaa andiko kwa ajili ya kuomba tractor na kuongeza vituo zaidi.</p>

		<p>MANISPAA YA KIGOMA UJIJI Halmashauri imepanga kuanzisha farm tractor centre kwa ajili ya kuondokana na kilimo cha jembe la Mkono. Ili kufanikisha shabaha hiyo Halmshauri imepanga kuanza na ununuzi wa tractor kubwa 2, 4wheel drive ambapo itatenga kiasi cha shilingi 150 milioni kwenye Mpango na Bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya utekelezaji.</p>
		<p>KASULU DC Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imeshaanza kuandaa andiko la kuanzisha kituo cha kutolea huduma ya matrekta kwa wakulima (Karakana ya kilimo). Kituo hicho kinatazamiwa kuwa na mtambo wa kung'olea visiki mashambani (excavator) pamoja na matrekta 10. Aidha kituo hicho kitatumika pia kutoa huduma ya matengenezo ya matrekta ya watu binafsi pamoja na kutoa elimu na hamasa ya matumizi ya zana za kilimo kwa wananchi</p> <p>KASULU TC Halmashauri itaanza utekelezaji wa mradi huu kwa kuingiza katika mpango na bajeti ya mwaka 2018/19. Halmashauri pia imeshaandaa andiko kwa ajili ya kuomba fedha za kununulia matrekta pamoja na zana zake.</p> <p>KAKONKO DC Halmashauri imebainisha eneo katika Kata ya Kasuga Kijiji cha Kinonko na Nyakayenzi kwa ajili ya uanzishwaji wa kituo cha kilimo (Farm Tractor center) cha wilaya. Kwa sasa Halmashauri ina trekta 1 ambalo ni bovu linaihitaji matengenezo na haina mtalaamu wa kutumia trekta hilo na kutoa mafuzo kwa Wakulima juu ya matumizi ya trekta hilo na zana nyingine za kilimo zilizopo ambazo zinafaa kutumika. Halmashauri katika Mpango na Bajeti 2017/2018 imeomba kuajiri mtalaamu mmoja na fedha kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Wakulima. Halmashauri itahakisha inatenga fedha katika Mpango na Bajeti ya 2018/2019 kwa ajili ya matengenezo ya trekta lililopo pamoja na kuongeza idadi ya matrekta.</p> <p>BUHIGWE DC Halmashauri ilishaanza kutekeleza mpango wa kuwa na "farm tractor center" ambapo kwa sasa inazo tractor 2 ambazo zinahudumia wakulima kwa utaratibu wa kukodi. Katika msimu wa 2016/2017 zimelima ekari 140. Kwa sasa Wakulima</p>

		<p>wamesha wasilisha maombi ya kulimiwa kwa msimu wa 2017/18.</p> <p>Halmashauri pia imeanza kuandaa andiko la “farm tractor center” ili kulinadi kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kupata zana nyingi zaidi na kuwa na kituo kikubwa na chenye vitendea kazi vya kutosha. Aidha, Halmashauri imepanga kutenga fedha kwenye bajeti ya 2018/2019 ili kununua tractor nyingine moja ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji.</p>
		<p>KIGOMA DC</p> <p>Halmashauri ya Wilaya Kigoma inaendelea kutoa huduma za matrekta kupitia Kituo cha Maendeleo ya Kilimo cha Kata (WARC) kilichopo Kidahwe. Kwa sasa Halmashauri ina Matrekta matatu (3) makubwa, mawili aina ya Farmtrac na moja Sonalika. Hata hivyo kituo kinahitaji maboresho zaidi hususan ununuzi wa samani na zana za kufundishia. Halmashauri imepanga itatenga fedha katika Mpango na Bajeti ya 2018/2019 kwa ajili ya maendeleo ya kituo hicho.</p>
		<p>KIBONDO DC</p> <p>Timu ya wataalamu wa Halmashauri ilipitisha ununuzi wa matrekta matatu ambayo yatawekwa sehemu moja kama “pool” na kuratibiwa kutoka Wilayani kwenda vijijini. Aidha Mh. Mkuu wa Wilaya akiwa Dar es Salaama alifanya mazungumzo na SUMA JKT ya namna Halmashauri inavyoweza kupata na kununua Matrekta. Kila trekta litanunuliwa pamoja na zana zake kwa maana ya jembe la kulimia, harrow pamoja na trela. Kamati ya Fedha imeridhia mpango huo na ikapendekeza fedha za ununuzi ya trekta hizo zitokane na mapato ya ndani hususan uuzaji wa viwanja vya makazi. Aidha andiko la mradi limeandaliwa lipo tayari.</p>
3	<p>Halmashauri ambazo hazijakamilisha agizo la kutengeza madawati zikamilishe kabla ya mwisho wa mwezi Mei, 2017</p>	<p>UVINZA DC</p> <p>Halmashauri ya Uvinza imeshakamilisha utengenezaji wa madawati. Hata hivyo kutokana na uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza 2017 kumekuwepo na ongezeko la mahitaji kwa baadhi ya shule. Taarifa ya utengenezaji wa madawati katika shule za msingi iliyotolewa 13/5/2017 ni kama ifutavyo:</p> <p><i>Idadi ya wanafunzi</i> 69,499</p>

	<table> <tr> <td><i>Mahitaji</i></td> <td>23,166</td> </tr> <tr> <td><i>Yaliyopo</i></td> <td>13,696</td> </tr> <tr> <td><i>Madawati yaliyotengenezwa</i></td> <td>9,623</td> </tr> <tr> <td><i>Jumla ya madawati yaliyopo</i></td> <td>23,316</td> </tr> <tr> <td><i>Ziada</i></td> <td>153</td> </tr> </table>	<i>Mahitaji</i>	23,166	<i>Yaliyopo</i>	13,696	<i>Madawati yaliyotengenezwa</i>	9,623	<i>Jumla ya madawati yaliyopo</i>	23,316	<i>Ziada</i>	153
<i>Mahitaji</i>	23,166										
<i>Yaliyopo</i>	13,696										
<i>Madawati yaliyotengenezwa</i>	9,623										
<i>Jumla ya madawati yaliyopo</i>	23,316										
<i>Ziada</i>	153										
	<p>MANISPAA YA KIGOMA UJIJI Halmashauri imekamilisha agizo la utengenezaji wa madawati, ambapo kwa sasa ina madawati 15,428.</p>										
	<p>KASULU DC Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu hakuna upungufu wa madawati kwa sasa. Halmashauri ina mahitaji ya madawati 20,916, yaliyopo ni 22,591 na kuna ziada ya madawati 1,675 kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa. Jitihada za ujenzi wa vyumba vya madarasa zinaendelea kutegemeana na mapokezi ya fedha na michango ya jamii na wadau</p>										
	<p>KASULU TC Halmashauri ya Mji wa Kasulu kwa sasa haina mwanafunzi anayekaa chini kwa kukosa dawati. Changamoto iliyopo ni uhaba wa vyumba vya madarasa. Kwa sasa madawati yaliyopo ni 13,601 na ndiyo mahitaji kulingana na uwezo wa vyumba vya madarasa vilivyopo. Aidha ujenzi wa vyumba vya madarasa ulioanza mwaka 2016/17 na unaendelea mwaka 2017/18 ukikamilika tutakuwa na mahitaji ya madawati 18,441 na hivyo tutatakiwa kutengeneza madawati 4,840 ili kukidhi mahitaji.</p>										
	<p>KAKONKO DC Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ilikamilisha utekelezaji wa agizo hilo kwa kutimiza madawati 10,304 yaliyokuwa yakihitajika kulingana na idadi ya Wanafunzi na vyumba vya madarasa na madawati hayo tayari yanatumika shuleni. Aidha, kadiri udahili unavyoongezeka ndivyo mahitaji mapya ya madawati yanavyojitokeza. Kwa sasa tunahitaji kuongeza madawati 1,536 ili tufikie idadi ya madawati 11840 ambayo ndiyo mahitaji ya sasa.</p>										
	<p>BUHIGWE DC Agizo hili limetekelezwa na Halmashauri ilikamilisha agizo la kutengeneza madawati kabla ya mwezi Mei, 2017 ambapo ilitimiza madawati 15,677 yaliyokuwa yakihitajika. Aidha</p>										

		<p>tumefanya tathimini baada ya udahili wa wanafunzi wa darasa la kwanza na kubaini ongezeko la mahitaji ya madawati 3,012 hivyo Halmashauri ina jukumu la kutengeneza madawati hayo ili kukidhi mahitaji ya madawati 18,689 yanayohitajika kwa sasa.</p> <p>KIGOMA DC Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ilikamilisha utekelezaji wa agizo hilo kabla ya mwezi Mei, 2017, ambapo iliweza kutimiza idadi ya madawati 16,996 yaliyokuwa yakihitajika wakati huo. Aidha Halmashauri kwa sasa ina ongezeko la mahitaji ya madawati kutoka 16,996 hadi kufikia 20,398. Hivyo upungufu ni madawati 3,402, ambao umetokana na ongezeko hilo la mahitaji limetokana na ongezeko la wanafunzi walioandikishwa Elimu ya Awali na Darasa la kwanza. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inaendelea kuhamasisha na kuomba wadau mbalimbali kuchangia madawati ili kuondoa kabisa upungufu huo na kumaliza tatizo la madawati.</p> <p>IBONDO DC Mahitaji ya madawati katika wilaya na kwa shule za msingi ni 21,140 kwa wanafunzi 63,419. Madawati yaliyopo ni 17,412 na upungufu ni 3,728. Upungufu huu ni mpya na umetokana na kasi na hamasa ya uandikishaji wa watoto wapya wa darasa la kwanza na wale wa awali kutokana na fursa ya Elimu Bure. Katika kuondoa upungufu huu serikali za Vijiji na Kata zimeagizwa kutengeneza madawati yaliyopungua na tayari yameshatengenezwa madawati 50. Halmashauri pia imetenga milioni 30 kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 kwa ajili ya utengenezaji wa madawati.</p>
4	Taarifa za miradi ya Kigoma Grand High School na Kigoma Grand Hospital ziandaliwe na kuwasilishwa katika kikao kijacho	<p>Taarifa zimeandaliwa zitawasilishwa katika mkutano huu.</p> <ul style="list-style-type: none"> - Taarifa ya Kigoma Grand High School itawasilishwa na Mkurugenzi wa Mji wa Kasulu na imeambatishwa iko kwenye krasa 54-56 - Taarifa ya Grand Hospital itawasilishwa wakati wa taarifa ya hali ya huduma za afya katika Mkoa iko krasa 91-92
5	Halmashauri ya Buhigwe ihakikishe soko la Nyamugali linaanza kufanya kazi ifikapo mwezi Juni 2017.	Taratibu za kuanza kulitumia soko la Nyamugali zimeshaanza kwa kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 31/08/2017 ambacho kiliagiza kuwa soko hilo lianze kutumika kila Jumanne ya wiki. Aidha soko hilo lilianza rasmi tarehe 21/09/2017. Kikao hicho pia kiliagiza Halmashauri kutenga fedha za kuweka vyoo na maji katika bajeti ya 2018/19.

6	Halmashauri ya Buhigwe ichunguze sababu za wananchi kutolitumia trekta ya Kijiji na kuchukua hatua za kutatua changamoto hiyo.	Wananchi wa wanaendelea kutumia trekta la kijiji. Kwa mwaka 2016/17, wananchi 48 waliomba kutumia trekta ambapo wananchi 44 walilimiwa ekari 115. Gharama za kulima ni sh 60,000/= kwa ekari. Bei hii ni ndogo ukilinganisha na maeneo mengine. Hata hivyo, Halmashauri itapitia tena gharama hizi. Kwa sasa changamoto ni uchakavu wa trekta ambalo linahitaji matengenezo mara kwa mara.
7	Katibu Tawala wa Mkoa achangea lengo la kuwashirikisha wakulima 100,000 katika mpango wa kuendeleza zao la Chikichi ili ijulikane kila Halmashauri itakuwa na wakulima wangapi.	Lengo la kuwashirikisha wakulima 100,000 katika mpango wa kuendeleza zao la chikichi limechanganuliwa ampapo kulingana na Hali ya uzalishaji na maeneo yanayofaa idadi ya wakulima kwa Halmashauri zilizoko kwenye mpango itakuwa kama ifuatavyo:- Kigoma DCWakulima 44,222 Uvinza DC.....Wakulima 33,166 Kigoma/Ujiji MC.....Wakulima 9,216 Kasulu DC.....Wakulima 8,205 Buhigwe DC.....Wakulima 5,191 Jumla.....Wakulima 100,000
8	Mkoa uandae andiko kamili la mradi wa kuendeleza zao la chikichi	Andiko limeandaliwa na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa barua yenye Kumb. Na.BA.8/131/01/95 kwa ajili ya kusaidia kupata Wafadhili wa kuendeleza zao la Mchikichi. Pamoja na mambo mengine andiko hilo lina mambo yafuatavyo;- i. Hali ya uzalishaji wa michikichi katia Mkoa wa Kigoma, Changamoto zinazoukabili Mkoa katika kilimo cha zao la chikich. ii. Kutafuta wawekezaji wa mashamba ya kati na makubwa. iii. Lengo la Mkoa la kuwa na wakulima 100,000 katika kuendeleza zao la chikichi. iv. Namna ya kupata fedha fedha kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji, v. Uanzishaji wa viwanda vya kusindika malighafi itakayozalishwa kutokana na mazao ya chikichi vi. Kuwa na mnyororo wa thamani wa chikichi na alizeti. vii. Matokeo yanayotarajiwa. viii. Shughuli kuu za kutekelezwa na makadirio ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Mpango huu n.k

9	Zao la chikichi halina bodi – ianzishwe bodi ya zao la chikichi ili kusaidia uendelezaji wa kilimo cha zao hilo.	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imemwandikia barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi yenye Kumb. Na.BA.8/131/01/104 ili kupata utaratibu/mwongozo wa kuanzisha Bodi ya zao la chikichi.
---	--	--

TAARIFA YA UJENZI WA SEKONDARI YA KIGOMA GRAND HIGH SCHOOL

A. UTANGULIZI

Halmashauri ya mji wa kasulu inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa shule ya Kigoma grand High School. Mradi huu kwa wastani upo katika hatua ya ukamilishaji. Utekelezaji wa mradi huu unafanyika kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu na JKT – Mtabila.

Katika utelezaji huo, Halmashauri ya Mji inawajibika katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi na ushauri wa kitaalamu wakati JKT Mtabila wanatoa nguvu kazi, utaalamu na ufundi katika awamu ya kwanza kwa majengo 11. Aidha kwa majengo ya Nyumba tatu zenye kukaa walimu wawili na madarasa 4 yenye kiofisi katikati kwa kuwalipa kiasi cha TZS 50,000,000/= kama gharama za mafundi na awamu ya tatu ya kujenga mabweni 2 yenye wanafunzi 80 kwa kuwalipa kiasi cha TZS 35,000,000/=.

B. MAPOKEZI YA FEDHA

Halmashauri ya Mji imepokea kiasi cha Tshs. **1,300,000,000.00** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Kiasi cha Sh. **48,140,941.29** kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa, Kigoma. Hivyo, fedha kiasi cha Tshs. **1,360,314,379.89** zimepokelewa kwa ajili ya mradi huo hadi kufikia tarehe 11.09.2017 kama inavyooneshwa hapo chini: -

Jedwali la mapokezi ya fedha:-

S/NA	STK NA	TAREHE YA MAPOKEZI	MAHALI ILPOTOKA	KIASI
1	019715	24/12/2016	Wizara ya elimu, sayansi na Technolijia	1,000,000,000
2	019729	26/6/2017	Katibu tawala mkoa	48,140,941.29
3	019733	5/7/2017	Wizara ya elimu, sayansi na Technolijia	300,000,000
4			Mchango wa halmashauri ya Mji	12,173,438.60
			Jumla kuu	1,360,314,379.89

Aidha kiasi cha TZS 48,148,941.29 hizi ni fedha iliyopokelewa kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa Kigoma kwenye fedha zilizobaki kwenye ujenzi wa Jengo la Utawala ambayo ilikuwa michango ya wananchi.

C. MATUMIZI YA FEDHA

Matumizi ya fedha hizo hadi kufikia tarehe 11.09.2017 ni Sh. 1,217,314,258.05.

Jedwali 01.Hatua za utekelezaji katika majengo ya shule ya Kigoma Grand High School.

Na	Majengo	Idadi	Hatua ya utekelezaji	Maelezo
1	Ujenzi wa vyumba vya madarasa	8	Vyumba vinne (4) vimekamilika na vinne (4) vipo katika hatua ya ukamilishaji.	Kazi inaendelea
2.	Ujenzi wa mabweni manne. Mabweni mawili (2) kwa ajili ya wanafunzi 48 kila moja na mabweni mawili kwa ajili ya wanafunzi 80 kila moja	4	Mabweni mawili ya wanafunzi 48 kila mmoja yamefikia hatua ya ukamilishaji. Mabweni mawili ya wanafunzi 80 kila moja yapo katika hatua ya ujenzi wa ya upandishaji wa ukuta.	Kazi inaendelea
3	Ukamilishaji wa jengo la utawala.	1	Jengo limefikia hatua ya ujenzi wa kuta	Maandalizi ya kuendeleza ujenzi yanaendelea.
4.	Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa shule	1	Nyumba ya mkuu wa shule imekamilika	Nyumba imekamilika
5.	Ujenzi wa nyumba za walimu 3 (2 kwa 1)	3	Nyumba za walimu zipo hatua ya upauaji	Kazi inaendelea
6.	Ujenzi wa bwalo moja kwa ajili ya chakula		Bwalo lipo katika hatua ya ukamilishaji.	Kazi inaendelea
7.	Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya maabara	3	Vyumba vya maabara vimekamilishwa	Ujenzi umekamilika
8.	Ujenzi wa vyoo vyenye matundu 18 katika mabweni yote mawili.	2	Vyoo vipo katika hatua ya ukamilishaji.	Kazi inaendelea
9	Ujenzi wa vyoo katika eneo la kufundishia matundu 13	1	vyoo vipo hatua ya ukamilishaji	Kazi inaendelea

Mhe. Mwenyekiti,

Mpaka kufikia June 2017 Halmashauri ilikuwa inadaiwa na watoa huduma wa vifaa mbalimbali kiasi cha TZS **363,876,900** /= kama inavyoonekana kwenye mchanganuo hapa chini:-

NA	MZABUNI ALIYETOA HUDUMA	AINA YA HUDUMA	KIASI(TSH.)
1	M/S GENERAGERERAL SUPPLIY	Vifaa mbali mbali pamoja na milango na madirisha	84,223,600
2	M/S DEUSDEDIT	mbao	127,398,300
3	M/S MALAGARASI ENTERPRISES AND CONTRACTORS LTD.	MCHANGA, KOKOTO NA VIFUSI	31,900,000
4	M/S NDOLIMANA VIBRITED BLOCKS Ndolimana	MATOFALI	19,011,000

5	M/S SEMPA S. KAPULU	VIFAA MBALI MBALI	29,737,000
6		SARUJI	18,700,000
7	Gharama za ujenzi kwa jkt		35,000,000
8	DAYOMA	VIFAA VYA MAABARA	17,907,000
		JUMLA YA MADENI	363,876,900

Aidha kati ya madeni hayo JKT Mtabila tumeshawalipa kiasi 25,000,000/= mwezi Julai 2017 hivyo kubaki na kiasi cha deni tunalodaiwa kuwa TZS 338,876,900/=. Hata hivyo tumeshapeleka maombi ya fedha kiasi cha TZS 1,379,438,301.16 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu yote pamoja na madeni katika shule ya Kigoma Grand zikiwepo na fedha za kukamilishaji wa Jengo la Utawala. Mchanganuo wa fedha zilizoombwa zimeonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:-

JEDWALI LA MCHANGANUO WA FEDHA ZINAZOOMBWA.

S/NA	KAZI ZITAKAZOFANYIKA	KIASI
1	UKAMILISHAJI WA JENGO LA UTAWALA	427,000,000
2	Ulipaji wa madeni	338,876,900
3	UWEKAJI WA UMEME	25,000,000
4	Uwekaji wa maji kwa kuchimba kisima	32,000,000
4	Umalizaji wa majengo yote	556,561,101.16
	JUMLA KUU	1,379,438,001.16

D. CHANGAMOTO

Changamoto iliyopo ni upungufu wa fedha Tshs. 1,379,438,001.16 kwa ajili ya kukamilisha miundombinu yote. Halmashauri imewasilisha maombi ya fedha wazara ya Elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kupewa fedha za kukamilisha mradi huo.

Pamoja na kuwa na madeni kwa wazabuni kazi hii inaendelea kwa kukamilisha mabweni 2 ya wanafunzi 80 pamoja na nyumba tatu za walimu two in one.

E. UANZISHAJI RASMI WA SHULE.

Halmashauri ilikuwa inashauri Shule ya Kigoma Grand High School ifunguliwe rasmi kwa kuingiza wanafunzi wa kidato cha kwanza wenye alama za juu za ufaulu na mwezi wa saba wataingia kidato cha Tano kwa masomo ya Sayansi kama ilivyokusudiwa na mkoa kuwa shule ya Sayansi.

Naomba kuwasilisha.

FATINA H. LAAY
MKURUGENZI WA MJI WA KASULU

**TAARIFA YA MPANGO
NA BAJETI YA MWAKA
2017/18 KAMA
ILIVYOPITISHWA NA
BUNGE**

TAARIFA YA MPANGO NA BAJETI YA MKOA YA MWAKA 2017/2018 KAMA ILIVYOPITISHWA NA BUNGE

1. Maombi Yaliyowasilishwa Kulingana na 'Ceiling' ya Awali:

Mkoa wa Kigoma (Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa) uliwasilisha maombi ya sh. 248,293,155,000. Kati ya fedha hizo, fedha za mishahara zilikuwa sh.176,991,759,000, matumizi mengineyo sh. 14,971,600,000 na fedha za maendeleo sh. 46,124,574,000 na vyanzo vya ndani vya Halmashauri sh. 10,205,222,000.

2. Fedha zilizoidhinishwa

Fedha zilizoidhinishwa ni sh. 205,929,838,000, ambapo sh. 159,680,888,000 (77.5%) ni kwa ajili ya kutekeleza bajeti ya matumizi ya kawaida na sh. 46,248,950,000 (22.5%) ni kwa ajili ya kutekeleza bajeti ya maendeleo.

Fedha za matumizi ya kawaida zimegawanyika ifuatavyo:

- Mishahara (PE) - sh.147,093,297,000
- Matumizi Mengineyo - sh. 8,505,500,000
- Vyanzo vya ndani MSM - sh. 4,082,091,000
- Jumla sh. 159,680,888,000**

Fedha za maendeleo zimegawanyika ifuatavyo:

- Fedha za ndani sh. 26,824,767,000
- Fedha za nje sh.13,301,052,000
- Vyanzo vya ndani MSM sh. 6,123,131,000
- Jumla sh. 46,248,950,000**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliidhinishwa sh. 9,130,403,000 na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishwa sh. 196,799,435,000 kama ilivyooneshwa hapa chini:

2.1 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa:

(a) Fedha za matumizi ya kawaida

- Mishahara: sh. 4,980,488,000
- Matumizi mengineyo sh. 1,437,577,000
- Jumla sh. 6,418,065,000**

(b) Miradi ya Maendeleo

- Fedha za Ndani sh. 2,300,000,000
- Fedha za Kigeni sh. 412,338,000
- Jumla sh. 2,712,338,000**

2.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa:

(a) Fedha za matumizi ya kawaida

• Mishahara:	sh. 142,112,809,000
• Matumizi mengineyo	sh. 7,067,923,000
• Vyanzo vya ndani	sh. 4,082,091,000
Jumla	sh. 153,262,823,000

(b) Fedha za Miradi ya Maendeleo

• Fedha za Ndani	sh. 24,524,767,000
• Fedha za Kigeni	sh. 12,888,714,000
• Vyanzo vya ndani	sh. 6,123,131,000
Jumla	sh. 43,536,612,000

Jedwali Na. 1 linalinganisha bajeti ya mwaka 2016/17 na mwaka 2017/18; Jedwali Na. 2 linaonyesha kwa muhtasari umbile la bajeti ya mwaka 2017/18 na Jedwali Na. 3 linaonesha miradi iliyopitishwa na inatekelezwa mwaka 2017/18.

Jedwali na 1: MLINGANISHO WA BAJETI YA MWAKA 2016/17 NA BAJETI YA MWAKA 2017/18

AINA YA BAJETI	MWAKA 2016/17	MWAKA 2017/18	ONGEZEKO/PUNGUFU	%
Bajeti ya Matumizi ya Kawaida:				
• Mishahara	126,134,165,000	147,093,297,000	20,959,132,000	16.6
• Matumizi mengineyo	13,663,319,000	8,505,500,000	(5,157,819,000)	(37.7)
Jumla Bajeti ya Matumizi ya Kawaida	139,797,484,000	155,598,797,000	15,801,313,000	11.3
Bajeti ya maendeleo:				
• Fedha za Ndani	15,681,760,000	26,824,767,000	11,143,007,000	71.1
• Fedha za Nje	13,278,132,000	13,301,052,000	22,920,000	0.2
Jumla Bajeti ya Maendeleo	28,959,892,000	40,125,819,000	11,165,927,000	38.6
Mapato ya Vyanzo vya ndani	9,987,523,000	10,205,222,000	217,699,000	2.2
JUMLA KUU	178,744,899,000	205,929,838,000	27,184,939,000	15.2

NB: Bajeti ya OC imepungua kwa 37.7% na bajeti ya fedha za maendeleo za ndani zimeongezeka kwa 71.1% kutokana na fedha 'elimu bure' zilizokuwa zikitengwa katika bajeti ya OC kuhamishiwa katika bajeti ya Maendeleo.

Jedwali Na.2: UMBILE LA BAJETI YA MKOA WA KIGOMA MWAKA 2017/18

RS/MSM	Bajeti ya Matumizi ya Kawaida				Bajeti ya Maendeleo				Jumla Kuu
	PE	OC	Mapato ya Ndani	Jumla	Mapato ya Ndani	Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
RS	4,980,488,000	1,437,577,000	0	6,418,065,000	0	2,300,000,000	412,338,000	2,712,338,000	9,130,403,000
Buhigwe DC	14,148,914,000	927,800,000	180,839,000	15,257,553,000	271,258,000	3,609,098,000	1,342,771,000	5,223,127,000	20,480,680,000
Kakonko DC	12,681,264,000	682,208,000	267,930,000	13,631,402,000	401,895,000	2,864,911,000	829,085,000	4,095,891,000	17,727,293,000
Kasulu DC	21,950,286,000	939,808,000	513,030,000	23,403,124,000	769,544,000	2,833,766,000	1,869,743,000	5,473,053,000	28,876,177,000
Kasulu TC	15,346,153,000	742,118,000	497,948,000	16,586,219,000	746,921,000	3,734,709,000	1,100,850,000	5,582,480,000	22,168,699,000
Kibondo DC	19,430,807,000	979,605,000	505,427,000	20,915,839,000	758,140,000	3,200,990,000	1,601,176,000	5,560,306,000	26,476,145,000
Kigoma DC	19,478,442,000	877,057,000	274,051,000	20,629,550,000	411,076,000	2,186,833,000	705,897,000	3,303,806,000	23,933,356,000
Kigoma MC	21,417,688,000	923,934,000	937,946,000	23,279,568,000	1,406,918,000	2,176,830,000	3,784,531,000	7,368,279,000	30,647,847,000
Uvinza DC	17,659,255,000	995,393,000	904,920,000	19,559,568,000	1,357,379,000	3,917,630,000	1,654,661,000	6,929,670,000	26,489,238,000
Jumla MSM	142,112,809,000	7,067,923,000	4,082,091,000	153,262,823,000	6,123,131,000	24,524,767,000	12,888,714,000	43,536,612,000	196,799,435,000
JUMLA KUU	147,093,297,000	8,505,500,000	4,082,091,000	159,680,888,000	6,123,131,000	26,824,767,000	13,301,052,000	46,248,950,000	205,929,838,000
%	71.4	4.1	2.0	77.5	3.0	13.0	6.5	22.5	100.0

RS – Sekretarieti ya Mkoa; MSM – Mamlaka za Serikali za Mitaa

JEDWALI NA. 3: MIRADI INAYOTEKELEZWA KATIKA MKOA WA KIGOMA MWAKA 2017/18 – (TSHS. 000)

CODE	JINA LA MRADI	RS	Kigoma MC	Kasulu TC	Kigoma DC	Kasulu DC	Kibondo DC	Kakonko DC	Buhigwe DC	Uvinza DC	JUMLA-MSM	RS NA MSM
	A: LOCAL FUNDS											
6331	Construction of DC's House (Kasulu)	200,000										200,000
6327	Construction of Govt. Houses (wilaya mpya)	660,000										660,000
6340	Rehab of Regional Block	225,000										225,000
6348	Rehab of RC's House	200,000										200,000
6532	Self Help Project	50,000										50,000
4933	EPZ Development	517,000										517,000
6531	Participatory appraisal	58,000										58,000
5404	Rehabilitation of Regional Hos	220,000										220,000
5499	HIV/AIDS	20,000										20,000
6389	(Divisional Offices)	150,000										150,000
6277	LGCDG		1,282,448	1,420,835	1,268,334	1,880,732	1,448,818	1,157,962	1,521,959	1,892,399	11,873,487	11,873,487
6209	Mfuko wa Jimbo		45,435	44,297	48,021	76,633	56,460	47,360	50,043	71,320	439,569	439,569
6401	Miradi Mingine						400,000	500,000	500,000		1,400,000	1,400,000
	Council building & staff house			1,500,000				700,000	700,000	700,000	3,600,000	3,600,000
4322	Free Primary Edu. Prog		395,271	487,168	583,560	542,052	532,123	347,555	532,407	813,605	4,233,741	4,233,741
4393	Free Secondary Edu. Prog		453,676	282,409	286,918	334,349	763,589	112,034	304,689	440,306	2,977,970	2,977,970
4946	LGA own source projects 60pc		1,406,918	746,921	411,076	769,544	758,140	401,895	271,258	1,357,379	6,123,131	6,123,131
TOTAL - LOCALFUND		2,300,000	3,583,748	4,481,630	2,597,909	3,603,310	3,959,130	3,266,806	3,880,356	5,275,009	30,647,898	32,947,898
	B: FOREIGN FUNDS										0	0
5421	HSBF	171299	486,232	498,495	534,222	1,257,363	1,083,845	473,168	654,118	1,256,983	6,244,426	6,415,725
4628	PFMRP_DIFD	160,000									0	160,000
5405	UNICEF	43,464	0	169,401	0	175,572	173,676	166,801	0	0	685,450	728,914
3280	RWSSP - CBG +DG	37,575	70,144	432,954	171,675	436,808	343,655	189,116	688,653	397,678	2,730,683	2,768,258
6403	TSCP		3,228,155								3,228,155	3,228,155
TOTAL FOREIGN FUNDS		412,338	3,784,531	1,100,850	705,897	1,869,743	1,601,176	829,085	1,342,771	1,654,661	12,888,714	13,301,052
GRAND TOTAL		2,712,338	7,368,279	5,582,480	3,303,806	5,473,053	5,560,306	4,095,891	5,223,127	6,929,670	43,536,612	46,248,950

**JEDWALI NA. 4: MGAWANYO WA FEDHA ZA OC ZA OFISI YA MKUU WA MKOA
KIGOMA**

SUB VOTE	JINA LA SUB VOTE	BAJETI YA MWAKA 2016/2017	BAJETI YA MWAKA 2017/2018
1001	Administration and Human Resource Management	231,975,000	359,651,000
1002	Finance and Accounts Unit	14,000,000	16,240,000
1003	Internal Audit Unit	3,600,000	5,000,000
1004	Procurement Management Unit	5,600,000	7,000,000
1005	DAS Kigoma	23,600,000	26,600,000
1006	DAS Kasulu	25,200,000	28,200,000
1007	DAS Kibondo	26,400,000	29,400,000
1008	DAS Kakonko	26,400,000	29,400,000
1009	DAS Buhigwe	25,200,000	28,200,000
1010	DAS Uvinza	25,200,000	28,200,000
1014	Legal Service Unit	2,800,000	4,000,000
1015	ICT	4,400,000	6,000,000
2001	Planning and Coordination	38,726,000	56,895,000
2002	Economic & Productive Sector	25,501,000	27,500,000
2003	Infrastructure Sector	31,200,000	35,500,000
2004	Social Sector	6,800,000	8,800,000
2005	Local Government Mgt Services	27,200,000	30,200,000
2006	Education	153,233,000	346,791,000
2007	Water Sector	8,800,000	10,000,000
3001	Regional Hospital	657,240,000	354,000,000
JUMLA		1,363,075,000	1,437,577,000

TAARIFA ZA MAENDELEO YA KISEKTA:-

KILIMO-TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KILIMO MSIMU 2016/2017 NA MAANDALIZI YA KILIMO MSIMU WA 2017/2018 MKOA WA KIGOMA

ELIMU-UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ELIMU KATIKA MKOA

MAJI- HALI YA HUDUMA YA MAJI KATIKA MKOA

AFYA- HALI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA KATIKA MKOA

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KILIMO MSIMU 2016/2017 NA
MAANDALIZI YA KILIMO MSIMU WA 2017/2018 MKOA WA KIGOMA**

UTANGULIZI

Sekta ya kilimo katika Mkoa wa Kigoma inatoa ajira kwa karibu asilimia 82 ya wakazi wa Mkoa. Sekta hii huchangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Mkoa na Taifa kwa ujumla. Mkoa unakadiriwa kuwa na eneo linalofaa kwa kilimo la hekta 2, 668,630. Eneo linalotumika kwa kilimo ni takriban hekta 896,895.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KILIMO 2016/2017 NA HALI YA CHAKULA

Katika msimu 2016/2017 Mkoa ulilenga kulima takribani hekta 756,556 za mazao ya chakula zilizotegemewa kuzalisha tani 1,700,988. Kwa upande wa mazao ya biashara jumla ya hekta 91,241 zililengwa kuzalisha tani 132,239.

Tathmini iliyofanyika mwishoni mwa mwezi Mei 2017 inaonyesha kuwa zililimwa hekta 632,200 za mazao ya chakula zilizozalisha tani 1,506,452.80 sawa na asilimia 88 ya lengo, na hekta 27,305 za mazao makuu ya biashara kwa maana ya pamba, tumbaku, kahawa na miwa. zimezalishwa tani 49,162 sawa na asilimia 37 ya lengo.

Katika msimu wa 2016/2017 Mkoa umeendelea kujitosheleza kwa chakula kwakuwa na Ziada ya tani 954,565.73 za chakula aina ya wanga ambapo ziada hii inaendelea kutumika mpaka sasa licha yakuwa na upungufu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, kwakuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji inapokea chakula kutoka Wilaya zenye ziada na Mikoa jirani kama Katavi hivyo kufidia upungufu huu.

Aidha pia hekta 121,548 zililimwa mazao ya jamii ya mikunde na kuzalisha tani 209,323. Uzalishaji huu mzuri unatokana na udongo kuwa na rutuba nzuri pamoja na matumizi mazuri ya pembejeo za kilimo, unyeshaji mzuri wa mvua kwa baadhi ya Halmashauri lakini pia uwajibikaji mzuri wa wananchi katika uzalishaji. Jedwali Na. 1 linaonyesha uzalishaji na mahitaji ya chakula aina ya wanga kwa kila Halmashauri.

Jedwali Na. 1. Hali ya Chakula Mkoa wa Kigoma

H/W	UZALISHAJI (TANI)	IDADI YA WATU	MAHITAJI (TANI)	ZIADA/PUNGUFU (TANI)
Kigoma	149,534.30	240,528	54,870.45	94,663.85
Buhigwe	163,975.00	289,160	65,964.63	98,010.38
Uvinza	416,649.00	436,158	99,498.54	317,150.46
kasulu Dc	358,626.00	484,083	110,431.43	248,194.57
Kasulu Tc	137,230	236,751	54,008.82	83,221.18
Kigoma/Ujiji	17,558.90	244,953	55,879.90	-38,321.00

Kakonko	121,049.65	190,492	43,455.99	77,593.66
Kibondo	141,829.95	297,106	67,777.31	74,052.64
JUMLA	1,506,452.80	2,419,231	551,887.07	954,565.73

CHANGAMOTO ZINAZOKABILI USALAMA WA CHAKULA

- Kuna uvushaji wa chakula kiholela hususani muhogo kwenda nje ya nchi kwa kutumia njia zisizo rasmi kutokana na Mkoa wetu kuwa na mpaka mrefu unaopakana n anchi jirani za Burundi na DRC
- Upungufu wa maghala kwa ajili ya kuhifadha mazao pindi yanapovunwa.

MIKAKATI YA KUPAMBANA NA UPUNGUFU WA CHAKULA NA KUENDELEA KUWA NA ZIADA YA CHAKULA

Ili kuondokana na upungufu wa chakula, Mkoa unaendelea kuhimiza na kushauri yafuatayo: - :

- Kuendelea kuelimisha wananchi kuhakikisha wanahifadhi chakula cha kutosha mara baada ya mavuno kwa ajili ya matumizi ya baadaye katika ngazi ya kaya.
- Kutotumia vibaya chakula kilichopatikana kwa msimu 2016/2017 hususani katika sherehe na kutengenezea pombe za kienyeji.
- Kuhimiza maandalizi ya mashamba mapema ili mvua zianzapo ziwe za kupandia na siyo za kulimia.
- Angalau kila kaya kupanda eka 2 za zao la muhogo.
- Kupanda mazao ya muda mfupi (mfano, kunde, maharage, mahindi ya muda mfupi).
- Kupanda mazao yanayostahimili ukame mfano mtama, muhogo, kunde na viazi vikuu.
- Kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya mito iliyopo na kuvuna maji ya mvua.
- Kuhamasisha na kuimarisha ufugaji wa kuku, bata, samaki na nyuki ili wakulima waweze kuuza na kujinunulia chakula na kujipatia kitoweo.
- Kujenga maghala ngazi za kaya na kuboresha yaliyopo kwa ajili ya kuwa na hifadhi ya chakula cha kutosha na cha uhakika.
- Kudhibiti utorohaji wa chakula kwenda nje ya nchi (mazao yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi sharti yawe na vibali vinavyotolewa na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi).

UPATIKANAJI WA PEMBEJEO ZA RUZUKU ZA KILIMO MSIMU 2016/2017

Msimu 2016/2017 Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iliamua kubadili mfumo wa utoaji wa pembejeo za ruzuku kutoka mfumo wa vocha na kutumia mfumo wa

kusambaza pembejeo za kilimo moja kwa moja hadi kumfikia mkulima lengwa kwa kuitumia Kampuni ya Mbolea Tanzania na Makampuni mbali mbali ya mbegu. Mkoa tulipata mgao wa mbolea ya ruzuku tani 900 ambazo ziligawiwa kwa Halmashauri zote za Mkoa. Jedwali Na. 2 linaonyesha mgao ulivyokuwa.

Jedwali Na.2: Mgawanyo wa pembejeo za Kilimo katika Mkoa.

HALMASHAURI	MGAO	KIASI KILICHOTUMIKA	KIASI KILICHOBAKI
KIGOMA	90	90	0
UVINZA	190	110.1	79.9
BUHIGWE	86	86	0
KASULU DC	214	185	29
KASULU TC	45	45	0
KAKONKO	90	90	0
KIBONDO	158	158	0
KIGOMA/UJIJI	27	27	0
JUMLA	900	791.1	108.9

CHANGAMOTO

- Mbolea kuchelewa kuwafikia wakulima na kukuta tayari mazao yameshaota hivyo kupunguza uhitaji.
- Baadhi ya Mawakala kutokuwa na uwezo wa kusambaza pembejeo kikamilifu.
- Baadhi ya wakulima kutokuwa na fedha za kuweza kununulia pembejeo

MAANDALIZI YA MSIMU 2017/2018

Msimu wa Kilimo katika Mkoa wetu tayari umeshaanza, tumeshazielekeza Halmashauri zetu zote kuendelea kuwahimiza wakulima kufanya maandalizi ya mwisho. Maandalizi yote muhimu ikiwa ni pamoja na kusafisha mashamba, nakuendelea kuyataarisha mashamba kwaajili ya kupanda.

UPATIKANAJI WA PEMBEJEO

Katika msimu wa 2017/2018 serikali kupitia wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imebadili utaratibu wa utoaji wa pembejeo za kilimo ambapo kwa kushirikiana na wadau wake ilifanya marekebisho ya kanuni za mbolea za mwaka 2011 kupitia **The Fertilizer (Amendment) Regulations, 2017** ambayo moja ya marekebisho hayo ni kuhakikisha bei ya mbolea inadhibitiwa na kutoa bei elekezi. Kwa mujibu wa sheria, Mamlaka ya Udhhibiti wa mbolea Tanzania imetangaza bei elekezi kwa mbolea za kupandia (DAP) na kukuzia (UREA), bei hizo zimepangwa kwa kuzingatia gharama za ununuzi wa mbolea kutoka kwenye chanzo, usafirishaji, tozo mbalimbali pamoja na faida ya wafanyabiashara. Aidha maelekezo ya ndani zaidi yapo kwenye mwongozo uliotolewa tarehe 7 Septemba, 2017 na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA ELIMU KATIKA MKOA

1.0. UTANGULIZI

Mkoa wa Kigoma una shule za msingi 151 kati ya hizo za serikali ni 636 na zisizo za serikali ni 15. Shule za sekondari zipo 179, shule za serikali ni 127 na zisizo za serikali 52. Shule za sekondari za juu Kidato cha Tano na Sita ni 16. Vyuo vya Ualimu vilivyopo ni vinne (04) kati ya hivyo viwili (02) ni vya serikali na viwili (02) visivyo vya serikali. Vyuo vitatu (03) ni vya maendeleo ya wananchi (FDC) na chuo kimoja ni cha VETA kilichopo Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Aidha, kuna matawi ya vyuo vikuu hapa Mkoani ambavyo ni St.John, Ekneford, Tawi la chuo cha Uhasibu (TIA) na Tawi la chuo kikuu huria cha Tanzania. Pia kipo chuo cha Hali ya Hewa kilichopo pia Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

2.1 ELIMU YA AWALI NA MSINGI

Mkoa una jumla ya wanafunzi darasa la kwanza hadi la saba 446,018 na Elimu ya awali 62,823 katika shule za msingi 636. Wanafunzi hao wanafundishwa na walimu 6,899 Kimkoa kwa uwiano wa 1:73. Mchanganuo wa hali halisi ya walimu na wanafunzi Kihalmashauri unafafanuliwa katika jedwali lifuatalo:-

2.1A: Takwimu za wanafunzi na walimu Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	IDADI YA WANAFUNZI I - VII	IDADI YA WANAFUNZI ELIMU YA AWALI	JUMLA
1	KASULU DC	65,975	8,729	74,704
2	KIBONDO	63,419	12,381	75,800
3	KIGOMA DC	61,193	7,635	68,828
4	KIGOMA MC	41,069	5,261	46,330
5	BUHIGWE	54,149	8489	62,638
6	KAKONKO	34,206	4009	38,215
7	UVINZA	76,532	10477	87,009
8	KASULU MJI	49,475	5847	55,322
JUMLA		446,018	62828	508,846

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

2.1B: Takwimu za wanafunzi na walimu Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	MAHITAJI YA WALIMU	WALIMU WALIOPO	UPUNGUFU	UWIANO WA MWALIMU KWA WANAFUNZI
1	KASULU DC	1868	673	1195	1:111
2	KIBONDO	1895	862	1033	1:88
3	KIGOMA DC	1721	1176	545	1:59
4	KIGOMA MC	1158	886	272	1:52
5	BUHIGWE	1566	768	798	1:82

6	KAKONKO	955	461	494	1:83
6	UVINZA	2175	1176	999	1:74
8	KASULU MJI	1383	894	489	1:62
JUMLA		12,721	6896	5825	1:73

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

Kwa ujumla tunao upungufu mkubwa wa walimu wa shule za msingi katika Mkoa. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ina upungufu mkubwa zaidi wa walimu kwa uwiano wa 1:111. Hali hii kwa kiasi kikubwa ina athiri ufundishaji na ujifunzaji katika Halmashauri hiyo ukilinganisha na Halmashauri zingine. Uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi uliopangwa kitaifa ni 1:40.

3.1 Miundombinu ya shule za msingi

Hadi kufikia Septemba 1, 2017 hali halisi ya miundombinu katika shule za msingi ilikuwa kama ifuatavyo:-

3.1A: Miundombinu shule za msingi hadi Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	VYUMBA VYA MADARASA			NYUMBA ZA WALIMU		
		MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MAHITAJI	ZILIZOPO	UPUNGUFU
1	KASULU DC	1868	552	1316	1868	155	1713
2	KIBONDO	1895	560	1335	1895	272	1623
3	KIGOMA DC	1721	643	1078	1721	187	1534
4	KIGOMA (M)	1158	365	793	1158	272	886
5	BUHIGWE	1566	582	984	1566	179	1387
6	KAKONKO	955	491	464	955	226	729
7	UVINZA	2175	730	1445	2175	231	1944
8	KASULU MJI	1383	454	929	1383	106	
JUMLA		12721	4377	8344	12721	1628	9816

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

3.1B: Miundombinu shule za msingi hadi Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	MATUNDU YA VYOO			
		WAVULANA		WASICHANA	
		MAHITAJI	VILIVYOPO	MAHITAJI	VILIVYOPO
1	KASULU DC	1340	354	1620	383
2	KIBONDO	1281	377	1570	400
3	KIGOMA DC	1058	387	1224	445
4	KIGOMA (M)	818	192	1005	182
5	BUHIGWE	1160	308	1378	88
6	KAKONKO	763	240	954	307
7	UVINZA	1914	387	1914	400
8	KASULU MJI	1095	262	1393	278
JUMLA		9429	2507	11058	2483

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

Jedwali hapo juu linaonesha upungufu mkubwa wa miundombinu katika shule za msingi na hivyo kila Halmashauri inapaswa ichukue hatua ili kujenga miundombinu hiyo kwa kushirikiana na serikali kuu pamoja na jamii.

4.1 Ufaulu wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi 2016

Pamoja na changamoto ya upungufu mkubwa wa walimu na miundombinu hususani madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo, hali ya ufaulu katika Mkoa wetu inazidi kuimarika ukilinganisha na miaka nyuma.

Katika Mtihani wa kumaliza Elimu ya msingi uliofanyika Septemba, 2016, watahiniwa **26,928** kati yao wavulana **13,468** na wasichana **13,460** walisajiliwa kufanya mtihani huo. Watahiniwa **19,062** wakiwemo wavulana **1,078** na wasichana **8,324** sawa na asilimia **70.79** walifaulu mtihani huo kwa kupata alama kati ya 100 hadi 250 na Mkoa kushika nafasi ya kumi na moja (**11**) kitaifa. Ufaulu huo ni ongezeko la asilimia **16.75** ya ufaulu wa kumaliza Elimu ya msingi (PSLE) 2015 wa asilimia **54.04**. Ufaulu huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na walimu kujituma pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa Halmashauri zetu pamoja na Mkoa. Mkoa pamoja na Halmashauri za Wilaya unaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuongeza ufaulu katika mitihani ijayo hasa kwa kuongeza ufaulu wa watahiniwa wanaopata madaraja ya **A** na **B**. Hatua hii inachukuliwa kwa vile watahiniwa **14,864** waliofanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2016, walipata wastani wa alama **“C”** sawa na asilimia **76** ya watahiniwa **19,062** waliofaulu mtihani huo. Watahiniwa **216** tu kati yao walipata alama **“A”** na watahiniwa **3982** walipata alama **“B”**. Madhara ya wanafunzi wengi kwenda sekondari kwa alama **“C”** ni kwamba wengi hawatamudu kuendelea na Elimu ya Kidato cha **V** na **VII** hivyo kushindwa kwenda vyuo Vikuu.

Ili kuimarisha ufaulu hasa kuwezesha wanafunzi wengi kupata madaraja **“A”** na **“B”** jitihada zifuatazo zinaendelea kuchukuliwa:-

- i. Kuhakikisha walimu wote wanafundisha vipindi vyote kikamilifu (fomu za mahudhuro ya walimu madarasani zinatumiwa na kukaguliwa na Maafisa Elimu Kata);
- ii. Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika shule zetu;
- iii. Kuwajengea uwezo Waratibu Elimu Kata na walimu wakuu ili waweze kusimamia ufundishaji katika Kata na shule zao;
- iv. Kutoa mazoezi ya kutosha kwa kila kipindi baada ya mwalimu kufundisha;
- v. Kila shule kuwa na malengo ya ufaulu hasa kuweka malengo ya kupata alama **“A”** na **“B”** katika kila jaribio linalofanyika shuleni na hivyo uwezekano pia wa kupata alama **“A”** na **“B”** zaidi katika mtihani wa mwisho;
- vi. Kufanya mitihani ya mara kwa mara ya upimaji kwa kushindanisha shule jirani, Kanda, Wilaya na Mkoa;

vii. Kuhakikisha shule inakuwa na vikao vya mabaraza ya shule angalau mara nne (04) kwa mwaka pamoja na vikao vya “klabu ya juu” za wanafunzi ili kuweza kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji shuleni.

viii. Kuimarisha usimamizi wa Elimu kwa kuteua Wakuu wa shule na Waratibu Elimu Kata wenye Elimu ya kutosha, waadilifu na wachapakazi.

5.1 Elimu ya sekondari

Hadi kufikia Mei, 2017 Mkoa ulikuwa na idadi ya wanafunzi **48,348** kati yao wavulana **28,333** na wasichana 20,015 wa Kidato cha kwanza hadi cha sita kwa shule za serikali. Shule zisizo za serikali zilikuwa na wanafunzi **13,650** kati yao wavulana **6,899** na wasichana **6,751** kwa Kidato cha kwanza hadi cha sita. Wanafunzi hao wanafundishwa na walimu **2,444** wakiwemo walimu wa Sayansi na Hisabati **480** na sanaa **1964**. Kati ya walimu **480** wa Sayansi na Hisabati waliopo, walimu **119** ni walimu wapya waliopangwa na serikali miezi ya **Aprili** na **Julai, 2017**. Walimu **19** kati ya waliopangwa hawakuripoti katika Mkoa wetu.

5.1A: Ikama ya walimu shule za sekondari Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	WALIMU WA MASOMO YA SAYANSI			
		MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU	ZIADA
1	KASULU DC	164	61	103	-
2	KIBONDO	152	59	93	-
3	KIGOMA DC	119	55	64	-
4	KIGOMA (M)	193	74	119	-
5	BUHIGWE	91	57	34	-
6	KAKONKO	65	37	28	-
7	UVINZA	288	60	228	-
8	KASULU MJI	114	72	42	-
JUMLA		1186	475	711	-

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

5.1B: Ikama ya walimu shule za sekondari Septemba, 2017.

NA	HALMASHAURI	WALIMU WA MASOMO YA SANAA			
		MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGU FU	ZIADA
1	KASULU DC	240	215	25	-
2	KIBONDO	255	259	-	24
3	KIGOMA DC	268	264	4	-
4	KIGOMA (M)	274	458	-	187
5	BUHIGWE	194	240	-	53
6	KAKONKO	74	134	-	60
7	UVINZA	291	155	136	-
8	KASULU MJI	182	239	-	57
JUMLA		1778	1964	165	381

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

Mkoa una upungufu wa walimu **711** wa Sayansi na Hisabati na ziada ya walimu **381** wa masomo ya Sanaa.

5.2 Miundombinu katika shule za sekondari

Mkoa una changamoto kubwa katika miundombinu kwa shule za sekondari kama inavyofafanuliwa hapa chini:-

5.2A: Hali ya miundombinu shule za sekondari Septemba, 2017

N A	HALMASHAURI	VYUMBA VYA MADARASA			NYUMBA ZA WALIMU		
		MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MAHITAJI	ZILIZOPO	UPUNGU FU
1	KASULU DC	199	176	23	259	62	197
2	KIBONDO	197	149	48	437	126	311
3	KIGOMA DC	191	200	9	287	55	232
4	KIGOMA (M)	221	234	13	202	38	164
5	BUHIGWE	174	170	4	279	83	196
6	KAKONKO	112	109	3	164	45	119
7	UVINZA	205	168	37	258	58	200
8	KASULU MJI	136	99	37	301	37	264
	JUMLA	1435	1305	130	2187	504	1683

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

5.2B: Hali ya miundombinu shule za Sekondari Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	MATUNDU YA VYOO								
		WAV			WAS			WALIMU		
		MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU	MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU	MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU
1	KASULU DC	114	91	23	85	85	0	32	14	18
2	KIBONDO	160	98	62	195	115	80	68	29	39
3	KIGOMA DC	150	129	21	111	103	8	41	41	0
4	KIGOMA (M)	210	141	69	175	120	55	57	27	30
5	BUHIGWE	141	108	33	105	106	-	44	34	10
6	KAKONKO	80	66	14	74	62	12	22	26	-
7	UVINZA	164	109	55	138	117	21	64	34	30
8	KASULU MJI	123	83	40	111	87	24	40	24	16
	JUMLA	1142	825	317	894	795	200	368	229	143

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

5.2C: Hali ya miundombinu shule za sekondari Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	MAABARA		
		MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU
1	KASULU DC	48	3	45
2	KIBONDO	51	19	32
3	KIGOMA DC	57	5	52
4	KIGOMA (M)	57	9	48
5	BUHIGWE	57	4	53
6	KAKONKO	33	9	24
7	UVINZA	54	3	51
8	KASULU MJI	33	3	30
	JUMLA	390	55	335

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

5.2D: Hali ya miundombinu shule za sekondari Septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	BWALO			MAKTABA		
		MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU	MAHITAJI	VILIVYOP O	UPUNGUF U
1	KASULU DC	16	1	15	16	1	15
2	KIBONDO	17	1	16	17	3	14
3	KIGOMA DC	19	1	18	19	-	19
4	KIGOMA (M)	19	1	18	19	3	16
5	BUHIGWE	18	1	17	18	-	18
6	KAKONKO	11	1	10	11	-	11
7	UVINZA	16	1	15	16	4	12
8	KASULU MJI	11	6	5	11	1	10
	JUMLA	127	13	114	127	13	115

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

Maelezo:

Majedwali ya hapo juu yanaonesha upungufu mkubwa wa miundombinu ya shule za sekondari. Hali ya upungufu kwa ujumla ni vyumba vya madarasa 130, nyumba za walimu 1,683, matundu ya vyoo vya wanafunzi wavulana 317, wasichana 200 na walimu 143. Maabara 335, mabwalo 114 na maktaba 115. Upungufu huu ni mkubwa na Mkoa hauna budi kufanya jitihada za pamoja ili kwenda sambamba na wito wa serikali wa kutoa Elimu bora.

Taarifa ya matokeo ya mtihani wa kumaliza Kidato cha pili, nne (2016) na Kidato cha Sita 2017.

Mtihani wa kumaliza Kidato cha Nne (CSEE) 2016, ulifanyika kuanzia tarehe 03.11.2016 hadi 17.11.2016. Watahiniwa 9,492 waliofanya mtihani huo kati yao watahiniwa 7,917

walipata daraja I hadi IV sawa na asilimia **84.03**. Kwa ufaulu huo Mkoa ulishika nafasi ya **4** kitaifa kati ya Mikoa **31** ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtihani wa upimaji wa Kidato cha pili (FTNA) ambao pia ulifanyika Novemba, 2016, jumla ya watahiniwa **12,070** walifanya mtihani huo ambapo watahiniwa **11,495** sawa na asilimia 95 walifaulu mtihani huo na Mkoa wetu kushika nafasi ya kwanza **(01)** kati ya Mikoa **26** ya Tanzania Bara.

Mtihani wa kumaliza Kidato cha Sita (ACSEE) ulifanyika Mei, 2017, jumla ya watahiniwa **1,628** walifanya mtihani huo, kati yao watahiniwa **1,612** walifaulu mtihani huo kwa asilimia **99.02** na Mkoa kushika nafasi ya kwanza kitaifa. Ufaulu huo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za walimu kufundisha kwa bidii mbali na changamoto kadhaa zikiwemo za miundombinu isiyoridhisha katika shule za sekondari zikiwemo upungufu wa maabara na nyumba za walimu.

Utekelezaji wa shughuli mbalimbali kuanzia Januari, 2017 hadi Septemba, 2017.

Mkoa umepokea fedha za Mpango wa Lipa kutokana na Matokeo **(EP4R)** kwa awamu tofauti kuanzia Januari hadi Septemba, 2017 ambazo zimeleaga ujenzi/ukarabati wa shule za msingi na sekondari; kama ifuatavyo:

Ujenzi/ukarabati wa shule za msingi

Fedha kiasi cha **Tshs.240,000,000/=** zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule za msingi Asante Nyerere, Kishanga, Mwibuye na Mwilamvya na ujenzi umefikia hatua mbalimbali. Pia kiasi cha fedha **26,400,000/=** zilipokelewa kwa ajili ya matundu ya vyoo katika shule hizo na ujenzi upo katika hatua mbalimbali.

Fedha **Tshs.20,000,000/=** zimepokelewa mwezi Septemba, 2017 katika shule za msingi Kikungu na Msimbazi kwa ajili ya ukarabati. Fedha kiasi cha **Tshs.180,000,000/=** zilipokelewa kwa ajili ya madarasa **3** katika shule za msingi Kilemba, Kikungu na Msimbazi. Fedha kiasi cha **Tshs.33,000,000/=** zilipokelewa kwa ajili ya matundu **10** ya vyoo katika shule za Kilemba, Kikungu na Msimbazi.

Kiasi cha fedha **Tshs.600,000,000/=** zimepokelewa kwa ajili ya ukarabati shule za sekondari Kibondo wasichana **Tshs.200,000,000/=** na Malagarasi sekondari **Tshs,400,000,000/=**. Aidha, kiasi cha **Tshs.80,000,000/=** zimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule ya sekondari Kibondo. **Tshs,7,380,000/=** kwa ajili ya kumaliza madarasa ya shule ya sekondari Mubondo na **50,000,000/=** kwa ajili ya Maktaba/Maabara katika shule hiyo. Vile vile, Kiasi cha **Tshs.300,000,000/=** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni manne (04) katika shule ya sekondari Muka na Kigoma Grand High School kila shule kujenga mabweni **2**. Tulipokea pia **Tshs.100,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa

jengo la Utawala kwa shule ya Kigoma Grand High School na **Tshs.40,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa darasa.

Kiasi cha **Tshs.140,000,000/=** kilitolewa kwa ajili ya ujenzi madarasa katika shule za sekondari Muka (**60,000,000**) na shule ya sekondari Mkabogo (**80,000,000**) na **Tshs.13,200,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule hizo (Muka sekondari Tshs.6,600,000/=) na Mkabogo sekondari **Tshs.(6,600,000)**.

Kiasi cha fedha **Tshs.1,533,000,000/=** zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa shule za sekondari “**A Level**” kwa shughuli za maabara/ukarabati ujenzi wa madarasa, Bwalo, mabweni na matundu ya vyoo katika shule za sekondari Kasangezi, Kalenge, Muyovozi, Bogwe, Kakonko na Mwandiga. Ujenzi/Ukarabati katika shule hizo upo katika hatua mbalimbali. Mkoa umeelekeza Halmashauri zilizopewa fedha hizo kusimamia kikamilifu matumizi fedha hizo kulingana na maelekezo ya serikali.

Changamoto na mikakati yake

Upungufu wa miundombinu kama vile vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vyoo vya walimu na wanafunzi maabara na maktaba.

Mkoa umeshatoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ili kushirikisha wazazi na wadau wa Elimu katika ujenzi wa miundombinu inayopungua katika shule zilizo katika Halmashauri zao.

Upungufu wa vifaa vya Sayansi na kemikali katika shule za sekondari.

Mkoa umeshatoa mwongozo wa matumizi ya fedha za Ruzuku ya uendeshaji wa shule ili kupunguza tatizo hilo. Mkoa pia umeelekeza Halmashauri za Wilaya kuhakikisha kuwa fedha zote za Ruzuku zinafika shuleni ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kupokelewa na zinatumika kufuata maelekezo na miongozo ya fedha za Serikali.

Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia

Mkoa unaendelea kuzielekeza Halmashauri kuwaelekeza walimu kufaragua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kulingana na mazingira yao.

Madai mbalimbali ya walimu.

Mkoa umeelekea kuratibu madai mbalimbali ya walimu kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwezi Agosti 2017, Mkoa uliwasilisha Ofisi ya Rais – TAMISEMI madeni ya walimu yasiyo ya mishahara ya jumla ya **Tshs.1,674,310,865.12**. Kati ya madeni haya, **Tshs.868,292,601.96** ni ya kuanzia mwezi Januari hadi Juni 2016 na **Tshs.806,018,263.12** ni ya kuanzia mwezi Desemba, 2015 na kurudi nyuma. Madeni hayo yaliyowasilishwa yanahusu likizo, masomo, uhamisho, kujikimu, kustaafu, mazishi, matibabu, lische na stahili za Wakuu wa Idara. Madai yanayohusu mishahara yanashughulikiwa na mfumo wa malipo ya mishahara ya watumishi (lowson) na kulipwa na Hazina kupitia akaunti za watumishi

husika. Madeni ya kuanzia mwezi Julai 2016 hadi Juni 2017 bado yanaendelea kuratibiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Mkoa.

Madeni ya wazabuni wa chakula katika shule za sekondari na msingi za bweni

Mkoa umeendelea kuratibu madeni ya Wazabuni shule za sekondari zenye Vidato ya vya **V** na **VI** za bweni za shule za msingi maalum. Jumla ya fedha **Tshs.919,063,459.71** zimewasilishwa OR – TAMISEMI Mwezi Septemba, 2017 kama madai ya wazabuni wa chakula katika shule za sekondari zenye mabweni na **Tshs.171,850,650/=** za shule ya msingi Kabanga maalum.

Pamoja na kuwasilisha madai haya, shule za sekondari zenye mabweni zimeelekezwa kutumia 50% ya fedha za ada za wanafunzi kwa ajili ya kugharamia chakula na kununua vyakula vyenye gharama nafuu ili kuepuka kulimbikiza madeni.

Uhaba wa madarasa

Mkoa unaendelea kuwahimiza Wakurugenzi washirikiane na wazazi ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo la madarasa linalokabili shule za msingi na sekondari katika Halmashauri zetu.

Baadhi ya shule hazina utaratibu wa kutoa motisha kwa walimu wanaofanya kazi inayotukuka na wanafunzi wanaofanya vizuri katika mtihani.

Mkoa umeshatoa maelekezo kwa walimu Wakuu na Wakuu wa shule ili wabuni namna ya kuwapa motisha walimu na wanafunzi. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa pia kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya motisha kwa walimu.

Uhaba wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati.

Mkoa unaendelea kuwasilisha uhaba wa walimu wa Sayansi na Hisabati OR – TAMISEMI kwa ajili ya kupangiwa walimu kulingana na mahitaji yaliyopo.

Upungufu wa madawati katika shule za msingi

Taarifa ya madawati shule za msingi hadi septemba, 2017

NA	HALMASHAURI	MAHITAJI	YALIYOPO	PUNGUFU	MAELEZO
1	BUHIGWE	18,689	15,677	3,012	Kila Kijiji kukarabati madawati yanayoharibika katika shule yake.
2	KASULU TC	18,441	13,601	4,840	–
3	KASULU DC	20,916	22,591	0	Kuna ziada 1675
4	KIBONDO DC	21,140	17,623	3,517	Kila Vijiji kutengeneza kulingana na mahitaji ya shule na bajeti 17/18 (OS) Tshs.30,M madawati 400.
5	UVINZA	25,511	23,319	2,192	–

6	KIGOMA	20,398	16,996	3,402	—
7	KIGOMA (M)	15,428	15,428	0	—
8	KAKONKO	11,840	10,304	1,536	—
JUMA		152,363	135,539	18,499	

Chanzo: Ofisi ya Elimu Mkoa wa Kigoma

Tatizo la uhaba wa madawati katika shule za msingi bado ni kubwa. Halmashauri zenye upungufu mkubwa wa madawati zinapaswa kuchukua hatua madhubuti za kuondoa mapungufu hayo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



MKOA WA KIGOMA



TAARIFA YA HALI YA HUDUMA YA MAJI MKOANI KIGOMA ILIYOWASILISHWA KWENYE KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC) TAREHE 13 OKTOBA 2017

Imeandaliwa na:
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S. L. P. 125,
KIGOMA

OKTOBA 2017

TAARIFA YA HALI YA HUDUMA YA MAJI MKOANI KIGOMA HADI OKTOBA 2017

1.0 HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

1.1 Utangulizi

Huduma ya maji vijijini inayotolewa kwa sasa inawafikia asilimia **61** ya Wananchi. Huduma hii inatolewa na visima vifupi, visima virefu vyenye pampu za mkono, skimu za maji ya mtiririko, miradi ya kusukuma kwa mashine, chemichemi pamoja na skimu za uvunaji wa maji ya mvua. Baadhi ya miradi ya maji vijijini haifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchakavu. Juhudi za kuifanyia miradi hiyo matengenezo na ukarabati zinaendelea kwa kutumia fedha kutokana na vyanzo mbalimbali hususani Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RWSSP).

1.2 Hali ya Huduma ya Maji Vijijini

Hadi kufikia mwezi Septemba, 2017 asilimia **61** ya wakazi waishio vijijini katika Mkoa wa Kigoma wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia miradi ya maji iliyopo. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika kila Wilaya kwa maeneo ya vijijini ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1**. Wananchi wengi waishio vijijini hutegemea zaidi vyanzo vya maji ya mito, chemichemi zilizohifadhiwa na visima.

Jedwali Na. 1: Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini katika kila Wilaya

Na.	Halmashauri	Idadi ya Watu Vijijini	Idadi ya Watu Wanaopata maji vijijini	Idadi ya Vituo vya kuchotea maji	Asilimia ya watu wanaopata huduma ya Maji
1	Kigoma MC	59,856	31,960	324	53
2	Kigoma DC	217,490	134,664	730	62
3	Kasulu DC	560,543	347,536	1,391	62
4	Kibondo DC	261,435	177,776	712	68
5	Uvinza DC	360,046	157,993	303	44
6	Kakonko DC	167,622	113,983	455	48
7	Buhigwe DC	261,209	175,010	607	67
	JUMLA	1,888,201	1,138,922	4,522	61

1.3 Mpango wa Kuongeza Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini

(a) Miradi Inayoleta Matokeo ya Haraka

Katika hatua za awali za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, utekelezaji ulianza na miradi midogo midogo inayoleta matokeo ya haraka. Miradi hiyo ilitokelezwa katika miaka ya 2007/2008 na 2008/2009. Fedha za kutekeleza miradi hiyo zilisitishwa kutolewa mwezi Juni, 2009 ili kuanza kutekeleza miradi mikubwa ya vijiji 10 katika kila Halmashauri.

(b) Utekelezaji wa Miradi katika Vijiji 10 katika kila Halmashauri

Vijiji vilivyopewa kipaumbele katika kupata huduma ya maji kupitia Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Programu chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma vimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na. 2: Vijiji Vilivyopewa Kipaumbele na Halmashauri katika kutekeleza

HALMASHAURI	VIJJI VILIVYOPEWA KIPAUMBELE
Kigoma DC	Nyarubanda, Kagongo, Nkungwe, Kandaga, Rukoma, Kalinzi
Kigoma MC	Kagera, Kibirizi, Bushabani, Buronge, Mwasenga, Buhanda, Businde, Katonga, Rutale, Mgumire,
Uvinza DC	Kalya, Ilagala, Nguruka , Uvinza
Kasulu DC	Rungwe-Mpya, Kasangezi, Nyarugusu, Nyumbigwa, Kigogwe, Kirungu, Munzeze, Bulimanyi na Nyamugali, Mubanga, Karunga/Heru juu, Munyegera
Kibondo DC	Kiga, Nyankwi, Kibingo, Nyabitaka, Minyinya, Nyagwijima, Muhange, Katanga, Ilabiro, Kiduduye, Kagezi
Buhigwe DC	<i>Hii ni Halmashauri mpya ambayo ina vijiji vya Kigogwe, Kirungu, Munzeze, Bulimanyi na Nyamugali, Mubanga (Vimetoka Kasulu DC)</i>
Kakonko DC	<i>Hii ni Halmashauri mpya ambayo ina vijiji vya Nyagwijima, Muhange, Katanga/Ilabiro, Kiga, Kiduduye (Vimetoka Kibondo DC)</i>

c) Ujenzi wa Miundombinu ya Maji

Hadi kufikia mwezi Septemba, 2017 jumla ya miradi **43** katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma ilipangwa kujengwa, miradi **26** ilikuwa inaendelea na ujenzi na ipo katika hatua mbali mbali, miradi **17** ujenzi wake umekamilika na inatoa huduma ya maji kwa wananchi kama ambavyo inaonekana katika **Jedwali Na. 3**.

Jedwali Na. 3: Miradi iliyopangwa kutekelezwa na inayotekelezwa

Maelezo ya Miradi ya BRN iliyopendekezwa	Miradi iliyopangwa kutekelezwa 2013/14					Miradi iliyokamili shwa hadi Juni 2017	Miradi inayoendelea kutekelezwa 2017/2018
	Kasulu DC	Kibondo DC	Kigoma DC & Uvinza DC	Kigoma MC	Jumla ya Miradi		
Miradi ya Maji ya Vijiji 10 (WSDP)	14	11	10	8	43	17	26
Miradi ya Ukarabati na/au upanuzi	15	9	22	0	46	0	0
Miradi ya Quickwin	10	37	0	0	47	0	0
Miradi ya Kitaifa	1	1	0	0	2	0	0

Aidha, Utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu katika miradi ya maji Vijiji 10 vilivyoainishwa na Halmashauri husika kulingana na fedha iliyotengwa umefanyikia kama ifuatavyo:

- i) Kigoma DC: Vijiji 3 kati ya 6 vimekamiliika na Wananchi wanapata huduma
- ii) Kigoma MC: Kijiji 1 kati ya 8 kimekamiliika na Huduma bado haijaanza kutolewa
- iii) Uvinza DC: Vijiji 2 kati ya 4 vimeanza kutoa huduma, wakati ukamilishaji wa miradi hiyo ukiendelea.
- iv) Kasulu DC: Vijiji 2 kati ya 14 vimekamiliika na Wananchi wanapata huduma. Aidha, vijiji 4 vinapata huduma wakati wakandarasi wanakamilisha ujenzi wa miundombinu.
- v) Kibondo DC: Vijiji 11 kati ya 11 vimekamiliika na Wananchi wanapata huduma. Hata hivyo kuna changamoto za uendeshaji kutokana na miradi yote kutumia nishati ya diesel. Halmashauri inaangalia uwezekano wa kufunga mifumo ya solar ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Jedwali Na. 4: Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji hadi Septemba 2017

Halmashauri	Vijiji vinavyotekelezwa	Hatua iliyofikiwa ya utekelezaji
Kigoma DC	Nyarubanda, Kagongo, Nkungwe, Kandaga, Rukoma, Kalinzi	<ul style="list-style-type: none"> - Miradi ya maji ya Vijiji vya Nyarubanda, Kagongo na Nkungwe imekamiliika kwa asilimia 100 na wananchi wanapata huduma ya maji. - Kandaga (80%) ujenzi unaendelea, Rukoma (80%) ujenzi umesimama, Kalinzi (85%) ujenzi unaendelea
Kigoma MC	Kagera, Kibirizi, Bushabani, Buronge, Mwasenga, Buhanda, Businde, Mgumire,	<ul style="list-style-type: none"> - Mradi ya maji wa Kagera umekamilika kwa asilimia 100, ulikabidhiwa KUWASA kwa ajili ya kuunganisha maji, hadi sasa huduma ya maji kutoka chanzo haijaungwa - Mradi wa Kibirizi (Kibirizi, Bushabani, Buronge,

		Mwasenga, Buhanda, Businde) ulikamilika kwa asilimia 48 na ulikabidhiwa KUWASA, hadi sasa bado haujakamilika. - Mgumire (40%)
Uvinza DC	Kalya, Ilagala, Nguruka , Uvinza	Kalya (95%), Ilagala (80%), Nguruka (67%), Uvinza (70%)
Kasulu DC	Rungwe-Mpya, Kasangezi, Nyarugusu, Nyumbigwa, Munzeze, Kigogwe, Kirungu Munzeze, Bulimanyi na Nyamugali, Mubanga, Karunga, Munyegera	-Miradi ya maji Mubanga, Munyegera imekamilika kwa asilimia 100 na wananchi wanapata huduma ya maji. -Nyumbigwa (99%) Wananchi wanapata huduma -Rungwe mpya (50%), Kasangezi (95%), Munzeze (97%), Nyarugusu (97%), Kigogwe (75%), Kirungu (90%), Bulimanyi na Nyamugali (55%)
Kasulu TC	Herujuu, Muhunga na Kimobwa	Herujuu (90%), Muhunga (96%), Kimobwa (96%)
Kibondo DC	Nyankwi, Kagezi, Minyinya, Kibingo, Nyabitaka, Nyagwijima, Muhange, Katanga, Ilabiro, Kiga, Kiduduye	Miradi ya Minyinya/Nyagwijima, Kibingo/Nyabitaka, Muhange, imekamilika kwa asilimia 100 na wananchi wanapata huduma ya maji -Miradi ya Kagezi/Kiduduye (100%), Katanga/Ilabiro (100%), Nyankwi/Kiga (100%) inatoa huduma na ipo katika vipindi vya matazamiaio.
Buhigwe DC		Halmashauri Mpya hivyo miradi inatekelezwa na Halmashauri Mama
Kakonko DC		Halmashauri Mpya hivyo miradi inatekelezwa na Halmashauri Mama

1.4 Mradi wa WASKiRP unaofadhiliwa na BTC

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji itatekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Halmashauri za Mkoa wa Kigoma (*Water and Sanitation Kigoma Region Projects - WASKIRP*). Miradi hiyo itagharimu **shilingi bilioni 20.6**, kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 18.13** sawa na **Euro milioni 8** zitatolewa na Serikali ya Ubelgiji na **shilingi bilioni 2.44** sawa na **Euro laki 8** zitatolewa na Serikali ya Tanzania. Mradi huo utatekelezwa ndani ya miaka 5 na unalenga kuwapatia huduma ya maji jumla ya wakazi **207,785**. Utekelezaji wa miradi hiyo umeanza kwa kubainisha jumla ya vijiji **26** vya kipaumbele katika Halmashauri za Mkoa wa Kigoma kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Vijiji na Idadi ya Watu watakaonufaika

Halmashauri	Uvinza	Kakonko	Kibondo	Kasulu	Buhigwe	Kigoma DC	Jumla
Idadi ya Vijiji	3	8	1	4	3	7	26

Vijiji vilivyoainishwa	Kazuramimba Nyanganga Zeze	Kakonko Muganza Mugunzu Mbizi Kiziguzigu Kabingo Kiyobera Ruyenzi	Kifura	Nyantare Kigondo Kidyama Nyansha	Mnanila Mwayaya Mkatanga	Kiganza Kibingo Bitare Mkongoro Kizenga Nyamhoza Mwandiga	
Idadi ya Watu (2015)	37,910	28,008	10,005	29,895	27,648	50,186	183,652
Idadi ya Watu (2020)	42,892	31,688	11,320	33,823	31,281	56,781	207,785

Utekelezaji wa mradi huo umeanza kwa kuandaa andiko la ambalo lilikwisha pitishwa na wadau wote. Aidha, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Kigoma imetoa Ofisi zitakazotumiwa na wataalam watakaoshiriki katika utekelezaji wa mradi huo. Mkataba wa utekeleza kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ubelgiji umesainiwa. Vilevile taratibu za ajira kwa wataalam watakaosimamia mradi huo, zinaendelea ambapo meneja wa mradi amejiriwa na ameshaanza kazi. Inatarajiwa utekelezaji wa mradi utanza rasmi mapema mwezi Novemba 2017.

1.5 Fedha za Utekelezaji wa Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa Mwaka 2016/2017 na Mwaka 2017/2018

Katika kipindi cha mwaka **2016/2017**, kiasi cha **Shilingi 15,169,621,000** kilitengwa kwenye bajeti za Halmashauri za Mkoa wa Kigoma. Mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizotengwa kwenye Halmashauri kimeonyeshwa katika **Jedwali Na. 6**. Hadi kufikia Mwezi Juni 2017, Wizara imetuma jumla ya **Shilingi 3,394,331,815.36** kwenda Halmashauri za Mkoa wa Kigoma kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7**

Jedwali Na. 6: Fedha zilizotengwa katika bajeti kwa Mkoa wa Kigoma kwa Mwaka 2016/2017

Mkoa	Halmashauri		Bajeti Fedha za Ndani (Sh)	Bajeti Fedha za Nje (Sh)	Jumla ya Bajeti (Sh)
Kigoma	Buhigwe	DC	932,000,000	351,723,000	1,283,723,000
	Kakonko	DC	932,000,000	261,621,000	1,193,621,000
	Kasulu	DC	3,104,577,000	268,884,000	3,373,461,000
	Kasulu	TC	720,000,000	125,000,000	845,000,000
	Kibondo	DC	848,994,000	274,982,000	1,123,975,000
	Kigoma	DC	1,752,066,000	286,396,000	2,038,462,000
	Kigoma/Ujiji	MC	1,679,724,000	69,860,000	1,749,584,000
	Uvinza	DC	3,252,035,000	309,759,000	3,561,794,000
Jumla	Shilingi		13,221,396,000	1,948,225,000	15,169,621,000

Jedwali Na. 7: Fedha Zilizotolewa kwa Mwaka 2016/2017 hadi Juni, 2017

Mkoa	Halmashauri	Fedha zilizotolewa za Ndani (Tshs)**	Fedha zilizotolewa za Nje (Tshs)	Jumla ya Fedha zilizotolewa (Tshs)
Kigoma	Buhigwe DC	-	45,970,783.03	45,970,783.03
	Kakonko DC	-	28,469,118.59	28,469,118.59
	Kasulu DC	401,472,500.00	29,732,003.93	431,204,503.93
	Kasulu TC	230,317,130.00	13,000,000.00	243,317,130.00
	Kibondo DC	112,881,649.00	308,797,274.39	421,678,923.39
	Kigoma DC	384,042,341.00	204,779,923.04	588,822,264.04
	Kigoma/Ujiji MC	-	575,356,856.97	575,356,856.97
	Uvinza DC	1,029,300,799.00	30,211,436.41	1,059,512,235.41
Jumla (Tshs)		2,158,014,419.00	1,236,317,396.36	3,394,331,815.36

**Fedha zote za Ndani zilizotolewa ni kwa ajili ya kulipia Hati za Madeni ya Wakandarasi zilizowasilishwa Wizarani. Baadhi ya Halmashauri hazijapatiwa fedha za Ndani kwa sababu hawana madeni ya Wakandarasi au wamekamilisha miradi ya Maji kwa Awamu ya Kwanza ya WSDP. Pia, Fedha zote za Nje zilizotolewa ni kwa ajili ya Kampeni ya Usafi wa Mazingira (*Sanitation Hygiene*), ufuatiliaji wa miradi pamoja na kuunda na kuendeleza Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSO) na kwa baadhi ya Halmashauri kukamilisha ujenzi wa miradi.

Tunapenda kuishuruku Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha za kulipa madeni ya wakandarasi wote ambapo katika mwaka 2016/2017 jumla ya **Tsh. 3,394,331,815.36** zilitolewa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kulipwa kwa wakandarasi, usimamizi, uundaji na uendelezaji wa COWSOs pamoja na usafi wa mazingira. Juhudi hizi ziliwezesha wakandarasi wote (isipokuwa Mkandari anayenga mradi wa Rukoma - Kigoma DC), waliokuwa wamesimama kutokana na ukosefu wa fedha, kurudi katika maeneo ya miradi na sasa ukamilishaji wa miradi unaendelea kwa kasi kubwa. Inatarajiwa kuwa miradi yote ya awamu ya kwanza itakamilika ifikapo mwezi Oktoba 2017.

Aidha, katika kipindi cha mwaka **2017/2018**, kiasi cha **Shilingi 13,057,829,000** kimetengwa kwenye bajeti za Halmashauri za Mkoa wa Kigoma. Mchanganuo wa kiasi cha fedha zilizotengwa kwenye Halmashauri kimeonyeshwa katika **Jedwali Na. 8**. Hadi kufikia Mwezi Septemba 2017, Wizara imetuma jumla ya **Shilingi 375,029,804.50** kwenda Halmashauri ya Wilaya wa Uvinza kwa ajili ujenzi wa Mradi wa Maji wa Nguruka. Hati za madai (*Interim Payment Certificates*) za Kasulu DC, Kasulu TC, Uvinza DC na Kigoma DC zimewasilishwa Wizarani ambapo fedha zilizoombwa hazijatumwa kwenye Halmashauri hizo.

Jedwali Na. 8: Fedha zilizotengwa katika Bajeti kwa Mkoa wa Kigoma kwa Mwaka 2017/2018

Halmashauri	Bajeti Fedha za Ndani (Sh)	Bajeti Fedha za Nje (Sh)	Jumla ya Bajeti (Sh)
Buhigwe DC	453,167,000	708,653,000	1,161,820,000
Kakonko DC	997,874,000	214,116,000	1,211,990,000
Kasulu DC	1,655,293,000	471,808,000	2,127,101,000
Kasulu TC	2,901,176,000	447,954,000	3,349,130,000
Kibondo DC	453,167,000	363,655,000	816,822,000
Kigoma DC	453,167,000	196,675,000	649,842,000
Kigoma MC	453,167,000	90,144,000	543,311,000
Uvinza DC	1,775,135,000	1,422,678,000	3,197,813,000
Jumla	9,142,146,000	3,915,683,000	13,057,829,000

1.6 Changamoto za Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini

Katika kutekeleza miradi ya maji Vijijini, Sekretarieti ya Mkoa pamoja na Halmashauri zote zinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i) Mkoa wa Kigoma upo pembezoni na miundombinu ya barabara siyo mizuri hususan wakati wa mvua za masika. Kutokana na hali hiyo wilaya zote hazina wakandarasi wenye sifa wa kutekeleza miradi ya maji. Hii inasababisha kurudia-rudia kutangaza zabuni za miradi ya maji na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi.
- ii) Upungufu wa fedha za usimamizi wa miradi kwa ajili ya RWST na CWSTs na fedha za uendeshaji na matengenezo ya magari;
- iii) Upungufu mkubwa wa wataalamu wa maji katika Halmashauri zote Mkoani. Hii ni baada ya kuwa Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Kasulu na Kibondo kugawanywa na kupata Halmashauri za Wilaya za Uvinza, Buhigwe na Kakonko. Hivyo Watumishi waliokuwepo kwenye Halmashauri mama wamegawanywa katika Halmashauri mpya;
- iv) Ukosefu wa fedha za ukarabati wa miradi ya zamani hasa kwa Halmashauri ambazo hazikupata fedha za *Quickwins*.
- v) Uwezo mdogo wa wataalamu wa maji wa Halmashauri katika eneo la usanifu wa miradi ya maji.

1.7 Mikakati ya kukabiliana na Changamoto katika Huduma ya Maji Vijijini

Ili kutatua changamoto zinazokabili huduma ya maji Vijijini, Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri zimeweka mikakati ifuatayo:-

- i) Kufanya vikao/mikutano mbali mbali na wakandarasi waliopo Mkoani Kigoma kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujenga miradi ya maji. Aidha, Wakandarasi wanashauriwa kuunganisha makampuni ili waweze kuongeza uwezo wa rasilimali watu, fedha, mitambo na kukidhi sifa za kuteuliwa kujenga miradi mikubwa ya maji;
- ii) Mkoa umewasilisha (Wizara ya Maji na Umwagiliaji) mahitaji ya Watumishi wa maji wanaohitajika katika Halmashauri zote na Sekretarieti ya Mkoa. Ufuatiliaji unaendelea ili mahitaji hayo ya rasilimali watu yaweze kupatiwa ufumbuzi. Aidha, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetenga fedha za kuajiri watumishi wa sekta ya maji na vibali mara vitakapopatikana nafasi zilizo wazi zitajazwa mara moja.
- iii) Mkoa unaendelea kuwasiliana na Wizara kuhakikisha fedha ya kutekeleza miradi ya maji iliyopangwa katika bajeti zinapatikana kwa wakati;
- iv) Uhamasishaji wa Wananchi unaendelea ili waweze kuongeza kasi ya kuchangia miradi ya maji. Aidha, mipango ya kuwajengea uwezo wataalam wa maji waliopo imeandaliwa na itatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.
- v) Mkoa umeunda Timu ya Wataalam wa Maji kutoka Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri na Ofisi ya Bonde la Ziwa Tanganyika (*think tank*) ambayo imepewa jukumu la kuzisaidia Halmashauri zenye uhitaji wa usanifu wa miradi ya maji. Timu hiyo ya wataalam wenye uzoefu inawajibika pia kufanya mafunzo mbali mbali kwa wataalam wa Halmashauri katika maeneo ya usanifu na usimamizi wa miradi ya maji.

2.0 HUDUMA YA MAJI MIJINI

2.1 Manispaa ya Kigoma/Ujiji

Huduma za maji na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji zinatolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji (KUWASA). Mamlaka hiyo ilianzishwa kwa sheria ya Maji Sura Na. 281 kwa tangazo la Serikali Na. 61 la tarehe 13 Februari, 1998 ambapo tarehe 1 Julai, 1998 ilipandishwa daraja na kuwa daraja la B.

2.1.1 Hali ya Huduma ya Maji

- Manispaa inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao takribani 242,584.
- Wakazi wanaopata huduma ya majisafi ni asilimia 72% ya wakazi wote
- Mamlaka inategemea chanzo cha maji cha Bangwe, Ziwa Tanganyika
- Uwezo wa uzalishaji wa maji wa chanzo kwa sasa ni wastani wa mita za ujazo 15,000 kwa siku

- Mahitaji halisi ni mita za ujazo 21,600 kwa siku.
- Idadi ya wateja waliosajiliwa kwenye mtandao ni 9,787. Wateja Wateja wenye dira zilizo nzima ni asilimia 50 ya wateja wote.
- Huduma inavyotolewa kwa sasa ni kwa mgao kwa wastani wa siku mbili kwa wiki kwa eneo la mgao.
- Upotevu wa maji(NRW) unakadiriwa kuwa asilimia 28.6 ya maji yote yanayozalishwa.

KUWASA kwa sasa bado haijaanza kutoa huduma za uondoaji wa majitaka. Kupitia mradi wa maji wa MDGI KUWASA imepokea gari la uondoaji wa majitaka vyooni (*Vaccum Truck*).

2.1.2 Changamoto

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zinazoathiri upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji:-

- Gharama kubwa za umeme.
- Uzalishaji wa maji ni mdogo kuliko mahitaji ya wakazi wa Manispaa
- Kuharibika kwa mitambo ya maji mara kwa mara kutokana na uchakavu
- Mtandao wa mabomba uliopo una vipenyo vidogo, ni chakavu na haujaenea kwenye maeneo yote ya Manispaa.
- Mradi wa Maji wa MDGI kuchelewa kukamilika. Mradi ulianza Mwezi Machi 2013 na ulipaswa kukamilika Mwezi Desemba, 2015 lakini hadi sasa umekamilika kwa asilimia 73 na Mkandarasi anasuasua kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha.

2.1.3 Mikakati ya kutatua Changamoto

- KUWASA imefunga pampu mpya mnamo mwezi Januari 2017 ikiwa ni msaada wa kuboresha huduma ya maji kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji, wakati inasubiriwa kukamilika kwa mradi wa maji ulio chini ya programu ya MDGI. Baada ya kufunga pampu mpya uzalishaji umepanda kutoka meta za ujazo 12,000 hadi 15,000 kwa siku. Migao ya maji imeongezeka kutoka mgao wa siku moja kwa wiki hadi wastani wa siku mbili kwa wiki kwa masaa 9 kwa siku.
- Wizara kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Kigoma inatekeleza Mradi mkubwa wa maji ambao hadi kufikia mwezi Agosti 2017, utekelezaji wake umefikia **asilimia 76**. Mkoa umefuatilia kwa muda mrefu kuhusu tatizo la kusuasua kwa mradi tangu mwaka 2014 kuliko sababisha kupungua kasi ya utekelezaji mwishoni mwa mwaka 2016. Ufuatiliaji umefanyika kwa kuanzia kwa Mkandarasi, Mtaalamu mshauri na pia Wizara ya maji na Umwagiliaji. Vikao vimefanyika na mkandarasi amekuwa akiahidi kutafuta fedha za kukamilisha kazi. Wizara ya Maji na Umwagiliaji bado inaendelea kufuatilia ili mkandarasi

aweze kulipwa haraka kila anapokamilisha baadhi ya kazi na kupewa hati ya madai (*Interim Payment Certificates*) ili akamilishe mradi mapema iwezekanavyo na kuwezesha wananchi kupata huduma ya majisafi kufikia tarehe 30 Novemba, 2017.

- KUWASA imefunga mfumo mpya wa kisasa wa taarifa za wateja unaoruhusu ufuatiliaji wa mapato kwa urahisi zaidi na kuruhusu matumizi ya teknolojia za malipo kwa njia ya mtandao kama Mpesa, tigopesa, airtel money n.k. Mfumo huo upo kwenye majaribio na utaanza kutumika rasmi baada ya zoezi la majaribio kukamilika. Lengo la kufunga mfumo mpya ni kuboresha mapato na mfumo wa huduma kwa wateja.

2.2 Mji wa Kasulu

Mji wa Kasulu uko umbali wa Km 90 Kaskazini Mashariki mwa Mji wa Kigoma katika barabara ya Kigoma – Mwanza. Eneo la Mji ni Kilomita za mraba 70. Mji wa Kasulu ulitangazwa kuwa Mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira mwaka 2003 chini ya sheria No. 8 ya mwaka 1997 na baadae kuwa majisafi na usafi wa mazingira chini ya sheria Na. 12 ya mwaka 2009. Mamlaka hii ipo daraja C na ina wajibu wa kutoa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mjini Kasulu.

2.2.1 Hali ya Huduma ya Maji

Huduma ya maji mjini Kasulu hutolewa kwa kutumia miradi ya maji ya kutega kutoka kwenye vyanzo vya vijito viwili vya Nyanka inayozalisha mita za ujazo 1491.8 kwa siku, Miseno mita za ujazo 1609.2 kwa siku na Chemichemi ya Nyakatoke inayozalisha mita za ujazo 346 kwa siku. Wastani wa uzalishaji wa vyanzo hivyo ni mita za ujazo 3,447 kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya mita za ujazo 5,054.

Mji wa Kasulu unakadiriwa kuwa na wakazi 74,442. Wakazi wanaopata huduma ya maji ni 51,587 sawa na 69.3% ya wakazi wote waishio eneo la Kasulu Mjini. Wateja waliounganishiwa maji kwenye mtandao na kusajiliwa ni 3374 na kati ya hao wateja hai ni 2826. Wateja waliounganishiwa dira za maji ni 865 sawa na asilimia 30.6 ya wateja wote hai. Mamlaka inatoa huduma ya maji kwa mgao wa masaa 15 katika eneo la mgao. Upotevu wa maji ni asilimia 45.37 ya maji yote yanayozalishwa hii ni kutokanana wateja walio wengi kutokuwa na mita za maji na mivujo kutokana na mtandao wa mabomba kuwa wa muda mrefu.

2.2.2 Changamoto

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zinazoathiri upatikanaji wa huduma ya maji mjini Kasulu:-

- Mtandao chakavu na usiokidhi mahitaji
- Kutokuwa na dira za kutosha kwa ajili ya kudhibiti upotevu wa maji. Dira za maji 2,000 zinahitajika kwa ajili ya kazi hiyo.
- Wateja wa kawaida na Taasisi za Serikali kutolipia ankara zao za maji kwa wakati.

2.2.3 Mikakati ya kutatua Changamoto

Mamlaka imeanza kutatua baadhi ya changamoto zilizopo kama ifuatavyo.

- Ufuatiliaji wa madeni unafanyika ili kupata mapato ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji na upanuzi wa miundombinu ya maji.
- Mamlaka kwenye bajeti yake ya mwaka 2017/2018 imepanga kununua dira za maji ili kudhibiti upotevu wa maji na vilevile mivujo inadhitiwa kila inapojitokeza.
- Kupitia Mamlaka ya Maji ya Kigoma Mjini, Mamlaka ipo kwenye hatua ya kumtafuta mkandarasi wa kuboresha sehemu ya miundombinu ya maji ya Mjini Kasulu
- Kuomba fedha kupitia bajeti ya Halmashauri ya Mji kwa ajili ya kufanya upanuzi wa mtandao wa maji.
- Kuongeza jitihada katika makusanyo ya maduhuli ili kupata fedha za ziada za kupanua mtandao.
- Kupitia Mamlaka ya Maji ya Kigoma Mjini, Mamlaka ipo kwenye hatua ya kumtafuta mkandarasi wa kuboresha sehemu ya miundombinu ya maji ya Mjini Kasulu kwa fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

2.3 Mji wa Kibondo

Mamlaka ya Maji Kibondo ndicho chombo cha kisheria ambacho kina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa Maji safi na salama yanapatikana kwa wakazi wa eneo la Kibondo mjini. Mamlaka ilianzishwa tangu mwaka 2004. Mamlaka ipo kundi C ambayo inategemea Serikali kulipia gharama za mishahara kwa watumishi waajiriwa, uwekezaji kwa maana ya miradi ya maendeleo pamoja na kulipia gharama za umeme. Mamlaka yenyewe jukumu lake kuu ni uendeshaji na matengenezo kutokana na maduhuli yanayokusanywa kwa kulipia gharama za vibarua pamoja na gharama za uendeshaji na matengenezo ya kila siku.

2.3.1 Hali ya Huduma ya Maji

Mamlaka ya Maji inategemea vyanzo vikuu viwili vya kuzalisha maji kwa wakazi wa Kibondo mjini ambavyo ni maji juu ya ardhi(mto mugoboka) na maji chini ya ardhi, visima virefu saba (07) pamoja na chemichemi zilizohifadhiwa tano (05). Mto mugoboka ndo chanzo kikuu cha maji kwa wakazi wa kibondo mjini. Mji wa Kibondo una wakazi wapatao 33,979. Hitaji la maji kwa siku ni 4,000m³/siku wakati uzalishaji kwa miundombinu iliyopo ni 1,543m³/siku. Aidha maji yanayopotea kutokana na uchakavu wa miundo mbinu kwa sasa yanakadiriwa kufikia 37%. Wateja Hai wanaohudumiwa na Mamlaka kwa sasa wemefikia jumla ya wateja 1,369 kati ya wateja wote jumla ya wateja 275 wamekatiwa huduma kutokana na malimbikizo ya madeni. Kati ya wateja wa

Mamlaka, wateja 594 tu ndiyo waliofungiwa dira za maji sawa na 43.3%. Hadi sasa wakazi wanaopata huduma ya maji ni **asilimia 45.8**

2.3.2 Changamoto

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zinazoathiri upatikanaji wa huduma ya maji mjini Kibondo:-

- Changamoto kubwa inayoikabili Mamlaka ni deni kubwa la ankara ya TANESCO ambalo limefikia shilingi milioni 160.
- Kuwepo kwa mtandao chakavu na usiokidhi mahitaji
- Ukosefu wa chujio unaosababisha maji kuwa na tope jingi hasa kipindi cha mvua
- Wateja wengi kutokuwa na dira za maji

2.3.3 Mikakati ya kutatua Changamoto

- Mamlaka imeomba Halmashauri ya Kibondo kusaidia kulipa deni la umeme.
- Kufuatilia utekelezaji wa kupata kampuni ya ushauri ili kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu iweze kufanyika kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji. Utaratibu wa kutafuta kampuni ya ushauri upo kwenye hatua za awali kwa ajili ya kufanya usanifu, kuandaa michoro na vitabu vya zabuni kwa miji midogo ya Kibondo na Kakonko kwa pamoja. Kazi ya *shortlisting* imeshafanyika chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Hatua inayofuata ni kupata Kampuni ya ushauri na mkataba kusainiwa.
- Aidha kupitia Mamlaka ya Maji ya Kigoma Mjini, Mamlaka ipo kwenye hatua ya kumtafuta mkandarasi wa kuboresha sehemu ya miundombinu ya maji ya Mjini Kibondo kwa fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

2.4 Miji ya Makuu Makuu ya Wilaya Mpya (Uvinza, Buhigwe & Kakonko)

Katika Mkoa wa Kigoma kuna Wilaya mpya tatu zimeanzishwa ambazo ni Uvinza, Buhigwe na Kakonko. Wilaya hizo zina makao makuu katika maeneo ambayo hapo awali yalikuwa ni vijiji. Wilaya ya Uvinza inayo Makao Makuu katika eneo la Lugufu, Wilaya ya Buhigwe Makao Makuu ni kijiji cha Buhigwe na Wilaya ya Kakonko inayo Makao Makuu katika kijiji cha Kakonko.

Hali ya huduma ya maji katika miji hiyo mipya ni kuwa kwa Mji wa **Uvinza ni asilimia 50, Buhigwe ni asilimia 56 na Kakonko ni asilimia 24**. Bado mitandao ya miundombinu ipo katika sura ya huduma ya maji vijijini kwa maana ya huduma inapatikana kwenye vituo vya kuchotea maji. Juhudi za makusudi zimeanza kuchukuliwa kuhakikisha miji hiyo inaboreshewa miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wateja majumbani (*house connection*) wanaunganishwa kwenye mtandao. Aidha, Halmashauri husika zimeelekezwa kuanza taratibu za kuanzisha Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazigira.

Aidha kupitia Mamlaka ya Maji ya Kigoma Mjini, Miji ya Kakonko na Uvinza ipo kwenye hatua ya kuwatafuta wakandarasi wa kuboresha sehemu ya miundombinu ya maji kwa fedha zilizotengwa katika bajeti.

HALI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA KATIKA MKOA

Mkoa una jumla ya Vituo vya kutolea huduma 278, (Hospitali ni 6, vituo vya Afya 32 na zahanati 240) kati yake Vituo vya Serikali ni 235 sawa na asilimia 85% (Hospitali 3, Vituo vya Afya 23 na Zahanati 209). Idadi hii inajumuisha Vituo vya mashirika ya dini, kambi za wakimbizi na binafsi, taasisi za umma kama magereza, Police, Jeshi, TRL n.k.

A: Mchanganuo wa vituo vya huduma za afya kwa mwaka 2017

HALMASHAURI	HOSPITALI		VITUO VYA AFYA			ZAHANATI				JUMLA
	GOV	FBO	GOV	FBO	PRIV	GOV	FBO	PAR	PRIV	
BUHIGWE DC	0	1	2	2	0	23	5	0	1	34
KIBONDO DC	1	0	3	0	1	38	1	1	0	45
KASULU DC	0	0	5	1	1	32	0	0	0	39
UVINZA DC	0	0	5	0	0	35	0	2	2	44
KIGOMA DC	0	0	2	2	0	32	3	2	2	43
KASULU TC	1	1	1	0	0	12	4	1	3	23
KAKONKO DC	0	0	3	0	0	20	3	1	1	28
KIG/UJJI MC	1	1	2	0	2	6	1	4	5	22
JUMLA	3	3	23	5	4	198	17	11	14	
	6		32			240				278

Vituo vingi vya Serikali vya kutolea huduma ya Afya vimejengwa na kuimarishwa kupitia fedha za ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma (JRF) na Mfuko wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM, 2007-2017). Mpango huu umetokana na sera ya Serikali inayosisitiza kuwepo kwa Zahanati kwa kila kijiji na kituo cha Afya kwa kila Kata. Kwa mpango huo utekezaji wa wigo wa MMAM kabla ya ongezeko la vijiji mwaka 2014, Mkoa ulikuwa umefikia asilimia 84 ya mahitaji ya uwepo wa vituo, kwa sasa uwepo wa zahanati kila kijiji ni asilimia 76 upungufu Mkubwa wa vituo upo katika ngazi ya Hospitali za wilaya ambapo Halmashauri 6 hazina kabisa Hospitali, na vituo vya afya vilivyopo ni asilimia 76 ya mahitaji.

UJENZI WA HOSPITALI MPYA YA RUFEE YA MKOA (GRAND REFERRAL HOSPITAL)

Mkoa ulianza mchakato wa ujenzi wa Hospitali Mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma tangu mwaka 2015, ambapo tayari eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika Kata ya Kagera Manispaa ya Kigoma Ujiji lilipatikana. Eneo hilo lipo karibu na miundombinu yote muhimu na tayari wananchi na wadau walianza kuchangia ujenzi wa hospitali hiyo ambapo hadi sasa kiasi cha fedha kilichopo benki ni Tshs 119,420,500. Fedha hiyo inaendelea kupungua kwani kuna Makato ya uendeshaji wa akaunti kila mwezi.

Lengo la kuanzisha hospitali hii lilikuwa ni kuwa na Hospitali ya kisasa na inayoweza kutoa huduma zote muhimu za kibingwa na hivyo kupunguza adha na gharama kubwa kwa wananchi kwenda Dar es Salaam na Mwanza. Hata hivyo ipo changamoto ya kutopata pesa kwa kuwa eneo hilo linahitaji kulipiwa fidia ambayo ilikadiriwa kuwa zinahitajika Sh. billion 1.4 kwa mwaka 2014, gharama hii kwa sasa itakuwa imeongezeka.

Juhudi za kuanzisha Hospitali hii zinafifia kutokana na kutopatikana kwa fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya kulipa fidia na ujenzi wa Hospitali hii. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 zilitengwa Tshs 900,000,000 kwa ajili ya kulipa sehemu ya fidia ya eneo lililotengwa lakini hazikutolewa. Wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya 2016/2017 tuliweza kuwasilisha agenda hii Wizara ya Afya ikaonekana ni ngumu kuifanyia kazi kutokana na fedha nyingi zinazohitajika kulipia fidia pamoja na kuanza ujenzi. Vile vile tulipata taarifa kuwa Jitihada za Wizara ya Afya kwa sasa ni kujenga Hospitali ya Kanda (Mkoani Tabora), hivyo hata kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hatukuweza kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hii bali tulipatiwa fedha Sh. 300 Milioni kwa ajili ukarabati wa miundombinu iliyopo ya Hospitali ya Mkoa. Aidha kutokana na mrudi huu kutotambuliwa na Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha inakuwa vigumu kuutengea fedha katika bajeti ya Serikali.

Mapendekezo:

- Kutokana na kukosa uhakika wa kupata fedha na gharama kubwa za kulipa fidia (1.4 Bilioni), tunapendekeza ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya Rufaa ya Mkoa ufanyike ndani ya eneo la sasa la Hospitali ya Mkoa kwa utaratibu wa *Rehabilitation and Extention* kwa kuwa ujenzi huu hautahitaji kulipa fidia na kupata idhini ya Tume ya Mipango. Bado lipo eneo la kutosha kwa upanuzi na jenzi wa miundombinu ya kisasa ya Hospitali. Ujenzi wa majengo ya ghorofa utasaidia kutumia vizuri eneo lililopo.
- Kwa kuwa fedha zilizochangwa na kuhifadhiwa Benki zinaendelea kupungua kutokana na makato ya kila mwezi, tunapendekeza kiasi cha fedha Tshs 119,420,500 zilizopo zitumike kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan) ya eneo la Hospitali na kuandaa michoro ya majengo yanayohitajika kujengwa ikiwa ni pamoja na kufanya "site plan" ndani ya eneo la Hospitali ya Mkoa ili kuwe na mtiririko mzuri wa huduma.

- Ili kuendelea kuimarisha huduma za afya katika Hospitali ya Mkoa, upo mpango wa kukarabati Jengo liliokuwa linatumika kwa ajili ya shughuli za Kliniki ya mama na mtoto ili litumike kwa ajili ya huduma kwa wagonjwa wanaotumia huduma ya Bima ya afya (NHIF) pamoja na kufungua duka la Hospitali. Ukarabati huo unategemea kutumia fedha za uchangiaji, kutokana na mapato kupatikana kidogo, hivyo tunapendekeza sehemu ya fedha hizo zikopwe ili kukamilisha kazi hiyo. Taratibu za kufanya manunizi zinaendelea, fedha hizo zitarejeshwa kwa awamu kila mwezi baada ya duka kuanza kufanya kazi pamoja na asilimia ya fedha za NHIF pindi zinapoletwa.

B: HALI YA WATUMISHI KATIKA MKOA.

Mahitaji ya watumishi wa sekta ya afya kwa mujibu wa Ikama mpya ya mwaka 2014 katika vituo vya umma kimkoa ni 5,007 Idadi ya watumishi waliopo ni 1,611 sawa na asilimia 32 ya mahitaji.

Mchanganuo wa mahitaji na hali ya watumishi katika Halmashauri kwa mujibu wa ikama ni kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

JINA LA HALMASHAURI/WILAYA	ZAHANATI	KITUO CHA AFYA	HOSPITALI	R/CHMT	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU	%
BUHIGWE DC	345	78	0	8	431	144	287	67
KIBONDO DC	570	117	200	8	895	284	611	68
KASULU DC	480	195	0	8	683	120	563	82
UVINZA DC	525	195	0	8	728	142	586	80
KIGOMA DC	480	78	0	8	566	122	444	78
KASULU TC	180	39	200	8	427	220	207	48
KAKONKO DC	300	117	0	8	425	138	287	68
KIGOMA UJIJI	90	78	200	8	376	210	166	44
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA	0	0	468	8	476	231	245	51
TOTAL	2970	897	1068	72	5007	1611	3396	68

Halmashauri za Kasulu, Uvinza na Kigoma ndizo zina idadi ndogo zaidi ya watumishi ikilinganisha na mahitaji. Mchanganuo wa hali ya Madaktari na Wauguzi katika mkoa ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.

NA.	KADA	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU	%UPUNGUFU
1	MADAKTARI BINGWA	21	3	18	86
2	MADAKTARI (GP)	68	22	46	68
3	MADAKTARI WASAIDIZI (AMO)	118	43	75	64
4	TABIBU/TABIBU WASAIDIZI	421	158	263	62
5	WAUGUZI	1537	641	896	58
6	MADAKTARI WA MENO/ FUNDI SANIFU	13	2	11	85
7	MAABARA/WAAIDIZI	280	15	265	95

8	WATEKNOLOJIA -DAWA	35	9	26	74
9	WAFAMASIA	10	7	3	30
	JUMLA KUU	2503	900	1603	64

C: HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI NA MTOTO

VIASHIRIA VYA HALI YA AFYA YA BABA, MAMA NA MTOTO KIGOMA

Takwimu mbalimbali zinazotokana na tathmini endelevu kwa mkoa wa Kigoma zinazofanywa kwa ushirikiano wa uongozi wa mkoa na CDC zinawekwa kwa uchache kwenye jedwali linalofuata hapa zikilinganiswa na hali halisi ya nchi nzima ya Tanzania;

Jedwali 1. Hali ya afya ya uzazi kwa mkoa wa Kigoma(2016) na Tanzania (2015/16)

Kiashiria	Mkoa wa Kigoma ¹	Tanzania ²
IDADI YA Vituo vinavyotoa huduma za RCH	245	
Idadi ya vizazi kwa mwanamke(total fertility rate (births per woman)	6.5	5.2
Mahudhurio manne(4) ya clinic ya wajawazito ³	43.1%	50.7%
Waliozalishwa na wahudumu wenye ujuzi(Delivered by a skilled provider) ³	58.7%	63.7%
Waliozalishwa kwa upasuaji (Delivered by Cesarean section) ³	5.1%	5.9%
Wanaotumia njia za uzazi wa mpango (women in union)	20.0%	32.0%
Wanaojifungulia vituoni (Zahanati, Vituo vya afya au Hospitali)	59.6%	62.6%
Uhitaji wa njia za uzazi wa mpango(Unmet need for FP(women in union)	39.2%	25.3%
Kiwango cha chanjo	95	
¹ 2016 Kigoma Reproductive Health Survey (CDC, 2015)		
² 2015-16 Tanzania Demographic and Health Survey (NBS, 2011&2016)		
³ Births since January 2009		

Maelezo zaidi

- Mwanamke wa kigoma ana wastani wa kuzaa mara saba ambapo ni wastani wa juu Zaidi ya wastani uliopo wa kitaifa
- Mahudhurio ya kliniki kwa mama wajawazito yako chini Zaidi hata ya wastani wa Taifa na chini ya kiwango kilichowekwa na shirika la afya duniani
- Utumiaji wa njia za uzazi wa mpango uko chini ya kiwango cha utumiaji kwa taifa
- Wakina mama wajawazito ambao wanajifungua nje ya vituo vya huduma kwa mkoa wa kigoma ni wengi Zaidi ukilingaisha na wastani wa taifa

Hata hivyo bado kasi ya kuboreka kwa viashiria hivyo imekua ndogo kuliko kasi na malengo ya kitaifa. Halikadhalika, kwa masikitiko makubwa, idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi imeongezeka sana kutoka 68(2015) mpaka 96(2016), 86 kati ya hivyo vikiwa vimetokea kwa vituo vya kutolea huduma. Hali hii imechangiwa na mambo mbalimbali ikiwemo miundombino finyu ya kutolea huduma, upungufu mkubwa wa watoa huduma wenye ujuzi, udhaifu wa mfumo wa rufaa na upungufu wa dawa na vifaa tiba.

Wakinamama 10,614 wenye matatizo ya dharula ya uzazi kati ya 68,156 waliojifungua walipata changamoto mbalimbali za uzazi zilizo hitaji utaalumu kuokoa maisha yao au kuzuia wasipate madhara ya kudumu.

D: HUDUMA ZA UPASUAJI WA DHARULA

Huduma za upasuaji wa dharura zinatolewa kwenye vituo 23 (vituo vya afya 17 na 6 Hospitali). Maeneo ya vijijini yamepewa kipaumbele kikubwa ambapo, mpaka sasa huduma hii inatolewa katika vituo vya Afya Kakonko, Nyanzige, Mabamba, Kifura, Nyenge, Kiganamo, Shunga, Nyarugusu, Matyazo, Bitale, Ujiji, Nguruka, Buhingu, Ilagala na Muyama. Aidha, kituo cha Kalya kimekamilika, kazi za upasuaji zimekwama kuanza kutokana na kutokuwa na Daktari wa kufanya upasuaji.

Mkoa umeendelea kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, ikiwa ni pamoja na Kipindupindu. Tarehe 05/09/2017 Mkoa ulipokea taarifa ya kuwepo kwa wagonjwa wanaodhaniwa kuwa na kipindupindu katika manispaa ya Kigooma Ujiji. Tarehe 05/09/2017 Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ilipokea wagonjwa wawili waliokuwa wanahisiwa kuwa na dalili za Ugonjwa wa Kipindupindu ambapo baada ya uchunguzi wa maabara waligundulika kuwa na vimelea vinavyosababisha kipindupindu. Kulikua na jumla ya wagonjwa 51 na wagojwa 2 walifariki kwa kipindi cha kuanzia tarehe 05/09-21/09/2017. Maeneo yalioathirika ni Kibirizi, Gungu, Kararangabo na Ujiji. Mpaka sasa hakuna mgonjwa aliyepatikana akiwa na kipindupindu.

HATUA ZA KIUTAWALA ZILIZOCHUKULIWA

- ▶ Kuzitaarifu mamlaka husika kuhusu uwepo wa mlipuko wa kipindupindu (Mkoa, KM- OR TAMISEMI, KM- AFYA)
- ▶ Kutoa maelekezo kwa Hamashauri kufungua kambi ya matibabu ya kipindupindu
- ▶ Kutoa tahadhari na maelekezo kwa Wakurugenzi na Waganga Wakuu wa Halmashauri hususani Uvinzana na Kigoma DC
- ▶ Kuongea na wadau mbalimbali kusaidia namna ya kukabiliana na ugonjwa huu ambapo mashirika ya UNICEF na UNIHCR walitoa lita 7000 za maji (Ringers Lactate) na vidonge vya kutibu maji.

HATUA ZA KITAALAMU ZILIZOCHUKULIWA

- ▶ Timu ya Wataalamu kutoka ngazi ya Mkoa, ilikutana na timu ya Maafisa Afya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji na kutoa maelekezo ya namna ya kudhibiti kuenea kwa mlipuko huo.
- ▶ Sambamba na hili Mkoa ulitoa vifaa tiba kama ifuatavyo;
 - Boksi 5 zavidongevya **Water guard** zenye Paketi 3,200 zavidonge 10 kilapaketi
 - Boksi 10 za **Water Purifiers** zenye paketi 240 kila boksi moja sawa na paketi 2400.

- ▶ Kuendelea kutoa elimu ya afya juu ya matumizi ya vyoo na utumiaji wa maji safi na salama. Pia, kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na usimamizi wa sheria za usafi, mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi na utoaji wa chanjo ya kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yameathirika zaidi.

Shughuli za usafi wa mazingira zilizofanyika kwa Julai-Septemba 2017

- Usimamizi shirikishi kuangalia utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira katika Wilaya, kata na vijiji.
- Kutoa motisha kwa kaya ambazo zilifanya vizuri katika uboroshaji wa vyoo ili kuvutia wengine kufanya vizuri zaidi. Jumla ya doti 10 za kanga zenye ujumbe wa Usafi wa Mazingira zilitolewa kwa kaya mbalimbali katika vijiji vya kibondo na Kakonko.
- Kuelekeza timu za wataalamu wa Mfumo wa Takwimu wa NSMIS kuanzakuizingiza Takwimu ambazo zilikuwa Hazijaanza kuingizwa kwenye mfumokama vile taarifa za;

-Afya na Usalama sehemu za kazi (Occupational Health and Safety)

-Majina na Usafi wa Mazingira katika Vituo vya Kutolea huduma za Afya (WASH in HCF)

-Maji salama na Usafi wa mazingira katika shule za Msingi na Sekondari (SWASH) Ukaguziwa Ubora na Usalama wa chakula (Food Safety) na Ukaguzi wa mazingira wa kila mwezi.

- Kukagua ujenzi wa vyoo na hali ya Usafi wa mazingira katika shule zinazotekeleza kamapeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira.
- Kufanya vikao na timu ya Maafisa Afya wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kusikiliza changamoto za utendaji kazi.
- Kuongeza morali ya maafisa Afya wa Manispaa baada ya kujadili kwa pamoja namna ya kushughulikia changamoto zinazowakabili, hususani baada ya kufanikiwa kupata Msaada wa Tsh. 11,348,000/- kutoka UNICEF kwa ajili ya kuimarisha Msukumo wa Usafi katika Manispaa ya Kigoma Ujiji.

E: HALI YA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI.

Kulingana na matokeo ya utafiti wa Malaria na UKIMWI (THIMS, 2007/08) uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu uliaonesha kuwa Mkoa wa Kigoma ulikuwa kiwango cha maambukizi asilimia 1.8 ambapo wastani wa Kitaifa ulikuwa asilimia 5.7. Utafiti wa mwaka 2011/12 imeonesha kuwa maambukizi yamefikia asilimia 3.4% ambapo yale ya kitaifa yamepungua kutoka 7.4% hadi kufikia 5.1. Hata hivyo vituo vinavyotoa huduma ya upimaji wa VVU imeongezeka kutoka vituo 6 (2005) hadi kufikia vituo 239 Mwaka 2015 na kutoka 239 hadi kufikia 262 kufikia 2017.

Vituo vinavyotoa huduma ya matunzo na tiba kwa wanaoishi na VVU (CTC) imeongezeka kutoka vituo 33 mwaka 2015 hadi vituo 67 Mwaka 2017. Hata hivyo zipo juhudi ili kuhakikisha kuwa vituo vinaongezeka kufikisha huduma kwa jamii hasa kwa kuzingatia kuwa sasa tunakwenda kwenye utaratibu mpya wa **kupima na kutibu**.

Katika Kipindi cha April- Juni 2017 jumla ya watu 41,986 walipima Afya zao Me 17,903, KE 24083 kwa njia mbalimbali kupitia vitengo vya VCT, PMTCT, PITC. Kati ya walio pima walio gunduliwa kuwa na maambukizi walikuwa 646 (ME 185, KE 461) (1.5%). Huduma ya Ushauri nasaha na Upimaji wa VVU inatolewa katika vituo 262 (Hospitali zote za Mkoa wa Kigoma, vituo vya Afya na zahanati). Pia huduma za kuzuia maambuki kutoka kwa mama kwenda kwa Mtoto (PMTCT) inatolewa katika vituo 245 vya kutolea huduma.

Sababu zinazochangia kuwepo maambukizi ya UKIMWI ni :-

- Kuwepo kwa jumuiiko kubwa la watu katika kambi za wavuvi kando kando ya ziwa Tanganyika.
- Umaskini wa kipato.
- Kufunguka kwa barabara hivyo kuongeza mwingiliano wa watu
- Ujio wa Wakimbizi kutoka Burundi na DRC.



Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Julai –Septemba 2017 kitengo cha UKIMWI.

- Kutoa huduma za ushauri na upimaji zinazoanzishwa nakuchochewa na watoa huduma wa afya katika wilaya na halmashauri zote (Provider Initiated Testing and Counseling) (PITC)
- Kutoa Huduma ya Tiba, matunzo na ufuatiliaji kwa wagonjwa wenye maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (Care and Treatment)
- Kutoa Huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, (Prevention of HIV from Mother to Child Transmission) (PMTCT)
- Utoajiwa huduma kwa wagonjwa majumbani hasa wale wenye magonjwa ya kusendeka (Home Based Care) (HBC)
- Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma za Afya kuhusu huduma stahili kwa watu walio na maambukizi ya VVU/UKIMWI kutoka halmashauri zote (Capacity Building)
- Kutoa huduma shirikishi za kifua kikuu na UKIMWI (TB/HIV)
- Kutoa huduma kwa wagonjwa wa magonjwa ya ngono na via vya uzazi (STI/RTI)
- Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na maambukizi ya VVU na huduma zinazotolewa kwa mtu anayegunduliwa kuwa na maambukizi ya VVU na mahali huduma hizo zinapopatikana.

F: HALI YA UGONJWA WA MALARIA

Takwimu kutoka katika vituo vya afya zinabainisha Kiwango cha ugonjwa wa Malaria kimepanda kutoka 23% mwaka 2015 hadi 38% mwaka 2016. Mkoa umefanikiwa kutekeleza mpango wa Taifa wa Kusambaza vyandarua vya bure vyenye dawa kwa kila kituo cha kutolea huduma kwa ajili ya mama wajawazito waokwenda kituoni kwa hudhulio la kwanza na watoto wanaofikisha umri wa miezi 9 kwa chanjo ya Surua/Rubella ambapo jumla ya vyandarua 80,280 vimegawiwa.

Kipindi ambacho tunapokea wagonjwa wengi wa malaria ni miezi ya Novemba hadi juni kama inavyojionyesha katika grafu hapa chini.



Vipimo kwa ajili ya ugonjwa wa malaria: Huduma za upimaji wa malaria umeboreshwa ambapo hivi sasa vituo vyote 267 vinatoa huduma ya upimaji wa malaria kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mRDT.

Shugulli zilizofanyika kwa kipindi cha Julai-Septemba 2017 ni kama ifuatavyo

1. Mafunzo ya utumiaji orodha hakiki (MSDQA) kwenye kitita cha huduma za Maralia ambayo yalikusishwa Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma.
2. Mafunzo ya ubora na uhakiki katika Kipimo cha malaria kwa wafamasia, wataalam wa maabara na waratibu wa malaria.
3. Usambazaji wa vyandarua kwenye vituo 220 vya kutolea huduma vya Serikali. Jumla ya vyandarua 80,280 vimesambazwa.

G: HUDUMA ZA KIFUA KIKUU NA UKOMA

Huduma za kifua kikuu na Ukoma hutolewa katika baadhi ya vituo vya Tiba. Kumekuwa na kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wanaoibuliwa kutoka 952 mwaka 2015 hadi 1,133 mwaka 2016, ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 19. Vituo vinavyopima kifua kikuu vimeongezeka kutoka 24 mwaka 2005 hadi kufikia 33 Mwaka 2016. Kiwango cha uponaji wa wagonjwa kimefikia asilimia 89

Wagonjwa wote wa Kifua kikuu wanapata huduma ya kupimwa VVU na waongundulika kuwa na magonjwa yote mawili ni asimilia 20 na hivyo wanapata matibabu ipasavyo. Dawa za kifua kikuu zimeendelea kutolewa bure yaani bila malipo kwa wagonjwa wote na idadi ya vidonge imeboreshwa kutoka vidonge 11 hadi 4 hivi sasa hivyo kuimarisha tiba ya ugonjwa huu na pia wagonjwa na jamii imeimarika na mgonjwa kupewa fursa ya kuchagua msimamizi wake katika umezaji wa dawa.

Shughuli za Kifua kikuu na Ukoma zilizofanyika kwa kipindi cha Julai-Septemba 2017

- Kutoa Elimu elekezi katika Halmashauri zinazotekeleza Mpango wa Uibuaji wa kasi wa Wagonjwa wa Kifua kikuu: Uvinza, Kakonko na Kigoma/Ujiji Manispaa.
- Kufanya Mkutano wa kwanza wa Mwaka wa kutathmini Mpango wa uibuaji wa wagonjwa wa Kifua kikuu katika Halmashauri zinazotekeleza Mpango: Uvinza, Kakonko na Kigoma/Ujiji Manispaa.
- Usimamizi shirikishi kwa wahudumu wa afya ngazi ya Jamii na Waambisha makohozi
- Usimamizi shirikishi kwa Waratibu wa TB na Ukoma kuangalia ubora wa takwimu za Kifua kikuu na Ukoma. Uvinza, Kasulu Tc na Kigoma/Ujiji Manispaa.
- Usimamizi shirikishi kwa wanao wahudumia wagonjwa wa Kifua kikuu sugu kambi ya wakimbizi Nduta.
- Kutoa elimu ya Kifua kikuu na kuwapima wahisiwa wa Kifua kikuu katika Halmashauri 4; Kakonko, Uvinza, Buhigwe na Kasulu TC.
- Usimamizi shirikishi wa huduma za Kifua kikuu na Ukoma na maambukizi ya VVU katika Halmashauri za Kigoma

- Ufuatiliji wa wahisiwa wa Kifua kikuu toka kwa Mgonjwa wa Kifua kikuu Sugu huko Uvinza DC - Mgambazi.
- Usimamizi shirikishi na elimu elekezi kwa Halmashauri zenye wagonjwa wa kifua kikuu sugu;Uvinza , Kibonda na Kasulu TC

H: HALI YA UPATIKANAJI WA DAWA MUHIMU KATIKA MKOA

Hali ya upatikanaji wa dawa kwa mwaka 2016/2017 kwa kutumia kigezo cha *Tracer medicine 30* , Halmashauri za Kasulu TC, Manispaa ya Kigoma-Ujiji na Uvinza DC zilifikia lengo la 80% na zaidi na Halmashauri zingine zilifikia kiwango cha 55-74% cha upatikanaji wa dawa na hivyo kufanya hali ya upatikanaji wa dawa Kimkoa kuwa 74%.

Aidha, hali ya kiwango cha fedha kwa ajili ya dawa, vifaa tiba, vifaa na vitendanishi vya Maabara zilizotengwa na Serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa imeongezeka kutoka kiasi cha Shilingi 2,588,834,200 kwa mwaka 2016/2017 hadi kufikia kiasi cha Shilingi 4,183,330,782.04 kwa mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 62.

2016/2017			
HOSPITAL		PHC	
Kasulu	257,505,100.00	Kasulu	348,653,000.00
Kibondo	169,886,600.00	Kibondo	213,986,000.00
Baptist	69,809,500.00	Kigoma DC	173,237,000.00
MRRH	247,341,000.00	Kgm/UJ MC	165,342,000.00
Kabanga	123,670,000.00	Uvinza DC	314,136,000.00
		Buhigwe DC	208,263,000.00
		Kakonko DC	137,199,000.00
		Kasulu TC	159,806,000.00
TOTAL	868,212,200.00		1,720,622,000.00

2017/2018			
HOSPITAL		PHC	
Kasulu	306,363,803.51	Kasulu DC	660,500,000.00
Kibondo	202,120,716.53	Kibondo	425,000,000.00
Baptist	83,055,092	Kigoma DC	328,200,000.00
MRRH	247,000,000.00	Kgm/UJ MC	334,400,000.00
Kabanga	153,670,000.00	Uvinza DC	594,600,000.00
		Buhigwe DC	380,290,820.00
		Kakonko DC	145,430,358.00
		Kasulu TC	322,699,992.00
TOTAL	992,209,612.04		3,191,121,170.00

I: MAGONJWA 10 YANAYOATHIRI ZAIDI JAMII YA WANA KIGOMA

Magonjwa 10 yanayoongoza kwa kila wilaya ni kama ifuatavyo:-

Malaria, Magonjwa ya njia ya hewa, Kuharisha, Magonjwa ya Minyoo, Nimonia, Magonjwa ya Ngozi, Upungufu wa damu, UTI, ajali na magonjwa ya macho

J: RUFEE NA HUDUMA HUSIKA

Mkoa wa Kigoma una upungufu wa kuwezesha kusafirisha wagonjwa hadi kufika kituo cha huduma ambako anaweza kupata huduma bora na kwa uharaka.

1. Changamoto za upatikanaji wa usafiri kutoka kwenye jamii kwenda kituo cha huduma, na kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine chenye huduma inayotakiwa.
2. Katika vituo vya afya na hospitali za umma kuna uhitaji wa magari ya wagonjwa kwa kiwango cha chini matano (5) kwa ajili ya kuboresha huduma za rufaa mkoa wa Kigoma

Mahitaji wa magari ya wagonjwa kwa vituo vya huduma vya serikali

Halmashauri	Hosp ya Mkoa	Hospitali ya wilaya	Vituo vya afya	Zahanati	Mahitaji	Pungufu
Kakonko DC	NA	0	4	0	3	0
Kibondo DC	NA	1	3	0	4	0
Kasulu DC	NA	0	3	0	5	2
Kasulu TC	NA	1	0	1	3	1
Buhigwe DC	NA	0	4	0	2	0
Uvinza DC	NA	0	3	0	5	2
Kigoma DC	NA	0	2	0	2	0
Kigoma/Ujiji MC	1	1	2	0	3	0
Total	1	3	21	1	27	5

K: BAADHI YA MAFANIKIO YA JUMLA SEKTA YA AFYA KIMKOA

- Kuongezeka kwa kiwango cha akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma,
- kuongezeka kwa wakinamama wanaotumia njia za uzazi wa mpango
- Kuongezeka kwa kiwango cha watoto wanaopewa chanjo

-Kuongezeka kwa vituo vinavyotoa huduma za dharura na upasuaji,

Vituo vya afya 17 kati ya 32 vimewezeshwa kuanza utoaji wa huduma za dharura za upasuaji hasa kwa wazazi na kingine kimoja kinatarajiwa kianze kazi hivi karibuni.

- Vituo vyote vya serikali vimefungiwa umeme wa jua na au umeme wa TANESCO zikiwemo nyumba za watumishi kupitia vyanzo mbalimbali.
- Mkoa wa Kigoma tumeongeza vituo vya tiba na matunzo na ufuatiliaji (CTC) kutoka 33 hadi 67 ambavyo vimesogeza huduma ya kutoa dawa za kufubaza virusi vya ukimwi kwa kila mtu anayeishi na virusi vya ukimwi.

- Watoa huduma wa Afya katika vituo vya kutolea huduma wameendelea kujengewa uwezo kwa kufundishwa mambo mbalimbali ili waweze kutoa huduma zilizoboreka vituoni katika Nyanja mbalimbali

L: CHANGAMOTO

- i. Uhaba mkubwa sana wa watumishi wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa asilimia 68%
- ii. Miundombinu ya majengo ya zahanati na vituo vya afya inahitaji ukarabati ili kukidhi ongezeko la idadi ya watu
- iii. Upungufu wa baadhi ya vifaa muhimu vya tiba kwenye vituo vya huduma na ukosefu wa wataalamu husika
- iv. Kukosekana kwa Madaktari bingwa na wataalamu wengine katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na wilaya kunasababisha wagonjwa wengi kupewa rufaa ambazo zingeliweza kushughulikiwa hapa mkoani.
- v. Magonjwa ya milipuko yameendelea kuathiri hasa wilaya ya Kigoma Mjini ambayo ilikumbwa na tatizo la ugonjwa wa Kipindupindu

Katika kukabiliana na changamoto hizi Mkoa unaongeza idadi ya watumishi kwa kuajiri, imendaa mpango mkakati wa kukabiliana na Ukimwi na Magonjwa ya milipuko na utaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya afya

M: MIPANGO ILIYOPO NA MATARAJIO

Kuendelea kutafuta na kuajiri watumishi wenye ujuzi wakiwamo Madaktari bingwa

- Kuimarisha upatikanaji wa Vivutio kwa watumishi wa afya mkoani mfano nyumba za watumishi na vivutio vinginevyo.
- Kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya rufaa ya Mkoa.
Wakala wa Nishati Vijijini ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Nishati na Madini ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania, ikiwa na jukumu kuu la kuhakikisha upatikanaji thabiti wa nishati ya kisasa katika maeneo yote ya vijijini nchini Tanzania. Wakala wa Nishati Vijijini ilianza kazi rasmi mnamo Octoba 2007 baada ya serikali kuanza rasmi utekelezaji wa sera yake ya nishati bora na ya kisasa. Hapo nyuma Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilikuwa na mfuko wa umeme vijijini na kwa kuanzia Shirika lilifanikiwa kupeleka nishati ya umeme kwenye makao ya Wilaya mbalimbali. Serikali ilibaini kuwa kasi ya utekelezaji wa kazi hiyo ni vyema kutenganisha majukumu na kuundwa kwa Wakala wa Nishati vijijini ili kuweka nia thabiti ya kupeleka maendeleo katika maeneo ya vijijini. Wakala wa Nishati Vijijini iliundwa chini ya sharia Na. 8 ya 2005 kwa kupewa jukumu la kuinua maisha na kipato cha watanzania zaidi ya asilimia 85 waishio vijijini kwa kuwapelekea nishati ya kisasa kwa kushirikiana na taasisi za serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi.

3.0 KAZI KUU ZA WAKALA WA NISHATI VIJIJINI (REA).

Serikali kwa kushirikiana sekta binafsi, taasisi zisizo za serikali, taasisi za kijamii imenuia kuhakikisha pesa zinapatikana ili kufikisha nishati bora vijijini kwa kupitia wakala wa nishati vijijini ambae majukumu yake makuu yakiwa ni;

- kufanikisha usambazaji wa nishati bora ili kufanikisha maendeleo vijijini,
- kukuza na kuendeleza uzalishaji na matumizi ya nishati vijijini na pia kufanikisha upatikanaji wa miradi ya nishati ya maendeleo vijijini.
- Kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuibua miradi ya umeme vijijini

4.0 MAENDELEO YA MIRADI YA UMEME VIJIJINI KATIKA MKOA WA KIGOMA

4.1: Awamu ya Kwanza

Mnamo mwaka 2010 serikali ilikamilisha ujenzi wa vituo vya kufua umeme katika wilaya mbili za Kasulu na Kibondo na kupitia wakala wa nishati vijijini (REA) ilifadhili miradi ya usambazaji wa umeme katika makao makuu ya wilaya za Kasulu na Kibondo ambayo ilikamilika mnamo Octoba 2011.

4.2: Awamu ya Pili

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) iliendeleza mpango wa usambazaji wa umeme kwa awamu ya pili ambapo kwa mkoa wa Kigoma ulinufaika kama ifuatavyo; Wilaya mpya za Uvinza, Buhigwe, Kakonko pamoja na wilaya za Kigoma vijijini, Manispaa ya Kigoma/Ujiji kijiji, Kasulu na Kibondo zilinufaika na mradi huu. Jumla ya vijiji 19 katika wilaya ya Kigoma vijijini, vijiji 25 katika wilaya ya Uvinza, vijiji 22 katika wilaya ya Buhigwe, vijiji 24 katika wilaya ya Kasulu, vijiji vitano katika wilaya ya Kibondo, vijiji 13 katika wilaya ya Kakonko na kijiji kimoja katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji vilinufaika na nishati ya umeme kupitia mpango huu wa awamu ya pili ambapo jumla ya kilometa 479.91 za msongo wa kilovolti 11 na 33 (MV Line) zilikamilishwa na kilometa 364.04 za msongo wa volti 400 zilikamilika na kuwafikia zaidi ya wateja 7,200

4.3: Awamu ya Tatu

Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), inatarajia kuanza utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Awamu ya Tatu wa kusambaza nishati vijijini utakaojumuisha vijiji 144 katika wilaya zote za mkoa wa Kigoma kama ifuatavyo; vijiji 19 vya Wilaya ya Kigoma Vijijini, vijiji 12 vya Wilaya ya Uvinza, vijiji 26 vya Wilaya ya Buhigwe, vijiji 19 vya Wilaya ya Kasulu, vijiji 40 vya Wilaya ya Kibondo na vijiji 30 vya Wilaya ya Kakonko vitanufaika na mpango huu wa usambazaji wa umeme vijijini wa awamu ya tatu ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka huu wa fedha 2016/17 hadi 2020/21.

5. CHANGAMOTO

- Uwepo wa vitendo vya ulaghai wa fedha kwa wananchi unaofanywa na baadhi ya wananchi wasio waaminifu kwa kudanganya wananchi kwamba watapata huduma hii kwa gharama fulani tofauti na inayolipwa TANESCO.
- Kuongezeka kwa vishoka punde miradi inapokamilika ambao wengi huwa na vibarua waliokuwa wameajiriwa na wakandarasi wa miradi hiyo ambao hufanya vitendo vya ulaghai kwa wananchi wakidhaniwa bado ni wafanyakazi wa mkandarasi.

- Ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi kutokana na uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi juu ya malipo ya fidia pale inapobidi kuruhusu ardhi kwaajili ya kupitisha miundombinu.
- Uharibifu wa miundombinu unaofanywa na wananchi kwa kuchoma nguzo kipindi cha kiangazi.

TENDER NO : 10

Lot 2: Kakonko & Kibondo Districts

S/N	REGION	DISTRICT	WARD	VILLAGE
1	Kigoma	Kakonko	Gwamumpu	Gwanumpu
2	Kigoma	Kakonko	Gwamumpu	Bukiripo
3	Kigoma	Kakonko	Gwarama	Kabare
4	Kigoma	Kakonko	Gwarama	Nyakiobe
5	Kigoma	Kakonko	Gwamumpu	Rusenga
6	Kigoma	Kakonko	Kasanda	Nkuba
7	Kigoma	Kakonko	Kasanda	Kewe
8	Kigoma	Kakonko	Kasanda	Juhudi
9	Kigoma	Kakonko	Kasuga	Njoomulole
10	Kigoma	Kakonko	Kanyonza	Kihomoka
11	Kigoma	Kakonko	Kanyonza to Nyakanazi	Kanyonza to Nyakanazi
12	Kigoma	Kakonko	Mugunzu	Kiniha
13	Kigoma	Kakonko	Muhange	Luhulu
14	Kigoma	Kakonko	Muhange	Muhange Juu
15	Kigoma	Kakonko	Nyantukuza	Nyanzige
16	Kigoma	Kakonko	Rugenge	Kikulazo
17	Kigoma	Kakonko	Kasanda	Chilambo
18	Kigoma	Kakonko	Kasuga	Kasuga
19	Kigoma	Kakonko	Rugenge	Kiga
20	Kigoma	Kakonko	Mugunzu	Mugunzu
21	Kigoma	Kakonko	Katanga	Irabiro
22	Kigoma	Kakonko	Kasuga	Kinonko
23	Kigoma	Kakonko	Katanga	Katanga
24	Kigoma	Kakonko	Kasuga	Nyakayenzi
25	Kigoma	Kakonko	Rugenge	Kasongati

26	Kigoma	Kakonko	Mugunzu	Kiduduye
27	Kigoma	Kakonko	Mugunzu	Nyagwijima
28	Kigoma	Kakonko	Muhange	Muhange
29	Kigoma	Kakonko	Muhange	Rubale
30	Kigoma	Kakonko	Muhange	Gwarama
31	Kigoma	Kibondo	Bunyambo	Bavunja
32	Kigoma	Kibondo	Rugongwe	Lukaya
33	Kigoma	Kibondo	Lusohoko	Maloregwa
34	Kigoma	Kibondo	Kizazi	Kasana
35	Kigoma	Kibondo	Kumsenga	Kukinama
36	Kigoma	Kibondo	Kagezi	Mlange
37	Kigoma	Kibondo	Kagezi	Mikonko
38	Kigoma	Kibondo	Mukabuye	Kageyo
39	Kigoma	Kibondo	Mukabuye	Nyakilenda
40	Kigoma	Kibondo	Busunzu	Nyamilembi
41	Kigoma	Kibondo	Busunzu	Nyarulanga
42	Kigoma	Kibondo	Misezera	Kumkugwa
43	Kigoma	Kibondo	Kitahana	Rugunga
44	Kigoma	Kibondo	Kitahana	Kibingo
45	Kigoma	Kibondo	Bunyambo	Bunyambo
46	Kigoma	Kibondo	Bunyambo	Minyinya
47	Kigoma	Kibondo	Itaba	Buyezi
48	Kigoma	Kibondo	Bunyambo	Samvura
49	Kigoma	Kibondo	Busagara	Kasaka
50	Kigoma	Kibondo	Itaba	Mukabuye
51	Kigoma	Kibondo	Itaba	Kigogo
52	Kigoma	Kibondo	Mabamba	Nyange
53	Kigoma	Kibondo	Busagara	Nyaruyoba
54	Kigoma	Kibondo	Busagara	Kumkuyu
55	Kigoma	Kibondo	Kizazi	Nyabitaka
56	Kigoma	Kibondo	Mabamba	Mabamba
57	Kigoma	Kibondo	Mabamba	Mukarazi
58	Kigoma	Kibondo	Rugongwe	Kigaga
59	Kigoma	Kibondo	Kizazi	Nyarugusu
60	Kigoma	Kibondo	Rugongwe	Kichananga
61	Kigoma	Kibondo	Kizazi	Kumshwabure
62	Kigoma	Kibondo	Mabamba	Nyakasanda
63	Kigoma	Kibondo	Kumsenga	Kagezi

64	Kigoma	Kibondo	Busunzu	Kisongwe
65	Kigoma	Kibondo	Kumsenga	Kumsenga
66	Kigoma	Kibondo	Busunzu	Busunzu
67	Kigoma	Kibondo	Kumsenga	Kibuye
68	Kigoma	Kibondo	Rugongwe	Magarama
69	Kigoma	Kibondo	Rugongwe	Kigina
70	Kigoma	Kibondo	Busunzu	Nyakwi

Lot 3: Kasulu, Kibondo, Kigoma & Uvinza

S/N	REGION	DISTRICT	WARD	VILLAGE
1	Kigoma	Buhigwe	Buhigwe	Mulera
2	Kigoma	Buhigwe	Muyama	Kalege
3	Kigoma	Buhigwe	Nyamugali	Bulimanyi
4	Kigoma	Buhigwe	Munanila	Nyakimwe
5	Kigoma	Buhigwe	Munanila	Mkatanga
6	Kigoma	Buhigwe	Rusaba	Rusaba
7	Kigoma	Buhigwe	Muhinda	Nyaruboza
8	Kigoma	Buhigwe	Biharu	Kigege
9	Kigoma	Buhigwe	Kibande	Bulimanyi
10	Kigoma	Buhigwe	Muhinda	Muhinda
11	Kigoma	Buhigwe	Kajana	Kajana
12	Kigoma	Buhigwe	Kibande	Bweranka
13	Kigoma	Buhigwe	Kibande	Kibande
14	Kigoma	Buhigwe	Munzeze	Kigogwe
15	Kigoma	Buhigwe	Mwayaya	Kibwigwa
16	Kigoma	Buhigwe	Rusaba	Kinazi
17	Kigoma	Buhigwe	Munanila	Kitambuka
18	Kigoma	Buhigwe	Munzeze	Munzeze
19	Kigoma	Buhigwe	Janda	Bukuba
20	Kigoma	Buhigwe	Buhigwe	Nyankoronko
21	Kigoma	Buhigwe	Kilelema	Migongo
22	Kigoma	Buhigwe	Muhinda	Mubanga
23	Kigoma	Buhigwe	Mugera	Mugera
24	Kigoma	Buhigwe	Janda	Kihungu
25	Kigoma	Buhigwe	Mugera	Katundu
26	Kigoma	Buhigwe	Kibwigwa to Buhigwe	Kibwigwa to Buhigwe

27	Kigoma	Kasulu	Ruhita	Ruhita
28	Kigoma	Kasulu	Nyamnyusi	Nyamnyusi
29	Kigoma	Kasulu	Kigondo	Kigondo
30	Kigoma	Kasulu	Basanza	Basanza
31	Kigoma	Kasulu	Buhoro	Shunga(Mtabila Refugees Camp)
32	Kigoma	Kasulu	Nyumbigwa	Nyumbigwa
33	Kigoma	Kasulu	Muhunga	Muhunga
34	Kigoma	Kasulu	Nyakitonto	Mugombe
35	Kigoma	Kasulu	Murufiti	Murufiti
36	Kigoma	Kasulu	Bugaga	Bugaga
37	Kigoma	Kasulu	Rusesa	Zeze
38	Kigoma	Kasulu	Buhoro	Shunga
39	Kigoma	Kasulu	Nyachenda	Nyachenda
40	Kigoma	Kasulu	Nyumbigwa	Kasyenene
41	Kigoma	Kasulu	Bugaga	Nkunduis
42	Kigoma	Kasulu	Kwaga	Kalela
43	Kigoma	Kasulu	Kwaga	Kwaga
44	Kigoma	Kasulu	Nyachenda	Mwali
45	Kigoma	Kasulu	Kigembe	Kigembe
46	Kigoma	Kigoma	Businde	Businde
47	Kigoma	Kigoma	Mahembe	Nkungwe
48	Kigoma	Kigoma	Mkigo	Mukigo
49	Kigoma	Kigoma	Kagongo	Mgaraganza
50	Kigoma	Kigoma	Bitale	Kizenga
51	Kigoma	Kigoma	Mkongoro	Chankele
52	Kigoma	Kigoma	Bitale	Bubango
53	Kigoma	Kigoma	Mkongoro	Nyamhoza
54	Kigoma	Kigoma	Mwamgongo	Mwamgongo
55	Kigoma	Kigoma	Kagongo	Mtanga
56	Kigoma	Kigoma	Matendo	Pamila
57	Kigoma	Kigoma	Matendo	Matendo
58	Kigoma	Kigoma	Kagunga	Kagunga
59	Kigoma	Kigoma	Kagongo	Kagongo
60	Kigoma	Kigoma	Mwamgongo	Bugamba
61	Kigoma	Kigoma	Kagunga	Zashe
62	Kigoma	Kigoma	Mwamgongo	Kiziba
63	Kigoma	Uvinza	Sunuka	Rulinga
64	Kigoma	Uvinza	Sunuka	Kanywangili

65	Kigoma	Uvinza	Mwakizega	Kabeba
66	Kigoma	Uvinza	Mwakizega	Katete
67	Kigoma	Uvinza	Ilagala	Sambala
68	Kigoma	Uvinza	Ilagala	Kajeje
69	Kigoma	Uvinza	Simbo	Kiseke
70	Kigoma	Uvinza	Kandaga	Kandaga
71	Kigoma	Uvinza	Kazuramimba	Nyanganga
72	Kigoma	Uvinza	Ilagala	Mwakizega
73	Kigoma	Uvinza	Uvinza	Chakuru
74	Kigoma	Uvinza	Mganza	Malagarasi

Nawasilisha,

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA)-MKOA WA KIGOMA

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2016/2017 NA MALENGO YA 2017/2018

A. MAMBO YALIYOFANYIKA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17

- **MALENGO YA MAKUSANYO**

a) Mkoa ulipangiwa kukusanya shilingi 13,290.00 Milioni ikiwa ni shilingi 11,670.80 milioni za Kodi za Ndani na shilingi 1,620.00milioni za Kodi za Forodha. Mkoa ulifanikiwa kuvuta malengo hayo kwa kukusanya shilingi 14,649.23 milion kati ya hizo Kodi za ndani shilingi 12,768.22 milioni na Kodi za Forodha shilingi 1,881.00 milion. Hiki ni kiwango cha utendaji cha asilimia 110.22.

b) Pia Mkoa ulipangiwa kukusanya shilingi 210.00 milioni za kodi ya Majengo (property Tax) na ulikusanya shilingi 327,35 milion, kiwango cha utendaji kazi kikiwa ni asilia 156.

Mafanikio hayo yanatokana na jitihada kubwa za wafanyakazi wa mamlaka pamoja na msaada mkubwa toka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na idara nyingine za serikali. Tunatoa shukruni za dhati kwa ushirikiano wenu na tunaomba uendelee mwaka wa fedha 2017/18

- **MIKAKATI YA UTENDAJI YA MWAKA 2016/17**

a) **KUPANUA WIGO WA KODI**

Hili tulilifanya kupitia usajili wa wanaostahili kulipa kodi, kusimamia ununuzi na utumiaji mashine za kieletroniki (EFDs), utoaji wa risiti kwa mauzo/manunuzi, ukadiriaji na ukusanyaji wa kodi majengo (property Tax).

b) **KUDHIBITI UKWEPAJI KODI**

Chini ya kakati huu tumefanya kaguzi thabiti kutambua Kodi iliyostahili kulipwa, tumesimamia vyema Kodi za Forodha kutokana na bidha

c) **KUKUSANYA MADENI SUGU**

Tulifanya oparetion maalumu ya kufuatilia wadaiwa sugu na kukusanya madeni yaliyokuwa yameshindikana kukusanywa. Kazi hii ilifanyika kwa msaada mkubwa toka kwa vyombo vya ulinzi na usalama waliokuwepo kwenye kikosi kazi maalumu

kwa kazi hii. Hapa tuliweza kukusanya kiasi cha shilingi 131,750,000,00. Tunatoa shukrani za dhati kwa ushirikiano wao mkubwa.

d) KUWATOZA ADHABU WAKWEPA KODI NA WACHELEWAJI KULIPA

Kupitia sheria ya usimamizi wa kodi ya 2015, wachelewaji kulipa na wakwepaji wa maeendelea kutozwa adhabu zinazostahiki ili kudhibit Mapato ya serikali.

e) KUTOA ELIMU KWA WALIPA KODNA WADAU WOTE

Tuliendelea kutoa elimu kwa wadau wote wa kodi ili kuhanasisha uhiari wa ilipaji Kodi. Hii, kwa mfano, imechangia sana kuweza kukusanyakiasi kikubwa cha kodi za majego kuliko kilichowahi kufikiwa hapo nyuma.

f) KUSIMAMIA UTENDAJI NA UADILIFU WA WAFANYAKAZI WETU

Kama tunavyofahamu utendaji wenye waledi na uadilifu ni dhana madhubuti katika kuboresha ufanisi wa kazi. Mamlaka hapa Mkoani inatilia mkazo mabo haya na bila shaka ufanisi umeongezeka kiasi kikubwa kwenye ofisi zetu.

B) MAMBO YATAKAYOFANYIKA MWAKA HUUWA FEDHA 2017/18

• **MALENGO YA MAKUSANYO**

Mwaka wa fedha 2017/18 Mkoa umepangiwa kukusanya shilingi 18,098.76 milioni kati ya hizo milioni 16075.76 zikiwa Kodi za ndani na milioni 2.023.00 kodi za Forodha.

• **MIKAKATI YA MWAKA**

Katia mwaka wa fedha 2017/18 tutaendelea kutekeleza mikakati-msingi ya usimamizi wa Kodi zilizo chini ya Mamlaka, kama tulivyotekeleza mwaka 2016/17.

Hata hivyo kutokana na mabadiliko mbalimbali yaliyoletwa na sheria ya Fedha ya Mwaka 2017, Mamlaka itakuwa na mikakati mingine zaidi na kusesitiza kwenye baadhi itakayoonekana kuhitaji msisitizo mkubwa:

A) KUPANUA WIGO WA KODI

- i. Tutawatambua, kuwasajili nakuwatoza Kodi wafanyabiashara walio katika sekta isiyo rasmi.(Information sector)
- ii. Tutatambua na kutoza majengo yote kwenye Halmashauri zilizoongezwa kwenye wigo wa tozo ya kodi ya Majengo.
- iii. Tutaanza kusimamia kwa kutambua na kutoza kodi za mabango,
- iv. Tutafanya doria kubaini wafanya biashara wasotoa stakabadhi za mauzo yao na kuaadhibu kwa mujibu wa sheria na

- v. Tutafanya usajiri wa takwimu zetu(data clean-up)kwa kuwafuta wasiostahili kuwepo kwenye jalada letu na kuingiza waliokuwa nje ya jalada,
- vi. Tutasimamia utozaji wa kodi kwenye michezo ya kubahatisha kama sheria ilivyobadilika.(Gaming Tax)

B) KUSIMAMIA UNUNUZI NA MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI(EFDs)

- i. Tutakagua ili kuhakikisha kila anayestahili kununua mashine hizo ananunua,vinginevyo anatozwa adhabu zinazostahili kisheria,
- ii. Tutafanya doria za kushtukiza ili kubaini wasiotoa au kudai risiti hizo na kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria na
- iii. Tutaelimisha wadau wote ikiwemo taasisi na wafanyakazi wa serikali kudai risiti kwa kila manunuzi wanayofanya,

CHANGAMOTO TUNAZOKABILIANA NAZO

• UHABA MKUBWA WA RASILIMALI WATU

Ili kutekeleza majukumu tuliyopangiwa kikamilifu na kwa ufanisi unaotegemewa tunahitaji rasilimali watu. Mkoa kwa muda sasa umekumbwa na uhaba wa watumish mkubwa wa watumishi uliotokana na kuhama,kufariki na hata kuongezeka kwa uzito na ukubwa wa majukumu yetu. Mahitaji ya Mkoa ni wafanyakazi 122 na tuiopo ni 51. Tumeshatambua na kutaarifu Makao makuu yetu juu ya upungufu wa wafanyakazi 71

Uhaba huu unatuathiri kwenye doria za kwenye biashara ili kusimamia utoaji wa risiti za EFDs, doria za mipakani, na hata kwenye shughuli za kawaida za kaguzi na huduma za ofisini.

Uhaba huo umesababisha hata kushindwa kufungua ofisi zetu hata pale zinapohitajika. Mfano tuna wilaya mpya za Buhingwe Uvinza na Kakonko mbazo hazina sio ofisi tu bali hat awafanyakazi na tuna vituo vya Forodha kama Muhange, Kakunga, Mgambo, Kalya, Ujiji na Airport ambavyo havina watumishi kabisa

• UHABA WA BAADHI YA VIFAA KAZI

Mpaka wa Mkoa wetu ni mpana na unaweza kuvunjika (porous) bidhaaharamu (phohibited/restricted goods) na hata zinazotakiwa kulipwa kodi (dutiabale goods) na pia inawezekana kuingiza silaha toka nchi majirani zilizo katika vita mara kwa mara, n.k.

Kitego chetu cha Forodha kinahitaji Boti ya Doria iliyo nzima na itakayofanya doria Ziwani.

Pia tuna uhaba wa vifaa kazi zikiwemo kompyuta kwenye baadhi ya ofisi zetu.

Uhaba huu umeisharipotiwa ngazi za juu na tunaamini itafanyiwa kazi mapema.

- **USUGU WA BAADHI YA WALIPAKODI KUTOKUTII SHERIA ZA KODI**

Kuna baadhi ya wafanyabiashara, ambao hata waelimishwe vipi, bado watakuwa hawatoi stakabadhi za mauzo au risiti za za EFDs ili wafiche mauzo yao. Hawa tutaendelea kupambana nao kila tukiwabaini na kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria.

- **MTANDAO WA UNTERNET KUWA NA MWENDO MDOGO SANA AU KUTOPATIKANA KABISA**

Usajili, ukadiriaji na ulipaji wa kodi za Mamlaka vinatengemea mifumo ya kielektroniki na mtandao wa internet. Mwendo mdogo sa na hata ukosekanaji wa internet vimekuwa na athari hasi katika kutoa huduma na kukusanya kodi tunazosimamia.

Nawasilisha

T.J. Kaliza
MENEJA WA MKOA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
KIGOMA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)

TAARIFA YA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA BANDARI YA KIGOMA

1.0 UTANGULIZI

- 1.1 Bandari ya Kigoma ilijengwa kati ya mwaka 1922 na 1927 na Serikali ya kikoloni ya Ubelgiji na kuanza kazi mwaka 1927. Bandari ya Kigoma inasimamia pia bandari za Kasanga, Kipili, kabwe, Kagunga pamoja na bandari ndogo ndogo zilizopo nchini katika mwambao wa ziwa Tanganyika.

Bandari ya Kigoma ina uwezo wa kuhudumia shehena jumla ya tani 680,000 kwa mwaka kupitia magati matatu ya abiria, mizigo na mafuta. Pia ina uwezo wa kuhudumia abiria 300,000 kwa mwaka. Pamoja na uwezo huo Bandari ya Kigoma kwa miaka kadhaa sasa imekuwa ikihudumia shehena iliochini ya uwezo wa bandari huo kutokana na sababu mbalimbali ikiwepo uchakavu wa Miundombinu na vifaa vya kutoa huduma.

Kwa kutambua hayo Mamlaka ya Usimamizi ya Bandari imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za Uboreshaji wa huduma na kuwekeza katika miradi ya maendeleo kwa nia ya kujenga uwezo wa Bandari katika kuhudumia shehena.

Takwimu za zinaonyeshwa kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliopita shehena ya mizigo imeongezeka kwa wastani **asilimia 16.5**, kutoka **tani 67,704** mwaka 2012/2013 na kufikia tani **137,800** mwaka 2016/2017.

2.0 MIRADI YA MAENDELEO

2.1 Uboreshaji wa bandari ya Kigoma

- 2.1.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania katika mipango yake ya muda mrefu imepanga kufanya maboresho ya gati la mizigo na gati la abiria. Upembuzi yakinifu uliofanywa na kampuni ya M/s Royal Haskoning ya Uholanzi katika gati la mizigo umekwisha kamilika. Shirika la Misaada la Japan (JICA) limeonyesha nia ya kutoa msaada kufanikisha ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa gati la abiria na ghala la kuhifadha mizigo.

Kwa sasa JICA wanaendelea na ukusanyaji wa takwimu mbalimbali (survey) ili kupata hali halisi ya sasa. Ni matarajio ujenzi wa mradi huu utanza mwezi aprili 2019.

2.2 Ujenzi wa bandari kavu Katosho

- 2.2.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania imetwaa eneo la katosho lenye ukubwa wa takribani hekta 68 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu. Bandari kavu hii itasaidia kupunguza mlundikano wa mizigo bandarini kutokana na mipango iliyopo ya kuimarisha miundombinu ya reli na barabara, kupunguza mlundikano katika Bandari ya Dar es salaam na pia

kusogeza huduma karibu kwa nchi tunazozihudumia za Burundi, DR Congo na Rwanda, ikiwa nia ni kuwezesha mizigo kuchukuliwa hapa Kigoma badala ya Dar Es Salaam..

Ujenzi wa bandari kavu unakwenda sambamba na uendelezaji wa ukanda wa biashara (Kigoma Special Economic Zone).

Kazi ya ubomoaji wa nyumba za wananchi waliolipwa fidia katika eneo hilo ilifanyika mwishoni mwa mwezi Juni 2017. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa sasa ipo hatua za upimaji 'survey' na baada ya taratibu hizi kukamilika, eneo litazungushiwa uzio.

2.3 Ujenzi wa magati

2.3.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ina jukumu la kujenga na kuendeleza miundombinu ya bandari katika mwambao wa ziwa Tanganyika. Kwa kutambua hilo Mamlaka imejenga gati Kagunga na imepanga kujenga magati katika maeneo ya Kibirizi, Ujiji, Lagosa na Kalya (Sibwesa). Aidha, miradi hiyo ipo katika hatua mbali mbali kama ifuatavyo:-

- i) **Gati la Kagunga** – Mradi huu unahusisha ujenzi wa gati, jengo la kupumzikia abiria, ghala la kuhifadhia mizigo, vyoo, ofisi, na uzio. Mradi huu umefikia 99% kumalizika. Bado mapungufu machache ambayo Mkandarasi anatakiwa kuyarekebisha kabla ya kukabidhi kwa Mamlaka. Kwa sasa Mamlaka ipo katika hatua ya kufanya uthamini wa nyumba na mali katika eneo la ujenzi wa barabara itakayounganisha bandari hiyo.
- ii) **Gati la Sibwesa (Kalya)** – Kama ilivyo katika mradi wa ujenzi wa gati la Kagunga mradi huu pia unahusisha ujenzi wa gati, ofisi, jengo la kupumzikia abiria, jengo la kuhifadhia mizigo na uzio. Mradi huu umefikia 68% kumalizika. Mradi huu unaendelea na unatarajia kukamilika katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.
- iii) Ujenzi wa gati katika bandari ndogo za **Kibirizi, Ujiji** na **Lagosa** – Miradi hii ni mipya. Tayari zabuni zimeshatangazwa kwa ajili ya kuanza ujenzi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Miradi ya Ujiji na Lagosa ipo katika hatua za tathmini 'Evaluation stage', Utekelezaji wa mradi wa kibirizi utashirikisha Benki ya Dunia 'World Bank'.

2.4 Ujenzi wa Ofisi ya Utawala

Zabuni ya ujenzi wa jengo la ofisi ya Utawala ilikwishatangazwa na kwa sasa ipo katika hatua ya tathimini. Ujenzi huu unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka huu wa fedha 2017/2018.

2.5 Ununuzi wa Vitendea kazi (Vifaa)

- 2.5.1 Katika kuboresha huduma za bandari ya Kigoma Mamlaka imenunua krini mpya yenye uwezo wa kubeba tani 30 ambayo imekabidhiwa mwanzoni mwezi Septemba 2017. Krini hiyo ni ya kisasa ambayo inaweza kutumika kuhudumia mizigo ya kawaida na pia makasha. Kwa kuongeza mashine hii ni wazi sasa Bandari ya Kigoma itaongeza tija katika huduma ya upakiaji na upakuaji wa shehena gatini.

Katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 Mamlaka inatarajia kununua 'mobile crane' yenye uwezo wa kunyanyua tani 15 kwa ajili ya bandari ya Kigoma.

3.0 HITIMISHO

- 3.1 Mamlaka ya Bandari Tanzania itaendelea kuboresha miundo mbinu ya bandari pamoja na vifaa ili kutumia fursa ya kijiografia kwa lengo la kukidhi matakwa ya wateja wetu wa nchi zinazopakana na mkoa wa Kigoma, na pia kujenga uwezo kulingana na mahitaji yaliyombele yetu

Naomba kuwasilisha

Kaimu Mkuu wa Bandari

KIGOMA

**TAARIFA KUTOKA MSM-JINSI
ZINAVYOTEKELEZA AGIZO LA
SERIKALI LA KUFANIKISHA UCHUMI
WA VIWANDA;-**

- 1. KIGOMA DC**
- 2. KIBONDO DC**
- 3. BUHIGWE DC**
- 4. KIGOMA/UJIJI MC**
- 5. KASULU TC**
- 6. KASULU DC**
- 7. KAKONKO DC**
- 8. UVINZA DC**

**TAARIFA KUHUSU MSM ZINAVYOTEKELEZA MAAGIZO YA UCHUMI WA VIWANDA.
MAENEO YA UWEKEZAJI, MIRADI YA VIWANDA, HALI ILIVYO, CHANGAMOTO, MIKAKATI NA
MIPANGO YA BAADAYE KWA MKOA WA KIGOMA**

1. HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA

Jedwali Na. 1 : Takwimu za Miradi ya Viwanda (Vidogo/vya Kati/vikubwa)

Na.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotelekezwa (Wilaya/Kata)	Kiasi cha ajira zilizopo	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/Mazao	1	Kalinzi Manyovu.	97	Kiwanda kinafanya kazi.
2.	Mafuta	4	- Bitale.	12	Kiwanda Kinafanya kazi.
3.	Mazao ya Misitu	1	- Mahembe	5	Kiwanda kinafanya kazi.
4.	Vifaa vya Ujenzi		0	0	0
5.	Chumvi				
6.	Chokaa	1	- Simbo	80 zinazotarajiwa	Hakijaanza kufanya kazi, taratibu za kuweka umeme na gas unaendelea.
7.	Madini mengineyo	0	0	0	0
8.	Maji/Vinywaji	0	0	0	0
9.	Vinginevyo	0	0	0	0

Jedwali Na. 2 (Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Viwanda)

Na.	Jina la Mahali Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo/	Aina ya viwanda vinavyokusudiwa	Hali yake (Limepimwa/Halijapimwa)	Limetengwa taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/Mkakati
1.	Mahembe	Hekta 2.5	Viwanda vidogo	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TPKG/12/26/1106	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa
2.	Kidahwe	Hekta 2.9	Viwanda vidogo	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TP 12/KG/42/032014	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa

3.	Mahembe	Hekta 1.02	Viwanda vidogo	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TP 12/KG/41/03201 4	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa
4.	Mwandiga	Hekta 1.12	Viwanda vidogo	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TP 52/21/0501	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa
5.	Mwandiga	Hekta 11.97	Viwanda vya Kati	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TP 12/KGM/31/032 013	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa
6.	Mahembe	Hekta 2.188	Viwanda vya Kati	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TP 12/KGM/40/032 014	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa
7.	Mahembe	Hekta 1.84	Viwanda vya Kati	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa katika mchoro wa Mipangomiji Na. TP 12/KGM/41/032 014	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa

Mkakati wa Halmashauri katika kufikia Uchumi na Viwanda

- Kutangaza Fursa za Uwekezaji zilizopo katika Halmashauri kwa njia ya Web site ya Halmashuri na Radio (TBC Radio Joy)
- Kutenga maeneo kwa ajili ya Wawekezaji mfano maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda kuhakikisha yamepimwa.
- Kuboresha Miundombinu kwenye maeneo ya Uwekezaji mfano umeme, maji na barabara.
- Kuendelea kuhamasisha Wanachi/Wakulima kulima mazao ya chakula na biashara kwa wingi.

2. HALMASHAURI YA WILAYA KIBONDO

Jedwali Na. 1 : Takwimu za Miradi ya Viwanda (Vidogo/vya Kati/vikubwa)

Na.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotelekezwa (Wilaya/Kata)	Kiasi cha ajira zinazotarajiwa/zilizo po	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/ Mazao	5	Kata za Kumwambu(1), Kitahana(2), Murungu(1) na Biturana (1).	15@ kiwanda sawa jumla ya ajira 75	Kata ya Kumwambu (Nabuhima) na Biturana (Nengo) kipo hatua ya kuunganishiwa umeme,punde umeme utakapo unganushwa uzalishaji utaanza. Kata ya Murungu ujenzi umeshakamilika ikiwa ni pamoja kusimika mashine za kuchakata mazao.Kata ya Kitahana 1 jengo limezekwa na kingine 1 bado jengo halijaezekwa.
2.	Mafuta	-	-	-	-
3.	Mazao ya Misitu	5	Kata ya Kibondo Mjini	50	Vivanda hivi vinazalisha milango,madirisha, samani za nyumbani,ofisini na maeneo ya biashara.
4.	Vifaa vya Ujenzi	-	-	-	-
5.	Chumvi	-	-	-	-
6.	Chokaa	1	Kumwambu	15	Kinazalisha chokaa
7.	Madini mengineyo	-	-	-	-
8.	Maji/ Vinywaji	1	Kibondo Mjini	10	Kinazalisha maji ya kunywa
9.	Vinginevyo: • Vifungas hio	1	Kibondo Mjini	10	Hakijaanza kuzalisha
	• Mikate	1	Kibondo Mjini	10	Kinazalisha mikate
	• Mazao ya nyuki	3	Kibondo Mjini, Busunzu na Busagara	≥200 ikijumuisha walinaji wa asali	Vinazalisha asali na nta

Jedwali na. 2 (Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Viwanda)

Na.	Jina la Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo/ Aina ya viwanda vinyavyokusudiwa	Hali yake (Limepimwa/halijapimwa/ taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/Mkakati

1	Kibondo Industrial area	Eneo la ekari 30 ambapo viwanda vikubwa na vya kati vinatarajiwa kujengwa.	Upimaji wa awali umefanyika yaani <i>Demacation</i> umefanyika.	Halmashauri imeweka mpango wa kufanya upimaji utakaokuwa na mchoro wa mpango Miji wa maeneo hayo. Kazi hii itafanyika katika bajeti ya mwaka huu 2017/18
2	SIDO	Ekari 20 kwa ajili ya viwanda vidogo		

Mkakati wa Halmashauri katika kufikia Uchumi wa Viwanda

Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ni miongoni mwa Halmashauri 8 za mkoa wa Kigoma ambazo zinatekeleza mpango wa serikali wa kufikia uchumi wa viwanda.

Mkakati wa kufikia Uchumi wa Kati

Ili kuhakikisha kwamba Wilaya inafikia uchumi wa viwanda katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda, Wilaya imeweka mikakati ifuatayo:-

- Halmashauri imetenga eneo la jumla hekta 25,000 katika bonde la mto Malagarasi na Lumpungu kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa ya sukari na kujenga kiwanda cha kuzalisha sukari. Tayari mwekezaji wa Kampuni ya Green Field Plantations kutoka Mauritius ameonesha nia ya kuwekeza katika eneo hilo na tayari kampuni hiyo kwa kushirikiana na Wataalamu wa Halmashauri wameshapima eneo hilo na kulifanyia mpango wa matumizi bora ya ardhi. Aidha, maeneo yaliyopimwa yamepelekwa Kituo cha uwekezaji Tanzania(TIC) kwa ajili ya usajili.
- Halmashauri kupitia vikao vya Baraza la biashara imeendelea kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza katika sekta ya viwanda. Kutokana na hamasa hiyo; hadi sasa jumla ya wawekezaji 5 wamejenga viwanda vya kusindika mazao ya kilimo hasa nafaka yaani mahindi na muhogo. Kati ya viwanda hivyo, Kiwanda kimoja kilichopo katika kata ya Murungu kipo tayari kuanza kwa kuwa kimeshakamilisha ujenzi wa jengo; mashine na mitambo ya kuchakata muhogo imeshafungwa. Aidha, Viwanda 2 vilivyopo katika kata ya Biturana(Nengo) na Kumwambu(Nabuhima) vimeshakamilisha ujenzi wa miundombinu na kufunga mitambo(Mashine) za kuchakatia mazo ya muhogo na mahindi. Kilichokwamisha uzalishaji ni kutokukamilika kwa ufungaji wa umeme kwa sababu ya gharama kubwa inayohitajika kwa mwekezaji wakufunga umeme wa Nabuhima(Tsh. 13 milioni) na kukosekana kwa nguzo za umeme kwa mwekezaji wa katika eneo la Nengo pamoja na kuwa ameshalipia gharama zote za kufungwa umeme.
- Halmashauri imetenga eneo lenye jumla ya ekari 30 katika kata ya Biturana eneo la Nengo kwa ajili ya kujenga viwanda vya kati na vikubwa na jumla ya ekari 20 kwa ajili ya Shirika la viwanda Vidogovidogo(SIDO).
- Halmashauri imetenga eneo lenye jumla ya ekari 56 katika kijiji cha Mukarazi kwa ajili ya kujenga soko la mpakani kati ya Tanzania na Burundi. Lengo ni kuhakikisha kuwa bidhaa zitakazozalishwa katika viwanda hivyo zinapata soko la ndani na nje ya nchi. Tayari shirika la UNCDF limekubali kutoa kiasi dola za Kimarekani 100 ambazo ni zaidi ya Tsh. 200 milioni

kwa ajili ya kujenga Soko, vyoo na kufunga miundombinu ya maji. Ujenzi unatarajia kuanza muda wowote kuanzia Novemba 2017.

- Halmashauri katika mpango na bajeti yake ya mwaka 2017/18 imetenga jumla ya Tsh. 38,136,800/= kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kilimo bora cha alizeti katika vijiji 15 na kuwezesha ununuzi wa mashine ya kuongeza thamani ya zao la alizeti katika kata ya Kumwambu. Aidha, katika bajeti hiyo, Halmashauri imetenga kiasi cha Tsh.8,880,000 kwa ajili ya kuwezesha kikundi cha Kibondo Big Power kuzalisha vipando vya zao la muhogo na kuwezesha mafunzo kwa wakulima juu ya namna ya kuongeza thamani ya zao hilo.
- Halmashauri imepanga kutenga fedha za kutosha kila mwaka katika bajeti yake ili kuhakikisha kuwa inajenga na kuboresha mazingira bora yatakayo wavutia zaidi wawekezaji hasa sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya viwanda.

3. HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE

Jedwali Na. 1 : Takwimu za Miradi ya Viwanda (Vidogo/vya Kati/vikubwa)

Na.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotelekezwa (Wilaya/Kata)	Kiasi cha ajira zilizopo	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/ Mazao	3	-Buhigwe -Mwayaya -Muyama	6	Viwanda vinafanya kazi.
2.	Mafuta	5	- Kigege -Janda -Kinazi	22	Viwanda vinafanya kazi.
3.	Mazao ya Misitu	0	0	0	0
4.	Vifaa vya Ujenzi	0	0	0	0
5.	Chumvi	0	0	0	0
6.	Chokaa	0	0	0.	
7.	Madini mengineyo	0	0	0	0
8.	Maji/ Vinywaji	0	0	0	0
9.	Vinginevyo	0	0	0	0

Jedwali Na. 2 (Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Viwanda)

Na.	Jina la Mahali Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo/	Aina ya viwanda vinavyokusudiwa	Hali yake (Limepimwa/Halijapimwa)	Limetengwa taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/Mkakati
1.	Bwega-Buhigwe	Ekari 20	Viwanda vidogo	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa	Mkakati uliopo ni kuhakikisha eneo limepimwa

Mkakati wa Halmashauri katika kufikia Uchumi na Viwanda

- Kuanzisha kiwanda cha Banana Wine katika Eneo la Makao Makuu ya Wilaya Buhigwe
- Kutangaza Fursa za Uwekezaji zilizopo katika Halmashauri ya Buhigwe kwa njia ya Web site ya Halmashauri
- Kutenga maeneo kwa ajili ya Wawekezaji
- Kuboresha Miundombinu kwenye maeneo ya Uwekezaji mfano umeme, maji na barabara.
- Kuendelea kuhamasisha Wanachi/Wakulima kulima mazao ya migomba kwa wingi.

4. HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJJI

UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji ni miongoni mwa halmashauri nane za mkoa wa Kigoma. Manispaa ya Kigoma/Ujiji katika kutekeleza Azma ya uchumi wa viwanda imeandaa mazingira ya kushawishi uwekezaji wa viwanda katika maeneo mbalimbali ili kuleta tija katika uchumi wanchi.

Hali halisi ya mazingira ya sasa ili kuingia katika uchumi wa viwanda

Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji inaendelea kuweka mazingira ya uanzishwaji wa viwanda kama inavyoonekana hapo chini

Uwepo wa Umeme

Kwa sasa umeme unaotumika katika Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji ni wa uhakika na unatumika katika viwanda vidogo vilivyopo. Aidha kwa sasa kuna mradi wa kuongeza umeme (kampuni ya Solar wazi) ambao utaongeza umeme wa na hivyo kuwa na umeme wa uhakika ambao unavutia wawekezaji ili kuwekeza. Mradi huu unasimamiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ingawa upo ndani ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Uwepo wa Ardhi kwa ajili ya Uwekezaji

Manispaa ya Kigoma/Ujiji ilitenga eneo kwa ajili ya uwekezaji lenye ukubwa wa Hekta 15 eneo linaitwa Forodhani. Aidha mpaka sasa eneo hilo limepata mwekezaji kampuni kutoka China na sasa Manispaa ipo katika hatua za Mwisho za makubaliano ili uwekezaji wa kituo kikubwa cha biashara kuanza uwekezaji

Uwepo wa Vikao kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma

Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwa Ufadhili wa Mradi wa Local Investment Climate (LIC) imekuwa ikifanya majukwaa ya majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi ili kuonesha fursa zilizopo katika Wilaya ya Kigoma hususan Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Katika vikao hivyo hasa kikao cha Baraza la Biashara kumekuwa na majadiliano ambayo yanaleta tija kwa ajili ya Uwekezaji wa Viwanda. PIA Manispaa ya Kigoma/Ujiji kupitia tovuti ya Halmashauri imeendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Mkoa.

Zifuatayo ni Takwimu ya Viwanda vilivyopo katika eneo la Manispaa/Kigoma/Ujiji

Jedwali Na. 1 : Takwimu za Miradi ya Viwanda (Vidogo/vya Kati/vikubwa)

Na.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotelekezwa (Wilaya/Kata)	Kiasi cha ajira zilizopo	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/Mazao	7	MWANGA KASKAZINI, KIGOMA NA GUNGU	49	viwanda vinafanya kazi.
2.	Kukamua mafuta ya Mise na utengenezaji wa Sabuni	38	MWANGA KASKAZINI, KATUBUKA	246	viwanda vinafanya kazi.
3.	Mazao ya Mimitu	9	MWANGA KASKAZINI (SIDO) & KATUBUKA	36	Viwanda vinafanya kazi
4.	Vifaa vya Ujenzi	hakuna			
5.	Chumvi				
6.	Chokaa				
7.	Madini mengineyo	hakuna			
8.	Maji/Vinywaji	2	GUNGU, KIGOMA	15	Viwanda vinafanya kazi
9.	Vinginevyo	1	KIPAMPA	-	Kiwanda cha kuzalisha Juice kipo hatua ya ukamilishaji

Jedwali Na. 2 (Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Viwanda)

Na.	Jina la Mahali Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo/	Aina ya viwanda vinavyokusudiwa	Hali yake (Limepimwa/Halijapimwa)	Limetengwa taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/Mkakati
1.	Forodhani -Ujiji	Hekta 15	Bidhaa za Viwandani	Limepimwa	Ulipaji wa Fidia katika eneo hili bado	Ulipaji wa Fidia kwa wananchi

CHANGAMOTO

- Uwezo mdogo wa Halmashauri kulipa fidia katika maeneo ya uwekezaji
- Miundombinu isiyoridhisha kwa wawekezaji hasa uwezekano wa barabara za kufika Kigoma kutoka Dar es salaam na kutoka Mwanza.

Mkakati wa Halmashauri katika kufikia Uchumi na Viwanda

- Kuendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo Katika halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwa kutumia vikao vya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma, Makongamano mbalimbali ya Kibiashara na Kilimo na kutangazwa kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji
- Kuendelea kuwashawishi wawekezaji ili kuja kuwekeza kwa kutumia mabalozi wa Nchi mbalimbali kufika Manispaa ya Kigoma/Ujiji kuoneshwa fursa zilizopo ili kuleta wakezaji. (Tayari Balozi wa China, Indonesia na Japan wameshafika Manispaa ya Kigoma/Ujiji)

- Kuendelea kutoa Elimu kwa wamiliki wa viwanda vidogo ili kukuza mitaji yao na kuingia kwenye soko la ushindani ili kuanzisha viwanda vya kati (Kuwaunganisha wajasiriamali wadogo wnye viwanda vidogo na Mamlaka za TBS, TFDA na Bar Code).
- Kushawishi serikali kuwa na soko la Pamoja kati ya Manispaa ya Kigoma na Nchi jirani ya DRC ili kupanua soko la vifaa mbalimbali na hivyo kupanua fursa za uwekezaji wa viwanda Kigoma badala ya Kuleta bidhaa zilizo tayari kutoka Dar es Salaam na maeneo mengine).

5. HALMASHAURI YA MJI WA KASULU

Jedwali Na. 1 : Takwimu za Miradi ya Viwanda (Vidogo/vya Kati/vikubwa)

Na.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotelekezwa (Wilaya/Kata)	Kiasi cha ajira zilizopo	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/ Mazao	1	Kasulu Mjini (kata ya Murusi)	7	kiwanda vinafanya kazi
2.	Mafuta ya alizeti	1	Kasulu Mjini (Kata ya Murubona)	4	kiwanda vinafanya kazi
3.	Mazao ya Misitu (karakana za kutengeneza samani)	10	Kasulu mjini (Kata ya Murusi, Kumsenga, Mwilamvya)	75	Viwanda vinafanya kazi
4.	Vifaa vya Ujenzi		0	0	0
5.	Chumvi	0	0	0	0
6.	Chokaa	0	0	0	0
7.	Madini mengineyo	0	0	0	0
8.	Maji/ Vinywaji	0	0	0	0
9.	Vinginevyo	0	0	0	0
	Viwanda vya sabuni za maji	1	Kasulu Mjini	31	kiwanda vinafanya kazi
	Viwanda vya utengenezaji wa matofali ya ujenzi	1	Kasulu mjini (kata ya Murubona na Murusi)	25	Kiwanda vinafanya kazi
	Viwanda vya kutengeneza mikate	1	Kasulu Mjini (Kata ya Murubona)	10	kiwanda vinafanya kazi
	Viwanda vya kuchakata muhogo (unga wa muhogo)	1	Kasulu Mjini (Kata ya Murubona)	9	Kiwanda kinafanya kazi.

Zingatia:Viwanda hivyo ni vile vidogo vidogo.

Jedwali Na. 2 (Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Viwanda)

Na .	Jina la Mahali Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo/	Aina ya viwanda vinavyoku sudiwa	Hali yake (Limepimwa/ Halijapimwa)	Limetengwa taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/Mkakati
1.	Ruhita	Ekari 100	Viwanda vidogo	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa. Eneo bado halijalipiwa fidia.	Halmashauri imepanga kuandaa michoro kwa eneo hili katika mwaka wa fedha 2017/2018.
2	Ruhita	Ekari 20	SIDO	Halijapimwa	Eneo hili limetengwa. Eneo bado halijalipiwa fidia.	Halmashauri imepanga kuandaa michoro kwa eneo hili katika mwaka wa fedha 2017/2018.
2.	Jengo la wajasiliamali	Ekari 0.25	Viwanda vidogo	Limepimwa	Eneo limepimwa na linamilikiwa na Halmashauri ya Mji.	Halmashauri imetenga eneo na jengo lililopo kwa ajili ya kuwakusanya wajasiliamali. Tayari wanaosindika unga wa muhogo wanafanya uzalishaji kupitia jengo hilo. Lengo ni kuwakusanya wajasiliamali wenye viwanda vidogovidogo katika jengo hili ili kuendelea kuwafikia kwa urahisi na kuhakikisha wanakuza viwanda vyao.

Mkakati wa Halmashauri katika kufikia Uchumi na Viwanda

i. Utoaji wa mikopo kwa wanawake na vijana kwa lengo la kukuza viwanda Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imetoa jumla ya Tshs. 50,000,000.00 ikiwa ni sehemu ya fedha za asilimia 10 ya wanawake na vijana kusaidia shughuli za ujasiliamali. Katika mwaka huo wa fedha vikundi viwili vyenye uelekeo wa kukuza viwanda vilipewa mikopo kama ifuatavyo: -

N a	Jina la kikundi	Kiasi walichopewa	Matumizi ya fedha	Mradi wa kikundi
-----	-----------------	-------------------	-------------------	------------------

1	KIKUNDI CHA 'WOMEN OF INFORMAL SECTOR IN CROSS BOARDERS TRADING ASSOCIATION'	6,500,000.00	Kununua mashine ya kuchakata mihogo kwa ajili ya unga wa muhogo kutoka sido	Kuchakata mihogo kwa ajili ya unga wa muhogo
2	UMWANA WOMEN GROUP	4,000,000.00	Kuongeza mtaji – kununua vifaa kwa ajili ya kutengeneza sabuni.	Utengenezaji wa sabuni.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Mji wa Kasulu imetenga kiasi cha Tshs. 124,486,900.00 kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana. Halmashauri imepanga kutumia mikopo ya wanawake na vijana kuimarisha shughuli za viwanda katika mji. Shughuli zenye uelekeo wa viwanda zitapewa kipaumbele katika utoaji wa mikopo ili kuongeza shughuli za viwanda.

- ii. Ushawishi kwa wafanyabiashara kuanzisha viwanda katika Halmashauri ya Mji na kutangaza fursa kwa kupitia website 'www.kasulutc.go.tz'

Uongozi wa Halmashauri utaendelea kufanya mazungumzo na wafanyabiashara wa ndani na nje ya Halmashauri ili kuwashawishi wawekeze katika eneo la viwanda. Vile vile, kwa kutumia 'website' iliyopo, fursa zilizopo zitatangazwa.

Halmashauri inazo fursa nyingi zinazoweza kutumika kwa ajili ya uwekezaji baadhi ni kama ifuatavyo:-

- Uwepo wa matunda mengi – nanasi, parachichi, ndizi nk zinazoweza kuruhusu uanzishaji wa viwanda vya kusindika matunda
 - Uwepo wa mahindi mengi yanayoweza kuongezewa thamani kwa kusagwa na kuhifadhiwa katika vifungashio stahili kwa ajili ya kuuza unga
 - Uwepo wa mazao mengine kama vile maharage na mihogo ambayo yanaweza kuongezewa thamani.
 - Uwepo wa chemchem za maji ambazo zinaruhusu kuanzisha kiwanda cha maji ya kunywa.
 - Uwepo wa miti inayoruhusu uanzishaji wa viwanda vya kutengeneza samani.
- iii. Uandaaji wa michoro kwa ajili ya eneo lililotengwa kwa ajili ya viwanda la Ruhita.

6: HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

Jedwali Na.1: Takwimu za Miradi ya Viwanda (vidogo/ Vya kati/ Vikubwa)

Na.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotekelezwa (Wilaya/ Kata)	Kiasi cha ajira zilizopo	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/ Mazao	2	Nyamidaho		Mashine 3 zimemekwa na ujenzi wa kiwanda upo hatua ya mwishoni ya ukamilishaji
2.	Mafuta	-	-	-	-
3.	Mazao ya misitu	-	-	-	-
4.	Vifaa vya ujenzi	1	Zeze	104	Ujenzi wa karakana unaendelea
5.	Chumvi	-	-	-	-
6.	Chokaa	1	Makere		Kiwanda kinazalisha chokaa
7.	Madini mengineyo	-	-	-	-
8.	Maji/ vinywaji	-	-	-	-
9.	Asali	2	Kagerankanda, Rusesa	130	Kiwanda kinafanya kazi kinazalisha Asali, Nta, Mafuta, Mishumaa na Wine
10.	Sabuni za miche na maji	3	Zeze, Nyakitonto, Makere	80	Kiwanda kinazalisha sabuni za miche na maji
11.	vinginevyo	-	-	-	-

Jedwali Na.2: Maeneo Yaliyotengwa Kwaajili ya Viwandana Uwekezaji

Na	Jina la mahali Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo	Aina ya viwanda vinavyokusudiwa	Hali yake (limepimwa/ halijapimwa)	Limetengwa (taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/ mkakati
1.	Nyamidaho	Hekta 48,017	Kiwanda cha Sukari na kilimo cha miwa	Limepimwa	Halijalipiwa fidia	Kumpa eneo mwekezaji mwengine Kulilipia fida eneo Kuliwekea eneo miundombinu ya umeme, maji na barabara.
2.	Mugombe	Ekari 212.5 (hekta 85)	Viwanda vidogo, vya kati na vikubwa	Halijapimwa	Hakuna fidia	Kulipima eneo "master plan" Kuliwekea miundombinu ya

		SIDO LIC	Ekari 50 Ekari 50			maji, umeme na barabara za ndani.
3.	Kigadye	Ekari 8,913	Viwanda vya nafaka/ mazao na kilimo cha mazao	Limepimwa	Halina fidia	Kufanya “master plan” ya eneo Kuweka miundombinu ya barabara, umeme na maji

Mkakati wa Halmashauri Kufikia Uchumi wa Viwanda

- i. Kusimamia eneo la uwekezaji wa viwanda vya mazao/ nafaka na kilimo cha mazao ya chakula na biashara shamba la Kilimo Kwanza (Shamba 209) lenye ukubwa wa ekari 8,913 ambalo tayari limeshapimwa na limeanza kutumika kwa shughuli za kilimo.
- ii. Kusimamia eneo lililotengwa kwaajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari lililopo chini ya Kituo cha Uwekezaji Nchini (TIC) lenye ukubwa wa hekta 48,017. Ambapo hadi sasa Halmashauri imemuandikia barua Katibu Tawala (M) Kigoma yenye Kumb.Na.KSDC/L.20/4/296 ya tarehe 14/09/2017 kushauri na kuomba eneo hilo apewe mwekezaji mwengine baada ya Kigoma Sugar kushindwa kuliendeleza eneo hilo.
- iii. Kusimamia eneo lililotengwa kwaajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa lenye ukubwa wa hekta 85 (ekari 212.5), ambapo hadi sasa SIDO wametengewa ekari 50 na LIC wametengewa ekari 50. Na Halmashauri inaendelea kutafuta utaratibu wa kulipima eneo na kuliwekea miundombinu ya maji na umeme
- iv. Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kwaajili ya kuzalisha mazao yatakayotosheleza kwa mahitaji ya viwanda kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo.
- v. Kufanya manunuzi ya matrekta, mashine na vifaa vya kisasa kwaajili ya uzalishaji mkubwa wa mazao yatakayotumika kwenye viwanda kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa maendeleo.
- vi. Kufanya matengenezo ya miundombinu ya barabara, maji na umeme kwa kushirikiana na serikali kuu na wadau mbali mbali wa maendeleo ili kuboresha miundombinu ya ujenzi wa viwanda.
- vii. Kuendeleza ujenzi wa chuo cha ufundi cha Nyamidahi VTC kwa kushirikiana na serikali kuu na wadau mbali mbali wa maendeleo kwaajili ya kupata vijana/ watu wenye ujuzi katika sekta ya viwanda.

HALMASHAURI YA WILAYA KAKONKO

TAARIFA YA TAKWIMU ZA VIWANDA NA MIKAKA YA KUJENGA UCHUMI WA VIWANDA

Jedwali Na. 1 : Takwimu za Miradi ya Viwanda (Vidogo/vya Kati/vikubwa)

N a.	Aina ya Kiwanda	Idadi	Mahali unapotelekezwa (Wilaya/Kata)	Kiasi cha ajira zinazotarajiwa/zilizopo	Hatua iliyofikiwa
1.	Nafaka/ Mazao	1	Kata ya Kakonko mjini	Ajira za kudumu 16, na ajira za muda 34 jumla ajira 50	Kiwanda kiko kwenye hatua ya ukamillishaji wa ufungaji Mashine. Uzalishaji unatarajiwa kuanza muda wowote.
2.	Mafuta	1	Kata ya Kakonko Mjini	Ajira watu 5	Kiwanda kinazalisha Mafuta ya Alizeti tangu mwaka 2013
3.	Mazao ya Misitu	1	Kata ya Kakonko Mjini	Ajira za kudumu hakuna, kazi zote zinafanywa kwa ushirikiano wa wanakikundi/wanachama wapatao 120	Kiwanda kinachakata asali na Mazao yake
		10	Katika kata za Kakonko, Nyabibuye, Kaasnda	5@kiwanda watu ajira 50	Viwanda hivi vidogo vinafanya kazi ya Kuzalisha Samani mbalimbali kama vile Milano, Meza Viti, Vitanda, kabati kwa matumizi mbalimbali za ofisini na

					majumbani
4.	Vifaa vya Ujenzi	-	Hakuna	Hakuna	-
5.	Chumvi	-	Hakuna	Hakuna	-
6.	Chokaa				
7.	Madini mengineyo	1	Kuna shughuli za uchimbaji mdogo unaendelea katika kata za Nyamtukuza, Muhange na kiga	-Kuna ajira za watu 21 ambao ndiyo wanaotambulika kwa mujibu wa ofisi za Madini Mkoa kuwa na Leseni za uchimbaji wa Madini aina ya Dhahabu katika maeneo tajwa	Shughuli zinaendelea kwa kutumia dhana duni
8.	Maji/Vinywaji		Hakuna	Hakuna	
9.	Vinginevyo:		Hakuna	Hakuna	
	• Vifungashi o				
	• Mikate	1	Kata ya Kakonko Mjini	03	Kinazalisha mikate
	•Viwanda vya kushona nguo/mafundi cherehani	6	Kata za Kakonko mjini, Kasanda na Kiziguzigu	5@kiwanda sawa na ajira ya watu 30	Vikundi vidogo vya watu kuanzia 5 na kuendelea vimejiunga pamoja na kufanya kazi za ufundi wa ushonaji

Jedwali Na. 2: Maeneo Yaliyotengwa Kwa ajili ya Viwandana Uwekezaji

Na.	Jina la Eneo lililotengwa	Ukubwa wa eneo/ Aina ya viwanda vinavyokusudiwa	Hali yake (Limepimwa/halijapimwa/ taarifa za ulipaji fidia)	Maelezo/Mkakati
1	Ibuga Industrial area	Eneo la ekari 30 ambapo viwanda vikubwa na vya kati vinatarajiwa kujengwa.	Upimaji wa awali umefanyika yaani Demacation umefanyika.	Halmashauri ya Wilaya Kakonko imeweka kwenye bajeti ya 2017/2018 gharama za kulipa fidia. Aidha Mradi wa kuboresha Mazingira ya Biashara na uwekezaji

2	SIDO	Ekari 20 zimetengwa kwa ajili ya viwanda vidogo	Eneo linahitaji fidia	(LIC) imeonesha nia ya kusaidia upimaji wa eneo hilo baada ya Halmashauri kulipa fidia.
---	------	---	-----------------------	---

Mkakati wa Halmashauri katika kufikia Uchumi na Viwanda

- ❖ Kuendelea kuhamasisha wananchi juu ya uwepo wa fursa uanzishwaji wa viwanda vidogo hasa vya kusindika Mazao wanayoyazalisha katika maeneo yao
- ❖ Kuboresha Mazingira ya Biashara na uwekezaji, hasa kuhakikisha kuwa maeneo yaliyotengwa yanafikika kiurahisi na muda wowote. Aidha kuhakikisha uwepo wa huduma za kijamii zile muhimu kama umeme na maji vitu ambavyo ni muhimu katika kiwanda vinakuwepo.
- ❖ Kushirikiana na wadau wa Biashara kama vile TANTRADE kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Wilaya ya Kakonko ndani na nje ya nchi.
- ❖ Halmashauri kuendelea kutangaza fursa zilizopo kupita majarida, vyombo vya habari kama Redio na Tovuti ya Halmashauri.

MIPANGO YA BAADAYE KWA YA WILAYA YA KAKONKO KUHAKIKISHA INATEKELEZA KAULI MBIO YA KUFIKIA UCHUMI WA VIWANDA

Katika kutekeleza agizo la Mh.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha nchi inafikia uchumi wa Viwanda, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imejiwekea mikakati ifuatayo

1. Kupitia idara ya kilimo, ushirika na umwagiliaji imepanga kuendelea kutoa elimu ya kwa wakulima katika Wilaya nzima ili kuongeza uzalishaji wa Mazao ya Biashara ambayo yatatumika kama malighafi za kuendesha viwanda vilivyopo na vile vinavyotarajiwa kuanzishwa, Mazao ambayo yanatarajiwa kuongeza uzalishaji ni pamaoja na:
 - a. a.)Pamba
 - b. b.) Kahawa
 - c. c.) Alizeti
 - d. d.) Muhogo zao hutomika kama zao la Biashara na Chakula
 - e. e.) Mpunga/chakula na Biashara
2. Kuendelea kushirikiana na SIDO katika swala zima la utoaji wa elimu ya usindikaji kwa kutumia zana rahisi zinazopatikana SIDO.
3. Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wa maendeleo kuhakikisha kuwa, fidia inalipwa kwa eneo lililengwa kwa ajili hiyo
4. Kwa kushirikiana na serikali, kuhakikisha kuwa Uchimbaji wa madini unaoendelea unarasimishwa ili kuongeza idadi ya Viwanda katika Wilaya lakini pia kuleta tija kwa Halmashauri na kwa Serikali.

HALMASHAURI YA WILAYA UVINZA.

Jedwali Na.1: Takwimu za Miradi ya Viwanda(Vidogo/vya Kati/Vikubwa).

NA	Aina ya Kiwanda.	Idadi	Mahali unapotekelezwa (Wilaya/Kata).	Kiasi cha ajira zinzohitajika/zi lizopo.	Hatua iliyofikiwa.
1	Nafaka/mazao.	0	0	0	0
2	Mafuta	04	Ilagala.	20	Vinaendelea.
3	Mazao ya misitu.	02	Uvinza.	20	Vinaendelea.
4	Vifaa vya ujenzi	0	0	0	0
5	Chumvi	04	Uvinza.	61	Vinafanya kazi.
6	Chokaa	08	Kazuramimba/Mwamila.	50	Vinaendelea.
7	Madini/mengineyo	0	0	0	Tafiti za kina zinafanyika.
8	Maji na Vinywaji	0	0	0	0
9	Vinginevyo	0	0	0	0

Jedwali Na.2: MAENEO YALIYOTENGWA KWA AJILI YA VIWANDA.

NA	Jina la eneo liliotengwa	Ukubwa wa eneo/aina ya viwanda vinavyokusudiwa	Hali yake (limepimwa/halijapimwa/taarifa za ulipaji fidia)	maelezo/mkakati
1.	Lugufu.	Ekari 53	Halijapimwa.	Mchoro umetoka na upimaji utafanyika.
2.	Ilunde.	Ekari 500	Halijapimwa	Litapimwa wakati wa zoezi la upimaji vitalu vya mifugo.
3.	Mto malagarasi.	Ekari 12,500	Halijapimwa	Mwekezaji akipatikana na akalipa fidia litapimwa.

MKAKATI WA HALMASHAURI KATIKA KUFIKIA UCHUMI WA VIWANDA.

- Halmashauri imetenga kiasi cha Ekari 13,053 kwa ajili ya Viwanda na shughuli za Uwekezaji.
- Wananchi pamoja na Wanasiasa wakubali kuruhusu wawekazaji katika maeneo yao.
- Kuboresha miundo mbinu katika maeneo ya Uwekezaji mfano Umeme, Maji na Biashara.
- Kuendelea kuhamasisha Wananchi/Wakulima kulima mazao ya chakula na Biashara.
- Kufanya utafiti wa Takwimu halisi wa malighafi za kulisha viwanda mfano Maziwa, Mafuta, Madini pamoja na mazao ya nafaka.